MINISTRY OF EDUCATION

# UPPER PRIMARY LEVEL DESIGNS

## LEARNING AREA: KISWAHILI

# GREDI YA TANO

NOVEMBER 2019

KENYA INSTITUTE OF CURRICULUM DEVELOPEMENT

## Kauli Kiini

Mwanafunzi wa lugha ya Kiswahili katika shule ya msingi daraja la juu atajenga stadi na umahiri ufaao kuwasiliana, kutangamana na kushiriki katika miktadha mbalimbali ya kitaifa, kikanda na kimataifa kwa kutumia lugha kuzungumza na kuandika. Mwanafunzi anahitaji kujifunza kunga za Kiswahili ili kuitumia lugha hii kama wenzo wa ujifunzaji. Aidha, mwanafunzi hufunzwa Kiswahili ili kushiriki na kukichangamkia katika hali zake mbalimbali. Hili humwezesha kujenga stadi za kimsingi za kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika. Kwa kujifunza sarufi na matumizi ya Kiswahili kimuktadha, mwanafunzi anaweza kuwasiliana kwa ufasaha, umahiri na kwa namna ambayo itaimarisha utangamano darasani na katika ulimwengu mpana. Nadharia ya sarufi bia ya Noam Chomsky (1965), inaeleza kuwa binadamu ana uwezo asilia wa kuvimudu vipengele vya kisarufi. Uwezo huu huchangia katika ukuaji wa lugha wa mwanafunzi na hivyo kumfanya mzungumzaji stadi wa lugha anayeweza kubaini matumizi sahihi na yasiyo sahihi.

## Matokeo Tarajiwa ya Kijumla katika Somo la Kiswahili, Kiwango cha Shule ya Msingi Daraja la Juu

Kufikia mwisho wa shule ya msingi daraja la juu, mwanafunzi aweze:

a) kusikiliza kwa makini na kuitikia ipasavyo kwa Kiswahili katika miktadha mbalimbali ya mawasiliano

b) kuzingatia kanuni za lugha kuwasiliana kiubunifu kwa njia ya mazungumzo na maandishi

c) kujieleza kwa ufasaha katika miktadha mbalimbali

d) kusoma kwa ufasaha na kufahamu matini mbalimbali yaliyochapishwa na ya kidijitali na kutumia maarifa anayoyapata katika mazingira tofauti maishani

e) kutumia hati za kimaandishi na mfumo wa kidijitali kuwasiliana ipasavyo kwa kuzingatia mitindo na miundo husika katika miktadha mbalimbali

f) kuchangamkia matumizi ya Kiswahili kama lugha rasmi na ya taifa katika mawasiliano ya kila siku.

<table>
<tr><th colspan="5">1.0 MAPISHI</th></tr>
<tr><th>MADA</th><th>MADA NDOGO</th><th>MATOKEO MAALUMU YANAYOTARAJIWA</th><th>MAPENDEKEZO YA SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI</th><th>MASWALI DADISI</th></tr>
<tr><td>1.1 Kusikiliza na Kuzungumza</td><td>1.1.1 Matamshi Bora: Silabi na Vitanzandimi<br>-Sauti f/v, s/z, l/r/ na th/dh<br><br>(Vipindi 4)</td><td>Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua silabi zinazotokana na sauti zinazokaribiana katika maneno<br>b) kutamka silabi zinazotokana na sauti zinazokaribiana kimatamshi<br>c) kutamka vitanzandimi vinavyoundwa kwa silabi za sauti zinazokaribiana kimatamshi ili kuimarisha mawasiliano<br>d) kuunda vitanzandimi vyenye maana kutokana na sauti zinazokaribiana kimatamshi<br>e) kuchangamkia kukariri vitanzandimi vinavyoundwa kwa silabi za sauti zinazokaribiana kimatamshi ili kuimarisha matamshi yake.</td><td>Mwanafunzi:<br>• atambue silabi za sauti lengwa kutokana na maneno kwenye vitabu, ubaoni au kwa kutumia vifaa vya kiteknolojia<br>• asikilize silabi za sauti f/v, s/z, l/r/ na th/dh zikitamkwa na mwalimu, mgeni mwalikwa au kutoka kwa vifaa vya kiteknolojia (k.v. kinasasauti)<br>• atamke silabi za sauti lengwa akiwa peke yake, wawiliwawili au katika vikundi<br>• asikilize vitanzandimi vinavyoundwa kutokana na maneno yenye sauti lengwa vikikaririwa (k.m. shirika la reli la Rwanda larejelea shughuli zake rasmi n.k.)<br>• aunde vitanzandimi vinavyotokana na sauti husika akiwa peke yake, wawiliwawili na katika vikundi<br>• aunde vitanzandimi kwenye vifaa vya kidijitali na kushirikiana na wenzake mitamboni kuvirekebisha<br>• kusakura mtandaoni ili kupata vitanzandimi zaidi vyenye sauti lengwa</td><td>1. Je, unajua maneno gani yenye silabi zinazokanganya kimatamshi?<br>2. Je, Unajua vitanzandimi gani vyenye silabi zinazokanganya kimatamshi?</td></tr>
<tr><td colspan="5">Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:<br>• Mawasiliano na ushirikiano – unakuzwa wanafunzi wanaposhirikiana katika kutamka silabi na kuunda vitanzandimi<br>• Ujuzi wa kidijitali – unakuzwa wakati vifaa vya kiteknolojia vinapotumiwa kusikiliza sauti na kuunda vitanzandimi mtandaoni<br>• Hamu ya ujifunzaji – inakuzwa mwanafunzi anapoendelea kukariri vitanzandimi na kusakura mtandaoni ili kupata vitanzandimi zaidi<br>• Ubunifu – unakuzwa mwanafunzi anapounda vitanzandimi<br>• Kujiamini- kunakuzwa mwanafunzi anapotamka kwa usahihi silabi zinazotokana na sauti lengwa na kuunda vitanzandimi sahihi<br>• Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo- unakuzwa mwanafunzi anapofikiria kuhusu vitanzandimi atakavyounda vyenye sauti lengwa</td></tr>
</table>

| Uhusiano na masuala mtambuko: | Uhusiano na Maadili: |
|---|---|
| • Masuala mtambuko anuwai kutokana na vitanzandimi vinavyoelekeza utoaji wa maelezo kuhusu masuala hayo k.v. utunzaji wa mazingira, ujuzi wa matumizi ya fedha, afya bora na utunzaji wa wanyama. | • Heshima na Umoja – mwanafunzi anapofanya kazi katika vikundi<br>• Maadili mbalimbali yaliyolengwa katika vitanzandimi k.v. upendo, uaminifu, uzalendo, uadilifu, amani na haki za kibinadamu. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>• English, Indigeneous Languages, Arabic na Music – masomo haya hurejelea matamshi bora | **Mapendekezo ya shughuli za huduma za kijamii zinazochangia ujifunzaji:**<br>• Kuwashirikisha wenzake shuleni na nyumbani katika kukariri vitanzandimi ili kuimarisha matamshi bora |

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kutambua na kutamka silabi za sauti lengwa ipasavyo. | Mwanafunzi anatambua na kutamka silabi za sauti lengwa ipasavyo na kwa urahisi | Mwanafunzi anatambua na kutamka silabi za sauti lengwa ipasavyo | Mwanafunzi anatambua silabi za sauti lengwa na kutamka baadhi yazo | Mwanafunzi anatambua baadhi ya silabi za sauti lengwa na kutamka baadhi yazo |
| Kukariri vitanzandimi ipasavyo | Mwanafunzi anakariri vitanzandimi vilivyoundwa kutokana na silabi za sauti lengwa ipasavyo na kwa urahisi. | Mwanafunzi anakariri vitanzandimi vilivyoundwa kutokana na silabi za sauti lengwa ipasavyo. | Mwanafunzi anakariri baadhi ya vitanzandimi vilivyoundwa kutokana na silabi za sauti lengwa ipasavyo. | Mwanafunzi anajaribu kukariri baadhi ya vitanzandimi vilivyoundwa kutokana na silabi za sauti lengwa. |
| Kuunda vitanzandimi vyenye maana kutokana na silabi za sauti lengwa kwa ufasaha | Mwanafunzi anaunda vitanzandimi vyenye maana kutokana na silabi za sauti lengwa kwa ufasaha na urahisi | Mwanafunzi anaunda vitanzandimi vyenye maana kutokana na silabi za sauti lengwa kwa ufasaha | Mwanafunzi anaunda baadhi ya vitanzandimi vyenye maana kutokana na silabi za sauti lengwa kwa ufasaha | Mwanafunzi anajaribu kuunda baadhi ya vitanzandimi kutokana na silabi za sauti lengwa |

| MADA | MADA NDOGO | MATOKEO MAALUMU YANAYOTARAJIWA | MAPENDEKEZO YA SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI | MASWALI DADISI |
|---|---|---|---|---|
| **1.2 Kusoma** | **1.2.1 Kusoma kwa ufahamu:** Kifungu cha Hadithi<br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua msamiati wa suala lengwa uliotumika katika kifungu ili kuimarisha ufahamu<br>b) kutumia msamiati lengwa kwa usahihi katika sentensi<br>c) kusoma kifungu cha hadithi kwa kuzingatia ujumbe, matukio na wahusika<br>d) kuonyesha uelewa wa kifungu kwa kutoa muhtasari na kujibu maswali<br>e) kujenga mazoea ya usomaji bora katika maisha ya kila siku. | Mwanafunzi:<br>• atambue msamiati wa suala lengwa (k.v. *vyakula, viungo vya kupikia, njia za kupika na vifaa vya kupikia)* kwa kutumia kadi za maneno, chati, mti maneno au kifaa cha kidijitali<br>• ashiriki katika vikundi kujadili na kutumia msamiati wa suala lengwa katika sentensi<br>• asome kifungu kuhusu suala lengwa kwenye kitabu au kwenye tarakilishi akiwa peke yake, wawiliwawili au katika vikundi<br>• atoe muhtasari kuhusu kifungu alichosoma<br>• ajibu maswali kutokana na kifungu alichosoma.<br>• Asome vifungu mtandaoni kuhusu suala lengwa na kujadiliana na wenzake kuhusu ujumbe ulioyomo | 1) Kusoma kuhusu mapishi kuna umuhimu gani?<br>2) Ni hadithi gani umewahi kuisoma kuhusu mapishi? |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano –unakuzwa mwanafunzi anaposhiriki katika mijadala na kazi za vikundi
- Ujuzi wa kidijitali –unakuzwa wakati vifaa vya kiteknolojia vinapotumiwa kusoma kifungu
- Hamu ya ujifunzaji –unakuzwa mwanafunzi anaposakura mtandaoni ili kusoma vifungu zaidi kuhusu suala lengwa

| | |
|---|---|
| **Uhusiano na masuala mtambuko:**<br>• Uraia - kutokana na kufanya kazi pamoja katika vikundi<br>• Stadi za maisha - mwanfunzi anapojifunza kuhusu mapishi<br>• Afya bora – kutokana na vifungu vinavyoeleza kuhusu mapishi | **Uhusiano na Maadili:**<br>• Heshima – mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika shughuli za vikundi<br>• Umoja – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za vikundi |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>• English, Indigeneous Language na Arabic – masomo haya hushughulikia vifungu vya hadithi na upanuzi wa msamiati | **Mapendekezo ya shughuli za huduma za kijamii zinazochangia ujifunzaji:**<br>• Kuwahamasisha wenzake shuleni na nyumbani kuhusu suala la mapishi |

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kutambua na kutumia msamiati wa suala lengwa katika tungo kwa usahihi | Mwanafunzi anatambua msamiati wa suala lengwa na kuutumia katika tungo kwa usahihi na urahisi | Mwanafunzi anatambua msamiati wa suala lengwa na kuutumia katika tungo kwa usahihi | Mwanafunzi anatambua baadhi ya msamiati wa suala lengwa na kuutumia katika tungo kwa usahihi. | Mwanafunzi anatambua baadhi ya msamiati wa suala lengwa na kutumia baadhi ya msamiati huo katika tungo. |
| Kusoma kwa kuzingatia ujumbe, matukio na wahusika katika kifungu kwa ufasaha | Mwanafunzi anasoma kwa kuzingatia ujumbe, matukio na wahusika katika kifungu kwa ufasaha na urahisi | Mwanafunzi anasoma kwa kuzingatia ujumbe, matukio na wahusika katika kifungu kwa ufasaha | Mwanafunzi anasoma kwa kuzingatia ujumbe, matukio na wahusika katika kifungu | Mwanafunzi anajaribu kusoma sehemu za kifungu bila kuzingatia ujumbe, matukio na wahusika |
| Kutoa muhtasari wa kifungu kwa usahihi | Mwanafunzi anatoa muhtasari wa kifungu kwa usahihi na urahisi | Mwanafunzi anatoa muhtasari wa kifungu kwa usahihi | Mwanafunzi anatoa muhtasari wa kifungu | Mwanafunzi anajaribu kutoa muhtasari wa kifungu |

<table>
<tr><th>MADA</th><th>MADA NDOGO</th><th>MATOKEO MAALUMU YANAYOTARAJIWA</th><th>MAPENDEKEZO YA SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI</th><th>MASWALI DADISI</th></tr>
<tr><td>1.3 Kuandika</td><td>1.3.1 Kuandika: Insha ya wasifu (Vipindi 2)</td><td>Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua insha ya wasifu kwa kuzingatia mtindo na muundo wake<br>b) kuandika insha ya wasifu kwa ubunifu ili kujenga maelezo yenye kutoa picha dhahiri<br>c) kufurahia kutunga insha bora ili kuimarisha mazoea ya kuandika</td><td>Mwanafunzi:<br>• atambue insha ya wasifu kwa kurejelea vielelezo vya insha zilizoandikwa kwenye matini mbalimbali au tarakilishi<br>• asome vielelezo vya insha ya wasifu vilivyoandikwa katika matini mbalimbali au tarakilishi<br>• ashirikiane na wenzake kujadili mada na muundo wa insha ya wasifu<br>• akishirikiane na wenzake katika vikundi ili kubainisha na kujadili vidokezo vifaavyo vya mada lengwa.<br>• aandike insha ya wasifu isiyopungua maneno 150 inayohusu mada lengwa (k.v. Mpishi nimpendaye) kwa kuzingatia, anwani, mpangilio mzuri wa mawazo, hati safi, kanuni za kisarufi (k.v uakifishaji mwafaka na tahajia) na kwa lugha ya kiubunifu inayojumuisha methali, tashbihi na nahau alizojifunza awali.<br>• aandike insha ya wasifu mtandaoni na kuisambaza kwa wenzake na mwalimu ili kuisoma na kuitathmini<br>• awasomee wenzake insha aliyoandika ili kumpa motisha kuandika zaidi.</td><td>1. Insha ya wasifu ni gani?<br>2. Unazingatia nini unapoandika insha ya wasifu?</td></tr>
<tr><td colspan="5">Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:<br>• Mawasiliano na ushirikiano – unakuzwa wanafunzi wanaposhiriki katika mijadala na kazi za vikundi<br>• Ujuzi wa kidijitali – unakuzwa wakati vifaa vya kiteknolojia vinapotumiwa kuandika insha mtandaoni na kurejelea kielelezo cha insha ya wasifu<br>• Ubunifu – unajengeka mwanafunzi anapoandika insha ya wasifu</td></tr>
<tr><td colspan="3">Uhusiano na masuala mtambuko:<br>• Uraia - kutokana na kufanya kazi pamoja katika vikundi.</td><td colspan="2">Uhusiano na Maadili:<br>• Heshima na adabu - hasa katika shughuli za vikundi<br>• Insha ya wasifu yaweza kulenga watu ambao wanajulikana kwa uaminifu, uwajibikaji, upendo na uzalendo.</td></tr>
<tr><td colspan="3">Uhusiano na masomo mengine:<br>• English na Indigeneous Languages – Masomo haya yanashughulika mada ya kuandika.</td><td colspan="2">Mapendekezo ya shughuli za huduma za kijamii zinazochangia ujifunzaji:<br>• Kuwahamasisha wenzake shuleni na nyumbani kuhusu umuhimu wa uandishi bora katika mawasiliano</td></tr>
</table>

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kutambua insha ya wasifu kwa kuzingatia mtindo na muundo wake | Mwanafunzi anatambua kwa urahisi na wepesi insha ya wasifu kwa kuzingatia mtindo na muundo wake | Mwanafunzi anatambua kwa urahisi insha ya wasifu kwa kuzingatia mtindo na muundo wake | Mwanafunzi anatambua insha za wasifu kwa kuzingatia mtindo na muundo wake | Mwanafunzi ana changamoto kutambua insha ya wasifu kwa kuzingatia mtindo na muundo wake |
| Kuandika insha ya wasifu kwa ubunifu akizingatia kanuni zifaazo za lugha na mpangilio mzuri wa mawazo | Mwanafunzi anaandika insha ya wasifu kwa kuzingatia kanuni zifaazo za lugha, mpangilio mzuri wa mawazo na kwa ubunifu wa hali ya juu. | Mwanafunzi anaandika insha ya wasifu kwa kuzingatia kanuni zifaazo za lugha, mpangilio mzuri wa mawazo na kwa ubunifu | Mwanafunzi anaandika insha ya wasifu kwa kuzingatia kanuni za lugha na mpangilio mzuri wa mawazo. | Mwanafunzi anaandika insha ya wasifu kwa kuzingatia baadhi ya kanuni za lugha. |

| MADA | MADA NDOGO | MATOKEO MAALUM YANAYOTARAJIWA | MAPENDEKEZO YA SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI | MASWALI DADISI |
|---|---|---|---|---|
| **1.4 Sarufi** | **1.4.1 Aina za Nomino:**<br>Nomino za Pekee<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua nomino za pekee kwenye sentensi au vifungu vya maneno<br>b) kutunga sentensi kwa kutumia nomino za pekee ili kukuza matumizi ya lugha sahihi<br>c) kuchangamkia kutumia nomino za pekee katika utungaji wa sentensi na kujaza mapengo kwenye vifungu. | Mwanafunzi:<br>• atambue nomino za pekee (*k.v. Kisumu, Mei, Rabuka, Alhamisi na Yohana*) kwenye tarakilishi, kapu maneno, mti maneno, kadi maneno au chati<br>• akiwa na wenzake ataje nomino za pekee kama vile za majina ya mji, majina ya mito, majina ya watu na majina ya miezi<br>• atambue nomino za pekee katika sentensi kwenye vitabu, tarakilishi, chati kwa kuzipigia mstari au kukolezea rangi<br>• ajaze mapengo kwa kutumia nomino za pekee<br>• atunge sentensi kwa kutumia nomino za pekee akiwa peke yake, wawiliwawili au vikundi | 1. Nomino za pekee zinahusu nini?<br>2. Ni nomino zipi za pekee unazozijua? |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano – unakuzwa mwanafunzi anaposhiriki katika kazi za vikundi
- Ujuzi wa kidijitali – unakuzwa wakati vifaa vya kiteknolojia vinapotumiwa katika kutambua nomino za pekee
- Ubunifu – unakuzwa mwanafunzi anapotunga sentensi sahihi akitumia nomino za pekee.
- Kujiamini - kunakuzwa mwanafunzi anapofaulu kutambua nomino za pekee na kuzitungia sentensi sahihi.

| **Uhusiano na Masuala Mtambuko** | **Uhusiano na Maadili** |
|---|---|
| • Masuala mtambuko anuwai kutokana na sentensi zinazoelekeza utoaji wa maelezo kuhusu masuala hayo k.v. usalama, utunzaji wa mazingira, afya bora na utunzaji wa wanyama | • Uwajibikaji: mwanafunzi anapofanya kazi ya darasani<br>• Uzalendo na heshima: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake na kuheshimu maoni ya wengine<br>• Maadili mbalimbali yanaweza kulengwa katika sentensi k.v. upendo, uaminifu, uzalendo, amani na umoja. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine** | **Mapendekezo ya shughuli za huduma za Kijamii zinazochangia ujifunzaji**: |
| • English na Indigeneous Languages – masomo haya yanashughulikia mada ya nomino | • Kushirikisha wengine katika kutaja nomino za pekee zinazohusu miji, watu, mito n.k. |

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kutambua nomino za pekee na kuzitumia kutunga sentensi sahihi kwa urahisi | Mwanafunzi anatambua nomino za pekee kwa wepesi na kuzitumia kwa urahisi kutunga sentensi sahihi | Mwanafunzi anatambua nomino za pekee na kuzitumia kutunga sentensi sahihi | Mwanafunzi anatambua baadhi ya nomino za pekee na kuzitumia kutunga sentensi sahihi | Mwanafunzi anatambua baadhi ya nomino za pekee na kutumia baadhi ya nomino alizotambua kutunga sentensi sahihi |

<table>
<tr><th>MADA</th><th>MADA NDOGO</th><th>MATOKEO MAALUM YANAYOTARAJIWA</th><th>MAPENDEKEZO YA SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI</th><th>MASWALI DADISI</th></tr>
<tr><td>1.4 Sarufi</td><td>1.4.2 Aina za Nomino:<br>Nomino za kawaida<br>(Vipindi 2)</td><td>Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua nomino za kawaida kwenye sentensi au vifungu vya maneno<br>b) kutunga sentensi kwa kutumia nomino za kawaida ili kukuza matumizi sahihi ya lugha<br>c) kufurahia kutumia nomino za kawaida katika utungaji wa sentensi na kujaza mapengo kwenye vifungu.</td><td>Mwanafunzi:<br>• atambue nomino za kawaida kwenye kadi au kapu la maneno (k.v.mtu, mtoto, darasa, ukuta, mwalimu, meza na kiti)<br>• akiwa na wenzake ataje nomino za kawaida<br>• atambue nomino za kawaida katika sentensi kwa kuzipigia mistari au kuzikolezea rangi kwenye tarakilishi<br>• atumie nomino za kawaida kujaza mapengo kwenye sentensi<br>• atunge sentensi kwa kutumia nomino za kawaida akiwa peke yake wawiliwawili au kwenye vikundi</td><td>1. Je, ni vitu gani vipatikanavyo katika mazingira yako?<br>2. Ni vitu gani vinavyotumiwa katika mapishi mbalimbali?</td></tr>
<tr><td colspan="5">Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa<br>• Ubunifu - anapotunga sentensi na kujaza mapengo<br>• Mawasiliano na ushirikiano - mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika vikundi kutaja nomino na kutunga sentensi</td></tr>
<tr><td colspan="3">Uhusiano na Masuala Mtambuko<br>• Uraia - hasa unatokea kwenye kazi za vikundi wakati mwanafunzi anashirikiana na wenzake<br>• Masuala mtambuko anuwai kutokana na sentensi zinazotoa maelezo kuhusu masuala hayo k.v. utunzaji wa mazingira, afya bora na utunzaji wa wanyama.</td><td colspan="2">Uhusiano na Maadili<br>• Upendo - mwanafunzi anapotagamana na wenzake kwenye vikundi<br>• Heshima - mwanafunzi anapothamini maoni ya wengine kwenye kikundi<br>• Maadili mbalimbali yanaweza kulengwa katika sentensi k.v. upendo, uaminifu, uzalendo, amani na umoja.</td></tr>
<tr><td colspan="3">Uhusiano na Masomo Mengine<br>• English na Indigeneous Languages - masomo haya yanashughulikia mada ya nomino</td><td colspan="2">Mapendekezo ya shughuli za huduma za Kijamii zinazochangia ujifunzaji:<br>• Mwanafunzi anarejelea nomino za kawaida katika mazingira yake</td></tr>
</table>

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kutambua nomino za kawaida na kuzitumia kutunga sentensi sahihi | Mwanafunzi anatambua nomino za kawaida na kuzitumia kwa urahisi kutunga sentensi sahihi. | Mwanafunzi anatambua nomino za kawaida na kuzitumia kutunga sentensi sahihi. | Mwanafunzi anatambua baadhi ya nomino za kawaida na kuzitumia kutunga sentensi sahihi. | Mwanafunzi anatambua baadhi ya nomino za kawaida na kutumia baadhi ya nomino alizotambua kutunga sentensi sahihi. |

<table>
<tr><th colspan="5">2.0 HUDUMA YA KWANZA</th></tr>
<tr><th>MADA</th><th>MADA NDOGO</th><th>MATOKEO MAALUM YANAYOTARAJIWA</th><th>MAPENDEKEZO YA SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI</th><th>MASWALI DADISI</th></tr>
<tr><td>2.1 Kusikiliza na Kuzungumza</td><td>2.1.1 Maamkuzi na Maagano<br>(Vipindi 2)</td><td>Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua aina mbalimbali za maamkuzi na maagano katika mawasiliano<br>b) kueleza maamkuzi na maagano yanayotumika katika miktadha mbalimbali<br>c) kutumia aina mbalimbali za maamkuzi na maagano katika mawasiliano<br>d) kuchangamkia maamkuzi na maagano katika mahusiano.</td><td>Mwanafunzi:<br>• atambue maamkuzi (k.v. shikamoo, Habari za utokako? Habari za adhuhuri? Habari za jioni?) kutoka kwenye chati, ubao au vifaa vya kidijitali, michoro na picha<br>• ashiriki kujadiliana na mwenzake au katika vikundi maamkuzi yanayolengwa na matumizi yake<br>• atambue maagano (k.v lala salama, safari njema, alamsiki) kutoka kwenye chati, ubao au vifaa vya kidijitali, michoro na picha<br>• ashirikiane na wenzake kuigiza maamkuzi na maagano lengwa<br>• atazame watu wakiamkuana na kuagana katika vifaa vya kidijitali<br>• aambatanishe maamkuzi na maagano na majibu sahihi</td><td>1. Je, watu husalimiana vipi katika jamii?<br>2. Je, watu huagana vipi katika jamii?</td></tr>
<tr><td colspan="5">Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa<br>• Mawasiliano na ushirikiano- mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kuigiza maamkuzi na maagano<br>• Ujuzi wa kidijitali- mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kujifunzia<br>• Kujiamini- anapotumia maamkuzi na maagano ipasavyo</td></tr>
<tr><td colspan="3">Uhusiano na Masuala Mtambuko<br>• Uraia - kupitia kuamkua na kujibu maamkuzi</td><td colspan="2">Uhusiano na Maadili<br>• Heshima- maamkuzi huimarisha heshima<br>• Upendo - maamkuzi huashiria upendo<br>• Umoja - maamkuzi huimarisha umoja na uhusiano mwema</td></tr>
<tr><td colspan="3">Uhusiano na Masomo Mengine<br>• English na Indigenous Languages- masomo haya yanashughlikia maamkuzi na maagano</td><td colspan="2">Mapendekezo ya shughuli za huduma za Kijamii zinazochangia ujifunzaji:<br>• Mwanafunzi awahamasishe wenzake katika jamii kuhusu jinsi ya kuamkua na umuhimu wa maamkuzi</td></tr>
</table>

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kutambua maamkuzi na maagano mbalimbali na kuyatumia katika miktadha tofautitofauti kwa ufasaha | Mwanafunzi anatambua maamkuzi na maagano mbalimbali na kuyatumia katika miktadha tofautitofauti kwa ufasaha na urahisi | Mwanafunzi anatambua maamkuzi na maagano mbalimbali na kuyatumia katika miktadha tofautitofauti kwa ufasaha | Mwanafunzi anatambua baadhi ya maamkuzi na maagano na kuyatumia katika miktadha tofauti tofauti kwa ufasaha. | Mwanafunzi anatambua baadhi ya maamkuzi na maagano na kutumia baadhi ya maamkuzi hayo kwa ufasaha. |

| MADA | MADA NDOGO | MATOKEO MAALUMU YANAYOTARAJIWA | MAPENDEKEZO YA SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI | MASWALI DADISI |
|---|---|---|---|---|
| **2.2 Kusoma** | **2.2.1 Kusoma kwa Kina:**<br>Matumizi ya Kamusi<br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua mpangilio wa maneno katika kamusi ili kupata maneno lengwa kwa urahisi<br>b) kutumia kamusi ipasavyo kutafuta maana za maneno asiyoyajua yaliyo katika matini teule ili kukuza msamiati wake<br>c) kuchangamkia kutumia kamusi katika kukuza msamiati wake. | Mwanafunzi:<br>• apange maneno aliyopewa kwenye chati, kapu maneno au mti maneno kialfabeti<br>• achague neno kutoka kapu maneno au mti maneno ili kulitafuta kwenye kamusi<br>• atumie kamusi kutafuta maana za maneno mbalimbali akiwa peke yake, wawiliwawili au katika vikundi<br>• atumie mtandao kutafuta maana za maneno | 1. Unatafutaje maana ya maneno kwenye kamusi?<br>2. Kwa nini tunatumia kamusi?<br>3. Je, ni habari zipi tunaweza kupata katika kamusi? |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anashirikiana na wenzake kutafuta maana za maneno
- Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anatumia mtandao kutafuta maana za maneno
- Hamu ya ujifunzaji – huu unajengeka mwanafunzi anapoanza kutumia kamusi kutafuta maana za maneno

| **Uhusiano na masuala mtambuko:** | **Uhusiano na Maadili:** |
|---|---|
| • Stadi za maisha – uwezo wa kujitegemea katika kutumia kamusi<br>• Uraia – uwezo wa kufanya kazi na wengine katika vikundi | • Uzalendo – hamu ya kukuza msamiati ili kuweza kutumia lugha ya Kiswahili kama lugha ya taifa |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>English na Indigenous Languages – masomo haya husisitiza matumizi mbalimbali ya kamusi | **Mapendekezo ya shughuli za huduma za kijamii zinazochangia ujifunzaji:**<br>Mwanafunzi awahamasishe wenzake shuleni na nyumbani kuhusu utumiaji sahihi wa maneno |

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kutumia kamusi kwa kuzingatia mpangilio wa maneno na kujikita katika maneno lengwa | Mwanafunzi anatumia kamusi kwa urahisi akizingatia mpangilio wa maneno na kujikita katika maneno lengwa | Mwanafunzi anatumia kamusi kwa kuzingatia mpangilio wa maneno na anajikita katika maneno lengwa | Mwanafunzi anatumia kamusi akizingatia mpangilio wa maneno bila kujikita katika maana za maneno lengwa. | Mwanafunzi anajaribu kutumia kamusi kutafuta maana za baadhi ya maneno lengwa |

<table>
<tr><th>MADA</th><th>MADA NDOGO</th><th>MATOKEO MAALUMU YANAYOTARAJIWA</th><th>MAPENDEKEZO YA SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI</th><th>SWALI DADISI</th></tr>
<tr><td>2.3 Kuandika</td><td>2.3.1 Kuandika Insha:<br>Insha za masimulizi<br>(Vipindi 2)</td><td>Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua insha ya masimulizi kwa kuzingatia ujumbe, mtindo na muundo<br>b) kuandika insha ya masimulizi kwa kufuata kanuni zifaazo<br>c) kuchangamkia utunzi mzuri wa insha ya masimulizi ili kukuza ubunifu wake</td><td>Mwanafunzi:<br>• atambue insha ya masimulizi kwa kurejelea vielelezo vya insha zilizoandikwa kwenye matini mbalimbali au tarakilishi<br>• ashiriki na wenzake kujadili mada ya insha na muundo wa insha ya masimulizi<br>• aandike insha isiyopungua maneno 150 inayosimulia kisa cha tukio linalohusiana na huduma ya kwanza kwa kuzingatia anwani, mpangilio mzuri wa mawazo, hati safi, tahajia, kanuni za kisarufi, uakifishaji mwafaka na kwa lugha ya kiubunifu<br>• aandike insha ya masimulizi mtandaoni na kuisambaza kwa wenzake na mwalimu ili kuisoma na kuitathmini<br>• awasomee wenzake insha aliyoandika ili kuitathmini.</td><td>1. Je, unazingatia nini ili kuandika insha nzuri ya masimulizi?</td></tr>
<tr><td colspan="5">Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:<br>• Mawasiliano na ushirikiano – unakuzwa wanafunzi wanaposhiriki katika mijadala na kazi za vikundi<br>• Ujuzi wa kidijitali – unakuzwa wakati vifaa vya kiteknolojia vinapotumiwa kuandika insha mtandaoni na kurejelea kielelezo cha insha ya masimulizi<br>• Ubunifu – unajengeka mwanafunzi anapoandika insha ya masimulizi<br>• Hamu ya ujifunzaji – unakuzwa mwanafunzi anapoimarisha ujuzi wake wa kutumia tarakilishi</td></tr>
<tr><td colspan="3">Uhusiano na masuala mtambuko:<br>• Uraia kutokana na kufanya kazi pamoja.</td><td colspan="2">Uhusiano na Maadili:<br>• Heshima na adabu hasa katika shughuli za vikundi<br>• Umoja – mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za vikundi</td></tr>
<tr><td colspan="3">Uhusiano na masomo mengine:<br>• English na Indigeneous Language – masomo haya yanashughulikia uandishi wa insha</td><td colspan="2">Mapendekezo ya shughuli za huduma za kijamii zinazochangia ujifunzaji:<br>• Mwanafunzi awahamasishe wenzake shuleni na nyumbani kuhusu umuhimu wa uandishi bora katika mawasiliano</td></tr>
</table>

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kuandika insha ya masimulizi kwa kuzingatia kanuni za lugha, mpangilio mzuri wa mawazo na kwa ubunifu. | Mwanafunzi anaandika insha ya masimulizi kwa kuzingatia kanuni za lugha, mpangilio mzuri wa mawazo na kwa ubunifu wa hali ya juu. | Mwanafunzi anaandika insha ya masimulizi kwa kuzingatia kanuni za lugha, mpangilio mzuri wa mawazo na kwa ubunifu | Mwanafunzi anaandika insha ya masimulizi kwa kuzingatia kanuni za lugha na mpangilio mzuri wa mawazo | Mwanafunzi anaandika insha ya masimulizi kwa kuzingatia baadhi ya kanuni za lugha |

| MADA | MADA NDOGO | MATOKEO MAALUM YANAYOTARAJIWA | MAPENDEKEZO YA SHUNGULI ZA UJIFUNZAJI | SWALI DADISI |
|---|---|---|---|---|
| **2.4 Sarufi** | **2.4.1 Aina za Nomino:** Nomino za wingi (Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze;<br>a) kutambua nomino za wingi<br>b) katika matini mbalimbali<br>c) kutumia nomino za wingi katika sentensi<br>d) kufurahia kutumia nomino za wingi katika mawasiliano. | Mwanafunzi<br>• atambue nomino za wingi (*k.m chumvi, sukari, maji, uji, mafuta na manukato*) kutoka kwenye kapu la maneno, chati, vitabu na vifaa vya kidijitali akiwa peke yake, wawiliwawili au katika kikundi<br>• atambue nomino za wingi kwa kuzipigia mistari au kuzikolezea rangi kwenye matini<br>• atumie nomino za wingi kujaza mapengo kwenye sentensi<br>• atumie nomino za wingi katika sentensi kwa kufanya mazoezi daftarini | 1. Unajua majina gani ambayo yanayohusu vitu vinavyopatikana katika wingi tu? |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**
- Mawasiliano na ushirikiano - vinakuzwa mwanafunzi anaposhiriki katika mijadala na kazi za vikund
- Kufikiri kwa kina – Anapotunga sentensi na kuzijadili na wenzake
- Ujuzi wa kidijitali - unakuzwa wakati vifaa vya kiteknolojia vinapotumiwa katika kutambua nomino za wingi

| Uhusiano na Masuala Mtambuko | Uhusiano na Maadili |
|---|---|
| • Utangamano – anaposhirikiana na wenzake kwenye kikundi<br>• Stadi za Maisha – anapokuza stadi ya kujieleza kupitia utungaji wa sentensi | • Upendo – Unakuzwa anaposhiriki kwenye vikundi<br>• Uwajibikaji – Anawajibika kukamilisha kazi zake pamoja na kutunza vifaa vya kiteknolojia kama vile tarakalishi |

| | |
|---|---|
| | • Maadili mbalimbali yaliyolengwa katika sentensi k.v. uaminifu, uzalendo, amani na umoja. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>• English na Indigenous Languages – masomo haya yanafunza nomino | **Shughuli za Huduma za Kijamii zinazochangia Ujifunzaji**<br>• Mwanafunzi anakuwa kielelezo kizuri katika kutumia lugha ya Kiswahili ipasavyo. |

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| **Viwango** / **Vigezo** | **Kuzidisha Matarajio** | **Kufikia Matarajio** | **Kukaribia Matarajio** | **Mbali na Matarajio** |
|---|---|---|---|---|
| Kutambua nomino za wingi na kuzitumia kutunga sentensi sahihi | Mwanafunzi anatambua nomino za wingi na kuzitumia kwa urahisi kutunga sentensi sahihi | Mwanafunzi anatambua nomino za wingi na kuzitumia kutunga sentensi sahihi | Mwanafunzi anatambua baadhi ya nomino za wingi na kuzitumia kutunga sentensi sahihi | Mwanafunzi anatambua baadhi ya nomino za wingi na kutumia baadhi ya nomino alizotambua kutunga sentensi sahihi |

| MADA | MADA NDOGO | MATOKEO MAALUM YANAYOTARAJIWA | MAPENDEKEZO YA SHUNGULI ZA UJIFUNZAJI | MASWALI DADISI |
|---|---|---|---|---|
| **2.4 Sarufi** | **2.4.2 Aina za Nomino:**<br>Nomino za vitenzi-jina<br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze;<br>a) kutambua nomino za vitenzi- jina kwenye kifungu cha maneno au kwenye sentensi<br>b) kutunga sentensi au vifungu vya maneno akitumia nomino za vitenzi-jina ili kukuza matumizi bora ya lugha<br>c) kufurahia kutumia nomino za vitenzi-jina katika utungaji wa sentensi na kujaza mapengo.. | Mwanafunzi:<br>• atambue vitenzi-jina kutoka kwenye kapu la maneno, vyombo vya kijiditali ( k.v. kusoma, kucheka, kula, kulia, kuandika and kadhalika.)<br>• atambue vitenzi-jina akiwa na wenzake kwa kuvipigia mistari au kuzikolezea rangi kwenye matini n.k.<br>• atumie nomino za vitenzijina kwa kujaza mapengo kwenye sentensi<br>• atunge sentensi au vifungu vya maneno kwa kutumia nomino za vitenzi-jina akiwa peke yake, wawiliwawili au katika vikudi. | 1. Ni mambo gani wewe hufanya ukiwa nyumbani?<br>2. Unapenda kufanya mambo gani darasani? |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**
- Kufikiri kwa kina – Anapotunga sentensi na kuzijadili na wenzake
- Hamu ya ujifunzaji – anaposhirikiana na wengine kwenye kazi za kikundi

| **Uhusiano na Masuala Mtambuko** | **Uhusiano na Maadili** |
|---|---|
| • Utangamano – anaposhirikiana na wenzake kwenye kikundi<br>• Uraia – Anapotagusana na wenzake wenye asili tofauti kwenye kikundi | • Upendo – Utakuzwa katika kushirikiana kwenye vikundi kufanya shughuli mbalimbali<br>• Uwajibikaji – Anawajibika kukamilisha kazi zake pamoja na kutunza vifaa vya kiteknolojia kama vile projekta na tarakalishi |
| **Uhusiano na Masomo Mengine** | **Shughuli za Huduma za Kijamii Zinazochangia Ujifunzaji** |
| • English na Indigenous Languages – masomo haya yanafunza nomino | • Mwanafunzi anapoendelea kutambua vitenzi jina katika shughuli za kila siku |

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kutambua nomino za vitenzi- jina na kuzitumia kutunga sentensi sahihi. | Mwanafunzi anatambua nomino za vitenzi - jina na kuzitumia kwa urahisi kutunga sentensi sahihi. | Mwanafunzi anatambua nomino za vitenzi - jina na kuzitumia kutunga sentensi sahihi. | Mwanafunzi anatambua baadhi ya nomino za vitenzi - jina na kuzitumia kutunga sentensi sahihi. | Mwanafunzi anatambua baadhi ya nomino za vitenzi - jina na kutumia baadhi ya nomino alizotambua kutunga sentensi sahihi. |

<table>
<tr><th colspan="5">3.0 MAPAMBO</th></tr>
<tr><th>MADA</th><th>MADA NDOGO</th><th>MATOKEO MAALUM YANAYOTARAJIWA</th><th>MAPENDEKEZO YA SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI</th><th>SWALI DADISI</th></tr>
<tr><td>3.1 Kusikiliza na Kuzungumza</td><td>3.1 Matamshi Bora: Vitendawili (Vipindi 2)</td><td>Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua vitendawili vya suala lengwa vyenye sauti zinazokaribiana kwenye orodha<br>b) kutamka maneno yenye sauti zinazokaribiana katika vitendawili lengwa<br>c) kutega na kutegua vitendawili vyenye sauti zinazokaribiana ili kujenga matamshi bora<br>d) kuchangamkia matumizi ya vitendawili vyenye sauti zinazokaribiana kama njia ya kujenga utamkaji bora wa maneno.</td><td>Mwanafunzi:<br>• atambue vitendawili vya mapambo vyenye maneno ya sauti f/v, s/z, l/r, th/dh katika chati, ubao au vifaa vya kidijitali (k.m Wafaa lakini wavaliwa bila matumizi maalum (Mtandio), Ananitazama, hasemi hasikii (Picha), Lapendeza rangi lakini halikai (Ua). Dhahabu yangu ya thamani haisimami (Mkufu.)<br>• ashiriki katika kutega na kutegua vitendawili vyenye sauti zinazokaribiana wakiwa wawiliwawili au katika vikundi<br>• asikilize vitendawili vikitegwa na kuteguliwa kupitia vyombo vya kidijitali.</td><td>1. Je, ni vitendawili gani unavyovijua?</td></tr>
<tr><td colspan="5">Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa<br>• Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anashiriki katika kutega na kutegua vitendawili kwenye vikundi<br>• Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo – unakuzwa mwanafunzi anapofikiria kuhusu majibu ya vitendawili<br>• Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kusikiliza vitendawili vikitegwa na kuteguliwa<br>• Kujiamini – mwanafunzi anapoweza kutega na kutegua vitendawili</td></tr>
<tr><td colspan="3">Uhusiano na Masuala Mtambuko<br>• Umoja wa kijamii – kushiriki katika vikundi<br>• Stadi za maisha – kutokana na maudhui katika vitendawili</td><td colspan="2">Uhusiano na Maadili<br>• Heshima – mwanafunzi anachangamkia maoni ya wenzake<br>• Umoja – wanafunzi wanapofanya kazi katika vikundi</td></tr>
<tr><td colspan="3">Uhusiano na Masomo Mengine<br>• English na Indigenous Languages- masomo haya hushughulikia vitendawili</td><td colspan="2">Mapendekezo ya shughuli za huduma za kijamii zinazochangia ujifunzaji<br>• Mwanafunzi anatarajiwa kukabiliana na masuala mbalimbali yanayohitaj uwazaji kina katika jamii.</td></tr>
</table>

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kutambua na kutamka kwa usahihi maneno yenye sauti zinazokaribiana katika vitendawili. | Mwanafunzi anatambua na kutamka kwa usahihi na wepesi maneno yenye sauti zinazokaribiana katika vitendawili. | Mwanafunzi anatambua na kutamka kwa usahihi maneno yenye sauti zinazokaribiana katika vitendawili. | Mwanafunzi anatambua na kutamka kwa usahihi baadhi ya maneno yenye sauti zinazokaribiana katika vitendawili. | Mwanafunzi anatambua baadhi ya maneno yenye sauti zinazokaribiana katika vitendawili na kutamka baadhi ya maneno hayo kwa usahihi. |
| Kutega na kutegua vitendawili kwa urahisi. | Mwanafunzi anatega na kutegua vitendawili kwa urahisi na wepesi. | Mwanafunzi anatega na kutegua vitendawili kwa urahisi. | Mwanafunzi atega na kutegua baadhi ya vitendawili kwa urahisi. | Mwanafunzi anatega baadhi ya vitendawili na kutegua baadhi yavyo. |

| MADA | MADA NDOGO | MATOKEO MAALUM YANAYOTARAJIWA | MAPENDEKEZO YA SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI | SWALI DADISI |
|---|---|---|---|---|
| **3.2 Kusoma** | **3.2.1 Kusoma kwa ufahamu:** Kifungu cha hadithi<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua msamiati wa mapambo uliotumiwa katika kifungu<br>b) kuelezea maana za msamiati mbalimbali wa mapambo<br>c) kusoma kifungu cha hadithi ili kupata ujumbe<br>d) kuonyesha uelewa wa hadithi kwa kutoa muhtasari na kujibu maswali<br>e) kuonea fahari kusoma hadithi kuhusu mapambo na kujibu maswali. | Mwanafunzi:<br>• atambue msamiati wa mapambo (*k.v vipuli*, *pete, bangili na ushanga*) kwa kutazama picha na vifaa halisi.<br>• atumie tarakilishi kutafuta msamiati wa mapambo na maana yake mtandaoni<br>• aeleze mapambo na sehemu yanapovaliwa.<br>• atunge sentensi akitumia msamiati husika, akiwa peke yake kisha kwenye wawiliwawili au kikundi.<br>• asome hadithi akishirikiana na wenzake kwa zamu ili kuelewa ujumbe kwa zamu<br>• atoe muhtasari wa hadithi aliyoisoma<br>• ajibu maswali kutokana na hadithi. | 1. Kwa nini ni muhimu kusoma kuhusu mapambo? |

**Umilisi wa Kimsingi unaokuzwa**
- Mawasiliano na ushirikiano- anaposoma mchezo mfupi kwa sauti na kupishana nafasi na wenzake.
- Kufikiri kwa kina – anapojibu maswali kutokana na mchezo mfupi aliousoma.

| | |
|---|---|
| **Uhusiano na Masuala Mtambuko**<br>• Elimu kwa maendeleo endelevu – anapotumia msamiati wa mapambo aliyojifunza.<br>• Kujiamini – anapofanya shughuli za darasani na kuzikamilisha | **Uhusiano na Maadili**<br>• Heshima – anaposikiliza wengine wakisoma mchezo mfupi.<br>• Upendo – anapowaelekeza wengine kujibu maswali. |
| **Uhusiano na masomo mengine**<br>• English and Indegineous Languages - masomo haya yana mada kuhusu vitendawili. | **Shughuli za kijamii zinazochangia ujifunzaji**<br>• Mwanafunzi awahamasishe wenzake shuleni na katika jamii kuhusu umuhimu wa kukuza utamaduni wa kusoma |

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kueleza na kutumia msamiati lengwa kwa ufasaha | Mwanafunzi anaeleza msamiati lengwa na kuutumia kwa ufasaha na wepesi | Mwanafunzi anaeleza msamiati lengwa na kuutumia kwa ufasaha | Mwanafunzi anaeleza baadhi ya msamiati lengwa na kuutumia kwa ufasaha | Mwanafunzi anaeleza baadhi ya msamiati lengwa na kutumia baadhi ya msamiati huo. |
| Kusoma kwa kuzingatia ujumbe na ufasaha. | Mwanafunzi anasoma kwa ufasaha na wepesi kwa kuzingatia ujumbe. | Mwanafunzi anasoma kwa ufasaha na kwa kuzingatia ujumbe. | Mwanafunzi anasoma kwa ufasaha. | Mwanafunzi anasoma sehemu ya kifungu. |
| Kujibu maswali ya ufahamu na kutoa muhtasari kwa usahihi. | Mwanafunzi anajibu maswali ya ufahamu na kutoa muhtasari kwa usahihi na urahisi. | Mwanafunzi anajibu maswali ya ufahamu na kutoa muhtasari kwa usahihi. | Mwanafunzi anajibu baadhi ya maswali ya ufahamu kwa usahihi. | Mwanafunzi anajaribu kujibu baadhi ya maswali ya ufahamu |

| MADA | MADA NDOGO | MATOKEO MAALUM YANAYOTARAJIWA | MAPENDEKEZO YA SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI | MASWALI DADISI |
|---|---|---|---|---|
| **3.3 Kuandika** | **3.3.1 Kuandika kwa Tarakilishi: Uchapaji**<br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua sehemu mbalimbali za tarakilishi zinazotumika kupigia chapa<br>b) kutumia tarakilishi ili kujenga maarifa ya kidijitali<br>c) kujenga mazoea ya kutumia tarakilishi kuandika na kuhifadhi maandishi. | Mwanafunzi :<br>• atambue sehemu mbalimbali za tarakilishi za kupigia chapa. (*k.v. bodidota, kipanya, kiwambo/mulishi n.k.*)<br>• atumie tarakilishi kuandika maneno au sentensi zinazolenga msamiati wa mapambo k.v. *herini, vipuli, pete, kipini, bangili, shanga, chapuo, taji, kugesi* na *hina*<br>• atumie tarakilishi kuandika kifungu kinahusisha mapambo mbalimbali<br>• ahifadhi kazi yake kwenye faili ya tarakilishi mara kwa mara<br>• ahariri kazi yake kwenye tarakilishi akishirikiana na wenzake katika kikundi<br>• atume kazi yake kwa mwalimu ili kuitathmini<br>• aendee kufanya mazoezi ya kuandika kwa kutumia tarakilishi akisaidiwa na mzazi/mlezi wake | 1. Je, ni sehemu zipi za tarakilishi unazozijua ?<br>2. Tarakilishi hutuwezesha kufanya kazi gani?<br>3. Ni hatua gani zinazohusika tunapotumia tarakilishi |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa** :

- Mawasiliano na ushirikiano - mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kazi za vikundi
- Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anapotumia tarakilishi kuandika na kuhifadhi kazi yake.
- Hamu ya ujifunzaji - mwanafunzi anapotagusana na vyombo vya kidijitali kama vile kutumia kipakatilishi, rununu n.k.

| **Uhusiano na masuala mtambuko** | **Uhusiano na maadili** |
|---|---|
| • Elimu ya maendeleo endelevu - kwa kuwa mwanafunzi anatumia ujuzi wa kiteknolojia ya kisasa kufanikisha uandishi. | • Umoja - kupitia kwa kazi za vikundi<br>• Uwajibikaji - mwanafunzi anaweza kuhifadhi vyombo vya kidijitali. |
| **Uhusiano wa masomo mengine** | **Mapendekezo ya shughuli za huduma za jamii zinazochangia ujifunzaji :** |
| • English na Science and Technology – masomo yana mada kuhusu masuala ya kidijitali. | • Kutumia tarakilishi na wenzake shuleni na nyumbani katika kufanyia mazoezi ya kuandika. |

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kutambua sehemu mbalimbali za tarakilishi za kupiga chapa na kuzitumia kuandika na kuhifadhi kazi kwa usahihi | Mwanafunzi anatambua sehemu mbalimbali za tarakilishi za kupiga chapa na kuzitumia kuandika na kuhifadhi kazi kwa usahihi na urahisi. | Mwanafunzi anatambua sehemu mbalimbali za tarakilishi za kupiga chapa na kuzitumia kuandika na kuhifadhi kazi kwa usahihi. | Mwanafunzi anatambua baadhi ya sehemu za tarakilishi za kupiga chapa na kuzitumia kuandika na kuhifadhi kazi. | Mwanafunzi anatambua baadhi ya sehemu za tarakilishi za kupigia chapa. |

| MADA | MADA NDOGO | MATOKEO MAALUM YANAYOTARAJIWA | MAPENDEKEZO YA SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI | MASWALI DADISI |
|---|---|---|---|---|
| **3.4 Sarufi** | **3.4.1 Aina za Nomino:**<br>Nomino za Makundi<br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua nomino za makundi katika sentensi ili kuzibainisha<br>b) kuelezea nomino za makundi kwa kutoa mifano mwafaka<br>c) kutumia nomino za makundi kwa usahihi katika sentensi<br>d) kuonea fahari matumizi ya nomino za makundi katika miktadha mbalimbali. | Mwanafunzi:<br>• atambue nomino za makundi *(k. v mlolongo wa magari, tita la kuni, mkungu wa ndizi, safu ya siafu, korija la maua, bunda la noti)* katika chati, kadi maneno, ubao, vifaa vya kidijitali n.k<br>• ajadili katika kikundi au wawiliwawili maana ya nomino za makundi huko akitoa mifano.<br>• atumie nomino za makundi katika sentensi na kuziandika daftarini mwake.<br>• atumie nomino za makundi kutunga sentensi mtandaoni akiwa na wenzake. | 1. Je, unajua maneno gani yanayotaja makundi ya watu na vitu?<br>2. Je, nomino za makundi hutumiwa vipi? |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anashiriki katika majadiliano ya nomino za makundi.
- Hamu ya kuendelea kujifunza-mwanafunzi anapojibu swali dadisi
- Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kutunga sentensi mtandaoni
- Kujiamini – mwanafunzi anapoweza kutumia nomino za makundi

**Uhusiano na Masuala Mtambuko**

- Uraia – mwanafunzi anaposhiriki katika vikundi vinavyojumuisha wanafunzi kutoka maeneo mbalimbali
- Stadi za maisha – mwanafunzi anapotangamana na wenzake katika shughuli za vikundi na kujifunza ukakamavu na kujiamini

**Uhusiano na Maadili**

- Heshima – wanafunzi wanapofanya kazi kwa zamu.
- Umoja – wanafunzi wanapofanya kazi katika vikundi
- Uwajibikaji – wanafunzi wanapokamilisha kazi yao kwa wakati ufaao

**Uhusiano na Masomo Mengine**

- English na Indigenous Languages – masomo haya yanashughulikia dhana ya nomino

**Mapendekezo ya shughuli za huduma za kujamii zinazochangia ujifunzaji:**

- Mwanafunzi atumie lugha kwa ustadi katika shughuli mbalimbali za kijamii

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kutambua nomino za makundi na kuzitumia kutunga sentensi sahihi | Mwanafunzi anatambua nomino za makundi na kuzitumia kwa urahisi kutunga sentensi sahihi | Mwanafunzi anatambua nomino za makundi na kuzitumia kutunga sentensi sahihi | Mwanafunzi anatambua baadhi ya nomino za makundi na kuzitumia kutunga sentensi sahihi | Mwanafunzi anatambua baadhi ya nomino za makundi na kutumia baadhi ya nomino alizotambua kutunga sentensi sahihi |

| MADA | MADA NDOGO | MATOKEO MAALUM YANAYOTARAJIWA | MAPENDEKEZO YA SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI | SWALI DADISI |
|---|---|---|---|---|
| **3.4 Sarufi** | **3.4.2 Aina za Nomino:** Nomino Ambata (Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua nomino ambata katika matini ili kuzitofautisha na aina nyingine za nomino<br>b) kutumia nomino ambata kwa usahihi katika sentensi ili kuimarisha mawasiliano<br>c) kuonea fahari matumizi ya nomino ambata katika mawasiliano. | Mwanafunzi:<br>• atambue nomino ambata (*k.v askarikanzu, mbwamwitu, mwanasiasa na mwananchi*) kwa kutumia kadi maneno, kapu maneno, chati au vifaa vya kidijitali akiwa peke yake, wawiliwawili au katika kikundi<br>• ajadili katika kikundi au wawiliwawili maana ya nomino ambata huko akitoa mifano.<br>• atumie nomino ambata katika sentensi na kuziandika katika daftari lake.<br>• atumie nomino ambata kutunga sentensi mtandaoni akishirikiana na wenzake.<br>• Asakure mtandaoni ili kupata mifano zaidi ya nomino ambata na kuziandika katika daftari lake | 1. Je, unajua maneno yapi yanayounganishwa kuunda neno moja? |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anashiriki katika majadiliano ya nomino ambata.
- Hamu ya kuendelea kujifunza – mwanafunzi anaposakura mtandaoni ili kupata mifano ya nomino ambata
- Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kutunga sentensi
- Kujiamini – mwanafunzi anapoweza kutumia nomino ambata kwa usahihi

| Uhusiano na Masuala Mtambuko | Uhusiano na Maadili |
|---|---|
| • Uraia – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za vikundi<br>• Stadi za maisha – mwanafunzi anapotangamana na wenzake katika shughuli za vikundi na kujifunza ukakamavu na kujiamini | • Heshima – wanafunzi wanapofanya kazi kwa zamu.<br>• Umoja – wanafunzi wanapofanya kazi pamoja katika vikundi<br>• Uwajibikaji- mwanafunzi anapokamilisha kazi yake |

| Uhusiano na Masomo Mengine | Mapendekezo ya shughuli za huduma za kujamii zinazochangia ujifunzaji |
|---|---|
| • English na Indeginous Languages – Masomo haya yanajumuisha mada ya nomino ambata | • Mwanafunzi awahamasishe wenzake shuleni na nyumbani kuhusu mawasiliano yenye kuzingatia kanuni za kisarufi. |

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kutambua nomino ambata na kuzitumia kutunga sentensi sahihi. | Mwanafunzi anatambua nomino ambata na kuzitumia kwa urahisi kutunga sentensi sahihi | Mwanafunzi anatambua nomino ambata na kuzitumia kutunga sentensi sahihi | Mwanafunzi anatambua baadhi ya nomino ambata na kuzitumia kutunga sentensi sahihi | Mwanafunzi anatambua baadhi ya nomino ambata na kutumia baadhi ya nomino alizotambua kutunga sentensi sahihi |

| MADA | MADA NDOGO | MATOKEO MAALUM YANAYOTARAJIWA | MAPENDEKEZO YA SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI | SWALI DADISI |
|---|---|---|---|---|
| **3.4 Sarufi** | **3.4.3 Aina za Nomino:** Nomino za dhahania (Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua nomino za dhahania katika matini mbalimbali<br>b) kuelezea nomino za dhahania kwa kutoa mifano mwafaka<br>c) kutumia nomino za dhahania kwa usahihi katika sentensi<br>d) kuonea fahari matumizi ya nomino za dhahania katika mawasiliano. | Mwanafunzi:<br>• atambue nomino za dhahania (*k.v upendo, uhodari, ukweli*) kwa kutumia kadi maneno, mti maneno, chati au vifaa vya kidijitali<br>• ajadili katika kikundi au wawiliwawili maana ya nomino za dhahania huko akitoa mifano.<br>• atumie nomino za dhahania katika sentensi na kuziandika sentensi hizo daftarini mwake<br>• atumie nomino za dhahania kutunga sentensi mtandaoni akishirikiana na wenzake. | 1. Je, unajua maneno yapi yanayotaja vitu ambavyo haviwezi kushikwa au kuonekana kwa macho? |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**
- Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anashiriki katika majadiliano ya nomino za dhahania.
- Hamu ya kuendelea kujifunza - mwanafunzi anapojibu swali dadisi
- Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kutunga sentensi
- Kujiamini – mwanafunzi anapoweza kutumia nomino za dhahania

| **Uhusiano na Masuala Mtambuko** | **Uhusiano na Maadili** |
|---|---|
| • Uraia – anaposhiriki katika vikundi vinavyojumuisha wanafunzi kutoka maeneo mbalimbali<br>• Stadi za maisha – mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za vikundi. Katika vikundi hivyo atajifunza ukakamavu, stahamala na kujiamini. | • Heshima – wanafunzi wanapofanya kazi kwa zamu.<br>• Umoja – wanafunzi wanapofanya kazi katika vikundi<br>• Uwajibikaji- mwanafunzi anapokamilisha kazi yake |
| **Uhusiano na Masomo Mengine** | **Mapendekezo ya shughuli za huduma za kijamii zinazochangia ujifunzaji** |
| • English na Indeginous Languages – masomo haya hufunza dhana ya nomino | • Mwanafunzi awahamasishe wenzake shuleni na nyumbani kuhusu mawasiliano yenye kuzingatia kanuni za kisarufi. |

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kutambua nomino za dhahania na kuzitumia kutunga sentensi sahihi. | Mwanafunzi anatambua nomino za dhahania na kuzitumia kwa urahisi kutunga sentensi sahihi | Mwanafunzi anatambua nomino za dhahania na kuzitumia kutunga sentensi sahihi | Mwanafunzi anatambua baadhi ya nomino za dhahania na kuzitumia kutunga sentensi sahihi | Mwanafunzi anatambua baadhi ya nomino za dhahania na kutumia baadhi ya nomino alizotambua kutunga sentensi sahihi |

| MADA | MADA NDOGO | MATOKEO MAALUM YANAYOTARAJIWA | MAPENDEKEZO YA SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI | SWALI DADISI |
|---|---|---|---|---|
| **3.4 Sarufi** | **3.4.4 Uakifishi**:<br>-Herufi kubwa<br>-koma (,)<br>-kikomo (.)<br>-kiulizi (?)<br><br>(Vipindi 4) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua herufi kubwa, alama ya koma, kikomo na kiulizi katika maandishi<br>b) kutumia herufi kubwa, koma, kikomo na kiulizi ifaavyo katika maaandishi<br>c) kufurahia matumizi ya herufi kubwa, koma, kikomo na kiulizi katika maaandishi | Mwanafunzi:<br>• atambue herufi kubwa, koma, kikomo na kiulizi katika maandishi<br>• ashiriki katika vikundi kuakifisha sentensi akitumia herufi kubwa, koma, kikomo na kiulizi (baadhi ya sentensi ziangazie suala lengwa)<br>• aandike sentensi akitumia herufi kubwa, koma, kikomo na kiulizi ifaavyo<br>• aandike sentensi zenye herufi kubwa, koma, kikomo na kiulizi akitumia kifaa cha kidijitali. | 1. Kwa nini alama za kuakifisha hutumiwa katika maandishi? |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano - wanafunzi wanaposhiriki mijadala kuhusu alama za uakifishi
- Ubunifu - mwanafunzi anapotunga sentensi sahihi wakitumia viakifishi
- Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anapoandika sentensi zenye herufi kubwa, koma, kikomo na kiulizi akitumia kifaa cha kidijitali.

| Uhusiano na Masuala Mtambuko | Uhusiano na Maadili |
|---|---|
| • Uraia – kutunga sentensi zinazolenga mapambo yanayotumiwa na watu tofautitofauti.<br>• Masuala mtambuko anuwai kutokana na sentensi zinazotoa maelezo kuhusu masuala hayo k.v. utunzaji wa mazingira, upunguzaji wa mikasa, usalama | • Umoja – wanafunzi wanapofanya kazi katika makundi<br>• Maadili mbalimbali yaliyolengwa katika sentensi k.v. upendo, uaminifu, uzalendo, amani na umoja. |

| Uhusiano na Masomo Mengine | Mapendekezo ya shughuli za huduma za Kijamii zinazochangia ujifunzaji: |
|---|---|
| • English Activities na Indigenous Language - Masomo haya hushughulikia uakifishi | • Mwanafunzi awe kielelezo cha kutumia lugha kwa ufasaha shuleni na nyumbani. |

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kutambua na kutumia herufi kubwa, koma, kikomo na kiulizi katika maandishi kwa usahihi. | Mwanafunzi anatambua na kutumia herufi kubwa, koma, kikomo na kiulizi katika maandishi kwa usahihi na urahisi. | Mwanafunzi anatambua na kutumia herufi kubwa, koma, kikomo na kiulizi katika maandishi kwa usahihi. | Mwanafunzi anatambua na kutumia baadhi ya alama lengwa za uakifishi katika maandishi kwa usahihi. | Mwanafunzi anatambua na kutumia baadhi ya alama lengwa za uakifishi katika maandishi. |

## 4.0 SAA NA MAJIRA

| MADA | MADA NDOGO | MATOKEO MAALUM YANAYOTARAJIWA | MAPENDEKEZO YA SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI | SWALI DADISI |
|---|---|---|---|---|
| **4.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **4.1.1 Heshima, adabu na vyeo:**<br>Maneno ya Heshima<br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua maneno ya heshima yanayohusiana na udugu yanayotumiwa katika mawasiliano<br>b) kutumia maneno ya udugu kwa usahihi katika mazungumzo yake ya kila siku<br>c) kuthamini kutumia maneno ya udugu katika mawasiliano ya kila siku. | Mwanafunzi:<br>• atambue maneno ya udugu (*k.v. bwana, bibi, ndugu, binti, bin, mama, mama mkubwa/mdogo, mjomba)* kwenye ubao, mti maneno, tarakilishi au kapu maneno.<br>• aeleze maana ya maneno lengwa kama yanavyotumiwa katika mahusiano ya kila siku kati ya watu.<br>• atunge sentensi kwa kutumia maneno lengwa kwa usahihi.<br>• atazame maigizo ya watu wakitumia maneno ya udugu kwenye tarakilishi na video.<br>• ajadili matumizi ya maneno ya udugu akishirikiana na wenzake darasani.<br>• aigize mazungumzo mafupi akiwa na wenzake huku akitumia msamiati wa udugu. | 1. Unatumia neno lipi la heshima kumrejelea mwalimu wako wa kike au wa kiume? |

**Umilisi wa Kimsingi unaokuzwa**
- Ujuzi wa kidijitali – anapotumia tarakilishi, video na projekta kutazama maigizo mafupi
- Mawasiliano na ushirikiano – anaposhiriki katika maigizo na mijadala

| **Uhusiano na masuala mtambuko** | **Uhusiano na maadili** |
|---|---|
| • Utangamano – anaposhiriki katika maigizo mafupi<br>• Stadi za maisha – anapotumia maneno ya udugu katika mawasiliano | • Heshima – anapotumia maneno ya udugu.<br>• Upendo – anapotumia maneno ya udugu kwa wenzake na kwa wakubwa wake. |
| **Uhusiano na masomo mengine** | **Shughuli za kijamii zinazochangia ujifunzaji** |
| • English, Indigenous Languages na Religious Studies – lugha ya heshima hufunzwa katika masomo haya | • Mwanafunzi ahimize wenzake kutumia maneno ya udugu shuleni na nyumbani. |

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kutambua maneno ya udugu na kuyatumia katika sentensi kwa usahihi. | Mwanafunzi anatambua maneno ya udugu na kuyatumia katika sentensi kwa usahihi na wepesi. | Mwanafunzi anatambua maneno ya udugu na kuyatumia katika sentensi kwa usahihi. | Mwanafunzi anatambua baadhi ya maneno ya udugu na kuyatumia katika sentensi kwa usahihi. | Mwanafunzi anatambua baadhi ya maneno ya udugu na kutumia baadhi ya maneno hayo katika sentensi. |

| MADA | MADA NDOGO | MATOKEO MAALUM YANAYOTARAJIWA | MAPENDEKEZO YA SHUNGULI ZA UJIFUNZAJI | SWALI DADISI |
|---|---|---|---|---|
| **4.2 Kusoma** | **4.2.1 Kusoma kwa Mapana:** Matini ya kidijitali (Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua na kuzingatia hatua za kiusalama katika matumizi ya vifaa vya kidijitali<br>b) kutambua msamiati wa suala lengwa katika matini ya kidijitali<br>c) kusakura matini kwenye tovuti salama ili kupata vifungu vya kusoma vyenye suala lengwa<br>d) kuchangamkia matumizi ya vifaa vya kidijitali katika kutafuta na kusoma ujumbe ili kuimarisha maarifa yake. | Mwanafunzi:<br>• azingatie hatua za kiusalama katika kutumia vifaa vya kidijitali k.v. kufungua mitandao ifaayo.<br>• atambue mitandao salama yenye matini inayohusu suala lengwa (saa na majira) na inayoafiki kiwango chake<br>• atambue umuhimu wa kutoa habari kwa mwalimu, mzazi au mlezi wake endapo atapata ujumbe kutoka kwa watu asiowajua mtandaoni na kutowasiliana nao<br>• asome matini kwa kutumia vifaa vya kidijitali yanayojumuisha msamiati wa saa *(k.v. kasoro dakika…, saa…kamili, saa…na dakika…)* na majira (nyakati za siku) (*k.v. alfajiri*, *asubuhi*, *adhuhuri*, *alasiri*, *thenashara*, *machweo na macheo*)<br>• asome vifungu vyenye suala lengwa ambavyo alisakura<br>• atoe habari kuhusu matini aliyosoma kwa muhtasari na kujibu maswali katika maandishi au mazungumzo na wenzake | 1. Ni njia zipi unazoweza kupata matini za kusoma katika vifaa vya kiteknolojia ? |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Ujuzi wa kidijitali – unakuzwa wakati vifaa vya kiteknolojia vinatumiwa katika kusakura na kusoma matini.
- Hamu ya kujifunza – mwanafunzi atapata hamu ya kutafuta matini za kusoma kwenye tarakilishi na mitandaoni

| Uhusiano na Masuala Mtambuko | Uhusiano na Maadili |
|---|---|
| • Stadi za maisha – mwanfunzi anazingatia hatua za kiusalama mtandaoni<br>• Usalama wa mtandaoni – mwanafunzi anapotambua hatari zinazoambatana na mtandao | • Uwajibikaji – katika utunzaji wa vifaa vya kidijitali na kuzingatia mitandao salama<br>• Uaminifu na ukweli – mwanafunzi anapohakikisha anasakura matini kwenye tovuti salama |

| **Uhusiano na Masomo Mengine** | **Mapendekezo ya shughuli za huduma za kijamii zinazochangia ujifunzaji:** |
|---|---|
| • Masomo yote kwa vile yanatakiwa kuzingatia ujuzi wa kidijitali | • Kuwahamasisha wenzake nyumbani na shuleni kuhusu kusoma matini ya kidijitali na kuzingatia usalama wa mtandaoni. |

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| **Viwango** / **Vigezo** | **Kuzidisha Matarajio** | **Kufikia Matarajio** | **Kukaribia Matarajio** | **Mbali na Matarajio** |
|---|---|---|---|---|
| Kutambua na kuzingatia hatua za kiusalama mtandaoni. | Mwanafunzi anatambua na kuzingatia hatua za kiusalama mtandaoni kwa urahisi | Mwanafunzi anatambua na kuzingatia hatua za kiusalama mtandaoni | Mwanafunzi anatambua na kuzingatia baadhi ya hatua za kiusalama mtandaoni | Mwanafunzi anatambua baadhi ya hatua za kuisalama na anajaribu kuzingatia baadhi ya hatua anazotambua mtandaoni |
| Kutambua tovuti salama zenye habari lengwa | Mwanafunzi anatambua tovuti salama zenye habari lengwa kwa urahisi | Mwanafunzi anatambua tovuti salama zenye habari lengwa | Mwanafunzi anatambua baadhi ya tovuti salama zenye habari lengwa | Mwanafunzi anajaribu kutambua tovuti salama |
| Kutafuta matini kwenye kifaa cha kidijitali au mtandaoni na kuzisoma | Mwanafunzi anatafuta kwa urahisi matini kwenye kifaa cha kidijitali au mtandaoni na kuzisoma | Mwanafunzi anatafuta matini kwenye kifaa cha kidijitali au mtandaoni na kuzisoma | Mwanafunzi anatafuta baadhi ya matini kwenye kifaa cha kidijitali au mtandaoni na kuzisoma | Mwanafunzi anajaribu kutafuta matini kwenye kifaa cha kidijitali au mtandaoni |

| MADA | MADA NDOGO | MATOKEO MAALUM YANAYOTARAJIWA | MAPENDEKEZO YA SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI | MASWALI DADISI |
|---|---|---|---|---|
| **4.3 Kuandika** | **4.3.1: Aina za Insha**: Baruapepe<br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua baruapepe kwa kuzingatia muundo wake<br>b) kuandika baruapepe kwa kuzingatia ujumbe, muundo na mtindo<br>c) kuchangamkia uandishi wa baruapepe katika mawasiliano. | Mwanafunzi:<br>• atambue muundo wa baruapepe kwa kurejelea kielelezo chake kilichochapishwa au kwenye tarakilishi<br>• ajadili sehemu mbalimbali za baruapepe kama vile anwanipepe ya mtumaji (k.m. tina18@gmail.com), anwanipepe ya mpokeaji, mada ya baruapepe, mtajo, mwili, hitimisho na jina la mwandishi/mtumaji.<br>• aandike baruapepe kwa rafiki, ndugu, au mzazi akishirikiana na wenzake darasani, kwa kutumia tarakilishi akizingatia muundo wa uandishi wa baruapepe, utaratibu ufaao, kutunga na kupanga sentensi kuunda aya katika uandishi barua<br>• ashirikiane na wenzake kujadili mada ya baruapepe na vipengele vyake/yale yanayofaa kujumuishwa<br>• aandike baruapepe kwa rafiki kwa kuzingatia ubora wa sentensi (sahihi kisarufi, zilizokamilika kimaana, zenye kufuatana kwa kujenga wazo na zenye kuzingatia uakifishi mzuri) kuunda aya<br>• ashirikishe msamiati wa mada lengwa katika baruapepe yake<br>• aandike baruapepe na kuituma kwa wenzake na mwalimu ili waisome na kuitathmini | 1. Unazingatia mambo gani unapoandika baruapepe?<br>2. Ni mambo gani unayoweza kumweleza rafiki yako katika baruapepe? |
| **Umilisi wa Kimsingi unaokuzwa**<br>• Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za kikundi na kujadiliana na wenzake kuhusu baruapepe<br>• Ubunifu – mwanafunzi anapoandika na kutuma baruapepe.<br>• Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anapotumia tarakilishi kuandika na kutuma baruapepe. | | | | |
| **Uhusiano na Masuala Mtambuko** | | | **Uhusiano na Maadili** | |

| | |
|---|---|
| • Stadi za maisha - anapotumia baruapepe kuwasiliana.<br>• Elimu kwa maendeleo endelevu – anapotumia teknolojia kuwasiliana | • Upendo – anapotuma baruapepe kwa kirafiki, mzazi au mlezi wake kuwajulia hali.<br>• Heshima – anapozingatia maoni ya wengine wakati wa mijadala.<br>• Uwajibikaji – anapotunza tarakilishi anayoitumia katika uandishi wa baruapepe. |
| **Uhusiano na masomo mengine**<br>• Masomo yote yanayoshughulikia ujuzi wa kidijitali | **Shughuli za kijamii zinazochangia ujifunzaji**<br>• Awahamasishe wenzake shuleni na nyumbani kuhusu matumizi ya vifaa vya kijitali katika mawasiliano |

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kutambua baruapepe kwa kuzingatia muundo wake | Mwanafunzi anatambua kwa wepesi baruapepe kwa kuzingatia muundo wake | Mwanafunzi anatambua baruapepe kwa kuzingatia muundo wake | Mwanafunzi anatambua baadhi ya baruapepe kwa kuzingatia muundo wake | Mwanafunzi anatazika kutambua baruapepe kwa kuzingatia muundo wake |
| Kuandika baruapepe kwa kuzingatia ujumbe, muundo na mtindo na kuituma. | Mwanafunzi anaandika baruapepe kwa urahisi kwa kuzingatia ujumbe, muundo na mtindo na kuituma. | Mwanafunzi anaandika baruapepe kwa kuzingatia ujumbe, muundo na mtindo na kuituma. | Mwanafunzi anaandika baruapepe kwa kuzingatia ujumbe na baadhi ya vipengee vya kimuundo na kimtindo na kuituma. | Mwanafunzi anajaribu kuandika baruapepe bila kuzingatia ujumbe, muundo na mtindo. |

| MADA | MADA NDOGO | MATOKEO MAALUM YANAYOTARAJIWA | MAPENDEKEZO YA SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI | SWALI DADISI |
|---|---|---|---|---|
| **4.4 Sarufi** | **4.4.1 Umoja na wingi wa nomino:** Ngeli I-ZI (Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua nomino katika ngeli ya I-ZI ili kuzitofautisha na nomino katika ngeli nyingine<br>b) kuandika nomino za ngeli ya I-ZI katika umoja na wingi<br>c) kuandika umoja na wingi wa mafungu ya maneno katika ngeli ya ngeli ya I-ZI<br>d) kuchangamkia kutumia nomino za ngeli ya I-ZI katika mawasiliano. | Mwanafunzi:<br>• atambue nomino katika ngeli ya I-ZI kwenye kadi, mti maneno, tarakilishi au kapu la maneno *(k.v. nguo- nguo, ndizi-ndizi, ndoo-ndoo na nyumba-nyumba*)<br>• aandike nomino katika ngeli ya I-ZI katika umoja na wingi akiwa peke yake, wawiliwawili au katika vikundi<br>• asikize usomaji wa nomino za ngeli ya I-ZI kutoka kwenye tepurekoda au kinasasauti<br>• aandike mafungu ya maneno yenye nomino za ngeli ya I-ZI katika umoja na wingi<br>• ajaze mapengo kwa kutumia viambishi vya ngeli ya I-ZI kwa maandishi ya mkono au kwa tarakilishi. | 1. Je, unajua nomino zipi ambazo hazibadiliki katika umoja na wingi? |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano – unakuzwa mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika vikundi
- Ubunifu - unakuzwa mwanafunzi anapotunga mafungu ya maneno
- Ujuzi wa kidijitali - unakuzwa tarakilishi inapotumika kutambua nomino na mafungu ya maneno kwenye kinasasauti

| **Uhusiano na Masuala Mtambuko** | **Uhusiano na Maadili** |
|---|---|
| • Utangamano – kufanya kazi kwa vikundi<br>• Stadi za Maisha - kujifanyia kazi darasani | • Uwajibikaji - kutunza vipakatalishi anavyotumia<br>• Uzalendo - kufanya kazi na wengine kwenye vikundi |
| **Uhusiano na Masomo Mengine** | **Mapendekezo ya shughuli za huduma za Kijamii zinazochangia ujifunzaji:** |
| • English na Indigenous Languages – masomo haya yanajumuisha ngeli za nomino | • Mwanafunzi atumie lugha kwa ufasaha kuimarisha mawasiliano katika jamii |

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| **Viwango** / **Vigezo** | **Kuzidisha Matarajio** | **Kufikia Matarajio** | **Kukaribia Matarajio** | **Mbali na Matarajio** |
|---|---|---|---|---|
| Kutambua nomino katika ngeli ya I-ZI | Mwanafunzi anatambua nomino za ngeli ya I – ZI kwa urahisi | Mwanafunzi anatambua nomino za ngeli ya I – Z | Mwanafunzi anatambua baadhi ya nomino za ngeli ya I – ZI | Mwanafunzi anatatizika kutambua nomino za ngeli ya I – ZI |
| Kuandika nomino za ngeli ya I-ZI katika umoja na wingi | Mwanafunzi anaandika kwa urahisi nomino za ngeli ya I-ZI katika umoja na wingi | Mwanafunzi anaandika nomino za ngeli ya I-ZI katika umoja na wingi | Mwanafunzi anaandika baadhi ya nomino za ngeli ya I-ZI katika umoja na wingi | Mwanafunzi ana changamoto kuandika nomino za ngeli ya I-ZI katika umoja na wingi |
| Kuandika umoja na wingi wa mafungu ya maneno katika ngeli ya ngeli ya I-ZI | Mwanafunzi anaandika umoja na wingi wa mafungu ya maneno katika ngeli ya I-ZI kwa usahihi na wepesi | Mwanafunzi anaandika umoja na wingi wa mafungu ya maneno katika ngeli ya I-ZI kwa usahihi | Mwanafunzi anaandika umoja na wingi wa baadhi ya mafungu ya maneno katika ngeli ya I-ZI kwa usahihi | Mwanafunzi anaandika umoja na wingi wa baadhi ya mafungu ya maneno katika ngeli ya I-ZI |

| MADA | MADA NDOGO | MATOKEO MAALUM YANAYOTARAJIWA | MAPENDEKEZO YA SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI | SWALI DADISI |
|---|---|---|---|---|
| **4.4 Sarufi** | **4.4.2 Umoja na wingi wa sentensi:** katika ngeli ya I-ZI<br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua viambishi vipatanishi vya ngeli ya I-ZI kwenye sentensi<br>b) kuunda sentensi akitumia nomino za ngeli ya I-ZI katika umoja na wingi akizingatia upatanisho wa kisarufi<br>c) kuonea fahari matumizi ya ngeli ya I-ZI katika mawasiliano | Mwanafunzi:<br>• atambue viambishi vya ngeli ya I-ZI katika sentensi kwa kuvipigia mstari daftarini au kuvikoleza rangi katika tarakilishi<br>• atumie nomino za ngeli ya I-ZI katika sentensi akiwa peke yake, wawiliwawili au katika vikundi<br>• asikize usomaji wa sentensi zilizoundwa kutokana na nomino za ngeli ya I-ZI kutoka kwenye tepurekoda au kinasasauti<br>• aunde sentensi kwa kutumia nomino ya ngeli ya I-ZI akiwa peke yake au kwa kushirikiana na wenzake<br>• ajaze mapengo kwa kutumia viambishi vya ngeli ya I-ZI kwa maandishi ya mkono au tarakilishi. | 1. Je, unajua nomino zipi ambazo zinaanza kwa herufi **U** katika umoja? |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano – unakuzwa mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kazi ya vikundi
- Ubunifu – unakuzwa mwanafunzi anapotunga sentensi sahihi
- Kufikiri kwa kina - kunakuzwa mwanafunzi anapowaza kwa kina kuhusu sentensi sahihi katika ngeli ya I-ZI
- Ujuzi wa kidijitali – kutumia tarakilishi kutambua nomino na katika kusikiliza sentensi kwenye tepurekoda

| Uhusiano na Masuala Mtambuko | Uhusiano na Maadili |
|---|---|
| • Uraia – kupitia kushiriki katika kazi ya vikundi vinavyojumuisha wanafunzi kutoka maeneo mbalimbali<br>• Stadi za Maisha - anapotangamana na wenzake katika kazi ya vikundi | • Uwajibikaji – mwanafunzi anapotunza vifaa vya kidijitali anavyotumia kujaza mapengo<br>• Umoja na amani – mwanafunzi anapofanya kazi na wengine kwenye vikundi |
| **Uhusiano na Masomo Mengine** | **Mapendekezo ya shughuli za huduma za Kijamii zinazochangia ujifunzaji:** |
| • English na Indigenous Languages – masomo haya yanafunza ngeli | • Mwanafunzi atumie lugha kwa ufasaha kuimarisha mawasiliano katika jamii. |

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
| --- | --- | --- | --- | --- |
| Kutambua nomino za ngeli ya I-ZI, viambishi vyake na kutumia nomino za ngeli hii kutunga sentensi sahihi zenye maana. | Mwanafunzi anatambua nomino za ngeli ya I-ZI, viambishi vyake na kutumia nomino za ngeli hii kutunga sentensi sahihi zenye maana kwa urahisi. | Mwanafunzi anatambua nomino za ngeli ya I-ZI, viambishi vyake na kutumia nomino za ngeli hii kutunga sentensi sahihi zenye maana. | Mwanafunzi anatambua baadhi ya nomino za ngeli ya I-ZI, viambishi vyake na kutumia nomino za ngeli hii kutunga sentensi sahihi zenye maana. | Mwanafunzi anatambua baadhi ya nomino za ngeli ya I-ZI, viambishi vyake na kutumia baadhi ya nomino alizotambua kutunga sentensi sahihi zenye maana. |

<table>
<tr><th colspan="5">5.0 KUKABILIANA NA UMASKINI</th></tr>
<tr><th>MADA</th><th>MADA NDOGO</th><th>MATOKEO MAALUM YANAYOTARAJIWA</th><th>MAPENDEKEZO YA SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI</th><th>SWALI DADISI</th></tr>
<tr><td>5.1 Kusikiliza na Kuzungumza</td><td>5.1.1 Methali: Methali zinazohusu bidii (Vipindi 2)</td><td>Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua methali zinazohusu bidii ili kuzitofautisha na aina nyingine za methali<br>b) kueleza maana na matumizi ya methali mbalimbali zinazohusu bidii katika jamii<br>c) kutumia methali zinazohusu bidii katika mawasiliano<br>d) kuchangamkia matumizi ya methali katika kuhimiza bidii.</td><td>Mwanafunzi:<br>• atambue methali zinazohusu bidii (k.v. mchagua jembe si mkulima, mgagaa na upwa hali wali mkavu, atafutaye hupata, anayejitahidi hufaidi, ukiona vyaelea vimeundwa) katika chati, ubao, vyombo vya kidijitali<br>• ajadili maana na matumizi ya methali zinazohusu bidii na wenzake darasani<br>• atoe mifano ya methali zinazohusu bidii<br>• asikilize methali zinazohusu bidii zikitumiwa kupitia vyombo vya kidijitali.<br>• ashirikiane na wenzake katika kukamilisha methali zinazohusu bidii<br>• asakure mtandaoni kwa kusaidiwa na mzazi au mlezi wake ili kupata methali zaidi zinazohusu bidii na matumizi ya methali hizo.</td><td>1. Je, ni nini umuhimu wa methali katika jamii?</td></tr>
<tr><td colspan="5">Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa<br>• Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anaposhiriki katika kujadili methali kwenye vikundi<br>• Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo – unakuzwa mwanafunzi anapofikiria kuhusu matumizi ya methali<br>• Ubunifu – mwanafunzi anapotumia methali kujieleza<br>• Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kutambua methali na kupata methali zaidi.</td></tr>
<tr><td colspan="3">Uhusiano na Masuala Mtambuko<br>• Ushauri nasaha – methali zinahusu maadili<br>• Uraia – unakuzwa kupitia kushiriki katika vikundi<br>• Stadi za maisha – kutokana na mafunzo ya methali zinazohusu bidii</td><td colspan="2">Uhusiano na Maadili<br>• Heshima – mwanafunzi anachangamkia maoni ya wenzake katika kikundi<br>• Umoja – wanafunzi wanapofanya kazi katika vikundi</td></tr>
</table>

| Uhusiano na Masomo Mengine | Mapendekezo ya shughuli za huduma za kujamii zinazochangia ujifunzaji |
|---|---|
| • English na Indigenous Languages – masoma haya yanajumuisha mada ya methali | • Mwanafunzi anatarajiwa kuwa kielelezo bora kwa wanajamii katika matumizi ya lugha kwa ubunifu katika mawasiliano |

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kutambua methali zinazohusu bidii katika matini | Mwanafunzi anatambua methali zinazohusu bidii katika matini kwa wepesi | Mwanafunzi anatambua methali zinazohusu bidii katika matini | Mwanafunzi anatambua baadhi ya methali zinazohusu bidii katika matini | Mwanafunzi anatatizika kutambua methali zinazohusu bidii katika matini |
| Kueleza maana na matumizi ya methali zinazohusu bidii kwa ufasaha | Mwanafunzi anaeleza maana na matumizi ya methali zinazohusu bidii kwa ufasaha na urahisi | Mwanafunzi anaeleza maana na matumizi ya methali zinazohusu bidii kwa ufasaha | Mwanafunzi anaeleza maana na matumizi ya baadhi ya methali zinazohusu bidii kwa ufasaha | Mwanafunzi ana changamoto kueleza maana na matumizi ya methali zinazohusu bidii |
| Kutumia methali zinazohusu bidii katika mawasiliano | Mwanafunzi anatumia methali zinazohusu bidii katika mawasiliano kwa urahisi na ufasaha | Mwanafunzi anatumia methali zinazohusu bidii katika mawasiliano kwa urahisi | Mwanafunzi anatumia baadhi ya methali zinazohusu bidii katika mawasiliano kwa urahisi | Mwanafunzi anajaribu kutumia baadhi ya methali zinazohusu bidii katika mawasiliano |

| MADA | MADA NDOGO | MATOKEO MAALUM YANAYOTARAJIWA | MAPENDEKEZO YA SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI | SWALI DADISI |
|---|---|---|---|---|
| **5.2 Kusoma** | **5.2.1 Kusoma kwa ufahamu:** Lugha katika ushairi<br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua vina na mizani katika shairi ili kuvibainisha<br>b) kusoma shairi akizingatia vina, mizani na ujumbe ili kuimarisha ufahamu<br>c) achangamkie kusoma shairi akizingatia mapigo ya sauti. | Mwanafunzi:<br>• atambue vina na mizani katika shairi lililochapisha au la mtandaoni<br>• ajadili vina na mizani katika shairi akiwa na mwenzake au katika kikundi<br>• ashirikiane na mwenzake kusoma shairi akizingatia vina, mizani na ujumbe<br>• asikilize shairi likisomwa kwa mahadhi kwenye vifaa vya kidijitali au na mgeni mwalikwa na kujadili vina, mizani na ujumbe wake<br>• ashirikiane na wenzake kutafuta mashairi mtandaoni na kujadili vina, mizani na ujumbe uliomo | 1. Je, ni nini kinachotofautisha mashairi na maandishi mengine? |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anaposhiriki katika kujadili msamiati unaotumika katika shairi
- Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo – unakuzwa mwanafunzi anapojadili ujumbe katika shairi
- Ubunifu – mwanafunzi anapofafanua ujumbe wa shairi
- Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kutambua vina na mizani katika shairi

**Uhusiano na Masuala Mtambuko**

- Ushauri nasaha – ujumbe unaozingatiwa katika shairi
- Uraia – kutokana na kushiriki katika vikundi
- Stadi za maisha – mwanafunzi anapotumia lugha kwa ufundi

**Uhusiano na Maadili**

- Heshima – mwanafunzi anachangamkia maoni ya wenzake katika kikundi
- Umoja – wanafunzi wanapofanya kazi katika vikundi

**Uhusiano na Masomo Mengine**

- English na Indigenous languages– masomo haya yanashughulikia nyimbo na mashairi.

**Mapendekezo ya shughuli za huduma za kijamii zinazochangia ujifunzaji**

- Mwanafunzi anaweza kutumia ushairi kutumbuiza na kama njia moja ya kuwahamasisha wengine katika jamii kuhusu masuala mbalimbali.

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kutambua vina na mizani katika shairi | Mwanafunzi anatambua vina na mizani katika shairi kwa urahisi | Mwanafunzi anatambua vina na mizani katika shairi | Mwanafunzi anatambua baadhi ya vina na mizani katika shairi | Mwanafunzi ana changamoto kutambua vina na mizani katika shairi |
| Kusoma shairi kwa kuzingatia vina, mizani na ujumbe | Mwanafunzi anasoma shairi kwa ufasaha na wepesi akizingatia vina, mizani na ujumbe | Mwanafunzi anasoma shairi kwa ufasaha akizingatia vina, mizani na ujumbe | Mwanafunzi anasoma shairi akizingatia vina, mizani na ujumbe | Mwanafunzi anasoma shairi bila kuzingatia vina, mizani na ujumbe |

<table>
<tr><th>MADA</th><th>MADA NDOGO</th><th>MATOKEO MAALUMU YANAYOTARAJIWA</th><th>MAPENDEKEZO YA SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI</th><th>SWALI DADISI</th></tr>
<tr><td>5.3 Kuandika</td><td>5.3.1 Insha ya Maelezo<br>(Vipindi 2)</td><td>Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua insha za maelezo katika matini mbalimbali<br>b) kuandika insha ya maelezo kwa kufuata kanuni zifaazo<br>c) kuchangamkia utunzi mzuri wa insha ili kuimarisha uandishi.</td><td>Mwanafunzi:<br>• atambue vifungu vya maelezo vilivyoandikwa kwenye matini mbalimbali au tarakilishi<br>• ashiriki na wenzake kujadili mada ya insha na muundo wa insha ya maelezo<br>• ajadiliane na wenzake kuhusu mambo muhimu yanayojenga mpangilio mzuri wa mawazo katika insha<br>• aandike insha ya maelezo (k.v. Jinsi ninavyoweza kuchangia kukabiliana na umaskini nyumbani, Maskini alivyogeuka kuwa tajiri, Jinsi elimu ilivyosaidia kumaliza umaskini, jinsi matumizi bora ya pesa yanasaidia kumaliza umaskini, jinsi ulipaji ushuru unasaidia kukabiliana na umaskini) isiyopungua maneno 150 kwa kuzingatia anwani, mpangilio mzuri wa mawazo, hati safi, tahajia, kanuni za kisarufi, uakifishaji mwafaka na kwa lugha ya kiubunifu unaojumuisha methali na nahau alizojifunza awali<br>• aandike insha ya maelezo mtandaoni na kuisambaza kwa wenzake na mwalimu ili kuisoma na kuitathmini<br>• awasomee wenzake insha aliyoandika ili kuitolea maoni.</td><td>1. Unazingatia nini unapoandika insha ya maelezo?</td></tr>
<tr><td colspan="5">Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:<br>• Mawasiliano na ushirikiano – unakuzwa wanafunzi wanaposhiriki katika mijadala na kazi za vikundi<br>• Ujuzi wa kidijitali – unakuzwa wakati vifaa vya kiteknolojia vinapotumiwa kuandika insha mtandaoni na kurejelea kielelezo cha insha ya maelezo<br>• Ubunifu – unajengeka mwanafunzi anapoandika insha ya maelezo<br>• Hamu ya ujifunzaji – unakuzwa mwanafunzi anapoyatafakari maswali dadisi na anapoimarisha ujuzi wake wa kutumia tarakilishi</td></tr>
<tr><td colspan="3">Uhusiano na masuala mtambuko:<br>• Uraia – kutokana na kufanya kazi pamoja.<br>• Elimu ya pesa – anapoandika insha kuhusu jinsi ya kukabiliana na umaskini</td><td colspan="2">Uhusiano na Maadili:<br>• Heshima na adabu hasa katika shughuli za vikundi</td></tr>
<tr><td colspan="3">Uhusiano na masomo mengine:<br>• English na Indigeneous Language hushughulikia dhana ya uandishi</td><td colspan="2">Mapendekezo ya shughuli za huduma za kijamii zinazochangia ujifunzaji:<br>• Kuwahamasisha wenzake shuleni na nyumbani kuhusu umuhimu wa uandishi mzuri katika insha</td></tr>
</table>

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kutambua na kuandika insha ya maelezo inayojenga picha dhahiri na yenye kuzingatia kanuni za lugha na mpangilio mzuri wa mawazo. | Mwanafunzi anatambua na kuandika insha ya maelezo inayojenga picha dhahiri na yenye kuzingatia kanuni za lugha na mpangilio mzuri wa mawazo kwa urahisi. | Mwanafunzi anatambua na kuandika insha ya maelezo inayojenga picha dhahiri na yenye kuzingatia kanuni za lugha na mpangilio mzuri wa mawazo. | Mwanafunzi anatambua na kuandika insha ya maelezo inayojenga picha dhahiri na yenye kuzingatia baadhi ya kanuni za lugha na mpangilio mzuri wa mawazo. | Mwanafunzi anatambua na kuandika insha ya maelezo bila kuzingatia kanuni za lugha na mpangilio mzuri wa mawazo. |

| MADA | MADA NDOGO | MATOKEO MAALUM YANAYOTARAJIWA | MAPENDEKEZO YA SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI | SWALI DADISI |
|---|---|---|---|---|
| **5.4 Sarufi** | **5.4.1 Umoja na Wingi wa Nomino:** Ngeli ya U-ZI<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua nomino katika ngeli ya U-ZI<br>b) kuandika nomino za ngeli ya U-ZI katika umoja na wingi<br>c) kuandika umoja na wingi wa mafungu ya maneno katika ngeli ya U-ZI<br>d) kuchangamkia kutumia nomino za ngeli ya U-ZI katika mawasiliano. | Mwanafunzi:<br>• atambue nomino katika ngeli ya U-ZI kwenye kadi, mti wa maneno, tarakilishi au kapu la maneno *(k.m. Uzi-Nyuzi, Ukuta-Kuta, Uta- Nyuta, ubavu-mbavu, wakati-nyakati, ukucha-kucha na ufunguo-funguo, wimbo-nyimbo)*<br>• aandike nomino katika ngeli ya U-ZI katika umoja na wingi akiwa peke yake, wawiliwawili au katika vikundi<br>• asikize usomaji wa nomino za ngeli ya U-ZI kutoka kwenye tepurekoda au kinasasauti<br>• aandike mafungu ya maneno yenye nomino za ngeli ya U-ZI katika umoja na wingi<br>• ajaze mapengo kwa kutumia viambishi vya ngeli ya U-ZI kwa maandishi ya mkono au kwa tarakilishi. | 1. Je, ni nomino zipi hupatikana katika ngeli ya U-ZI? |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**
- Mawasiliano na ushirikiano – unakuzwa mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika vikundi
- Ubunifu – unakuzwa mwanafunzi anapoandika mafungu ya maneno
- Ujuzi wa kidijitali - unakuzwa tarakilishi inapotumika kutambua nomino na katika kusikiliza mafungu ya maneno kwenye kinasasauti

| Uhusiano na Masuala Mtambuko | Uhusiano na Maadili |
|---|---|
| • Utangamano – kufanya kazi kwa vikundi<br>• Stadi za Maisha - kujifanyia kazi darasani | • Uwajibikaji - kutunza vipakatalishi anavyotumia<br>• Uzalendo - kufanya kazi na wengine kwenye vikundi |

| Uhusiano na Masomo Mengine | Mapendekezo ya shughuli za huduma za Kijamii zinazochangia ujifunzaji: |
|---|---|
| • English na Indigenous Languages – masomo haya yanajumuisha mada za sarufi | • Mwanafunzi atatumia lugha kwa ufasaha kuimarisha mawasiliano katika jamii |

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kutambua nomino za ngeli ya U-ZI, viambishi vyake na kuzitumia kutunga mafungu sahihi yenye maana. | Mwanafunzi anatambua nomino za ngeli ya U-ZI, viambishi vyake na kuzitumia kutunga mafungu sahihi yenye maana kwa urahisi. | Mwanafunzi anatambua nomino za ngeli ya U-ZI, viambishi vyake na kuzitumia kutunga mafungu sahihi yenye maana. | Mwanafunzi anatambua baadhi ya nomino za ngeli ya U-ZI, viambishi vyake mbalimbali na kuzitumia kutunga mafungu sahihi yenye maana. | Mwanafunzi anatambua baadhi ya nomino za ngeli ya U-ZI, viambishi vyake mbalimbali na kuzitumia baadhi ya nomino alizotambua kutunga mafungu sahihi yenye maana. |

<table>
<tr><th>MADA</th><th>MADA NDOGO</th><th>MATOKEO MAALUM YANAYOTARAJIWA</th><th>MAPENDEKEZO YA SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI</th><th>SWALI DADISI</th></tr>
<tr><td>5.4 Sarufi</td><td>5.4.2 Umoja na wingi wa sentensi:<br>Ngeli ya U-ZI<br>(Vipindi 2)</td><td>Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua viambishi vipatanishi vya ngeli ya U-ZI kwenye sentensi<br>b) kuunda sentensi akitumia nomino za ngeli ya U-ZI katika umoja na wingi akizingatia upatanisho wa kisarufi<br>c) kufurahia matumizi ya ngeli ya U-ZI katika mawasiliano</td><td>Mwanafunzi:<br>• atambue viambishi vya ngeli ya U-ZI katika sentensi kwa kuvipigia mstari daftarini mwake au kuvikoleza rangi katika tarakilishi<br>• asikize usomaji wa sentensi zilizoundwa kutokana na nomino za ngeli ya U-ZI kutoka kwenye tepurekoda au kinasasauti<br>• aunde sentensi kwa kutumia nomino ya ngeli ya U-ZI akiwa peke yake au kwa kushirikiana na wengine<br>• ajaze mapengo kwa kutumia viambishi vya ngeli ya U-ZI kwa maandishi ya mkono au tarakilishi.</td><td>1. Je, nomino za ngeli ya U-ZI huchukua viambishi vipatanishi gani ?</td></tr>
<tr><td colspan="5">Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa<br>• Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anashirikiana na wenzake katika vikundi<br>• Ubunifu - mwanafunzi anapotunga sentensi<br>• Ujuzi wa kidijitali - kutumia tarakilishi kutambua maneno na katika kusikiliza sentensi kwenye tepurekoda</td></tr>
<tr><td colspan="3">Uhusiano na Masuala Mtambuko<br>• Uraia – kutokana na kufanya kazi katika vikundi<br>• Stadi za Maisha - kujifanyia kazi darasani</td><td colspan="2">Uhusiano na Maadili<br>• Uwajibikaji - kutunza vipakatalishi anavyotumia<br>• Uzalendo - kufanya kazi na wengine kwenye vikundi</td></tr>
<tr><td colspan="3">Uhusiano na Masomo Mengine<br>• English na Indigenous Languages – masomo haya yanafunza dhana ya nomino</td><td colspan="2">Mapendekezo ya shughuli za huduma za Kijamii zinazochangia ujifunzaji:<br>• Mwanafunzi atatumia lugha kwa ufasaha kuimarisha mawasiliano katika jamii.</td></tr>
</table>

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kutambua nomino za ngeli ya U-ZI, viambishi vyake mbalimbali na kutumia nomino za ngeli hii kutunga sentensi sahihi zenye maana kwa urahisi. | Mwanafunzi anatambua nomino za ngeli ya U-ZI, viambishi vyake mbalimbali na kutumia nomino za ngeli hii kutunga sentensi sahihi zenye maana kwa urahisi. | Mwanafunzi anatambua nomino za ngeli ya U-ZI, viambishi vyake mbalimbali na kutumia nomino za ngeli hii kutunga sentensi sahihi zenye maana. | Mwanafunzi anatambua baadhi ya nomino za ngeli ya U-ZI, viambishi vyake mbalimbali na kutumia nomino za ngeli hii kutunga sentensi sahihi zenye maana. | Mwanafunzi anatambua baadhi ya nomino za ngeli ya U-ZI, viambishi vyake mbalimbali na kutumia baadhi ya nomino alizotambua kutunga sentensi sahihi zenye maana. |

| 6.0 MAADILI | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **MADA** | **MADA NDOGO** | **MATOKEO MAALUMU YANAYOTARAJIWA** | **MAPENDEKEZO YA SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI** | **SWALI DADISI** |
| **6.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **6.1.1 Matamshi Bora:** Ushairi (Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kukariri shairi kwa kuzingatia matamshi na mahadhi mbalimbali<br>b) kueleza maana ya msamiati uliotumiwa katika shairi<br>c) kutumia msamiati uliotumiwa katika shairi kuboresha masiliano<br>d) kuonyesha ufahamu wa ujumbe katika shairi kwa kujibu maswali<br>e) kuchangamkia ushairi kama njia ya kujieleza kwa ufasaha. | Mwanafunzi:<br>• akariri shairi kuhusu mada lengwa (maadili) kwa kuzingatia matamshi na mahadhi mbalimbali<br>• asikilize shairi lengwa likikaririwa au kuimbwa na mwalimu, mgeni mwalikwa (mghani) au kupitia vifaa vya kidijitali<br>• ashirikiane na wenzake kukariri au kuimba shairi kwa mahadhi mbalimbali<br>• atambue msamiati uliotumika katika ushairi kuhusu maadili (*k.m. haki, usawa, heshima na uwajibikaji*) na kuueleza akiwa peke yake au kwa kushirikiana na wenzake<br>• ashirikiane na wenzake kujadili ujumbe katika shairi<br>• ajibu maswali yanayotokana na shairi alilosikiliza, aliloimba au kukariri | 1. Ushairi unaweza kuboresha mazungumzo yako vipi? |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**
- Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anashirikiana na wenzake katika vikundi
- Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anasikiliza shairi lililorekodiwa likikaririrwa kupitia vyombo vya kidijitali
- Kujiamini – mwanafunzi anajenga umilisi huu anapokariri shairi

| **Uhusiano na masuala mtambuko:** | **Uhusiano na Maadili:** |
|---|---|
| • Stadi maisha- anapokariri shairi kwa mahadhi mbalimbali | • Heshima – kuheshimu maoni ya wenzake katika vikundi<br>• Uwajibikaji – majukumu katika vikundi na kufuata mafunzo katika shairi |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>• English – somo hili linashughulikia mada ya ushairi<br>• Music – Muziki hushughulikia nyimbo za mahadhi mbalimbali | **Mapendekezo ya shughuli za huduma za kijamii zinazochangia ujifunzaji:**<br>• Mwanafunzi atawahamasisha wenzake shuleni na nyumbani kuhusu umuhimu wa mashairi katika kuboresha mazungumzo<br>• Mwanafunzi atawakariria watu mashairi katika hafla mbalimbali |

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kukariri au kuimba shairi kwa mahadhi mbalimbali kwa ufasaha | Mwanafunzi anakariri au kuimba shairi kwa mahadhi mbalimbali kwa ufasaha na urahisi | Mwanafunzi anakariri au kuimba shairi kwa mahadhi mbalimbali kwa ufasaha | Mwanafunzi anakariri au kuimba sehemu za shairi kwa kuzingatia mahadhi | Mwanafunzi anakariri au kuimba sehemu za shairi bila mahadhi murua. |
| Kueleza na kutumia msamiati lengwa katika tungo kwa usahihi | Mwanafunzi anaeleza msamiati uliofunzwa na kuutumia katika tungo kwa usahihi na urahisi | Mwanafunzi anaeleza msamiati uliofunzwa na kuutumia katika tungo kwa usahihi. | Mwanafunzi anaeleza baadhi ya msamiati na kuutumia katika tungo kwa usahihi. | Mwanafunzi anaeleza baadhi ya msamiati uliofunzwa na kutumia baadhi ya msamiati huo katika tungo. |
| Kujibu maswali yanayolenga ujumbe, matukio na wahusika katika shairi kwa usahihi | Mwanafunzi anajibu maswali yanayolenga ujumbe, matukio na wahusika katika shairi kwa usahihi na urahisi | Mwanafunzi anajibu maswali yanayolenga ujumbe, matukio na wahusika katika shairi kwa usahihi | Mwanafunzi anajibu baadhi ya maswali yanayolenga ujumbe na wahusika katika shairi kwa usahihi | Mwanafunzi anajibu baadhi ya maswali yanayolenga wahusika katika shairi |

| MADA | MADA NDOGO | MATOKEO MAALUMU YANAYOTARAJIWA | MAPENDEKEZO YA SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI | MASWALI DADISI |
|---|---|---|---|---|
| **6.2 Kusoma** | **6.2.1 Kusoma kwa Mapana:** Makala (Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) Kutambua makala ya kusoma katika maktaba ili kuimarisha uchaguzi bora wa makala<br>b) kusoma makala mbalimbali ili kujenga ufasaha wa lugha<br>c) kufurahia kusoma makala mbalimbali ili kujenga ufasaha wa lugha. | Mwanafunzi:<br>• achague makala atakayosoma katika maktaba<br>• asome makala ya aina mbalimbali ya kujichagulia<br>• ajadiliane na wenzake kuhusu makala aliyoyasoma na alichojifunza kutokana na makala hayo<br>• atumie kamusi kupata maana za msamiati uliotumika katika makala.<br>• asaidiwe na mzazi au mlezi wake kupata makala zaidi na kuyasoma ili kujenga mazoea ya usomaji. | 1. Unapenda kusoma makala ya aina gani?<br>2. Ni ujumbe upi uliopata kwenye makala uliyowahi kusoma? |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anapojadiliana na wenzake katika vikundi
- Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anaposoma makala katika blogi
- Kujiamini – mwanafunzi anajenga umilisi huu anaposimulia alichokisoma

| Uhusiano na masuala mtambuko: | Uhusiano na Maadili: |
|---|---|
| • Stadi za maisha – uwezo wa kuongoza na kuelekeza usomaji wake<br>• Ushauri nasaha – anaposoma masuala ya kimaadili katika matini anayoyasoma | • Heshima, upendo, uzalendo – anaposoma matini mbalimbali na kuzingatia mchango wa wenzake |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>• English na Indigenous Languages– Masomo haya hulenga kukuza umilisi wa kusoma kama mojawapo ya stadi za lugha | **Mapendekezo ya shughuli za huduma za kijamii zinazochangia ujifunzaji:**<br>• Mwanafunzi atatumia mawazo na maadili aliyopata kutokana na hadithi kuelekeza wenzake |

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kusoma kwa kuzingatia ujumbe, vipengele vya matini na kueleza alichokisoma kwa ufasaha | Mwanafunzi anasoma akizingatia ujumbe, vipengele vya matini na kueleza alichokisoma kwa ufasaha na wepesi | Mwanafunzi anasoma akizingatia ujumbe, vipengele vya matini na anaweza kueleza alichokisoma kwa ufasaha | Mwanafunzi anasoma akizingatia sehemu za ujumbe, anafahamu baadhi ya vipengele vya matini na kueleza baadhi ya yale aliyoyasoma | Mwanafunzi anasoma sehemu za matini |

| MADA | MADA NDOGO | MATOKEO MAALUMU YANAYOTARAJIWA | MAPENDEKEZO YA SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI | MASWALI DADISI |
|---|---|---|---|---|
| **6.3 Kuandika** | **6.3.1 Kuandika Insha:** Insha za Wasifu<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua vipengele vya kimuundo vya insha za wasifu.<br>b) kuandika insha ya wasifu kwa kuzingatia muundo na mtindo ufaao<br>c) kufurahia uandishi wa insha za wasifu ili kukuza stadi ya kuandika. | Mwanafunzi:<br>• atazame nakala za insha za wasifu kwenye chapa au kwenye tarakilishi.<br>• atambue vipengele muhimu vya kimuundo kama vile kichwa, mwili, hitimisho<br>• ajadili na wenzake kuhusu kinachoweza kuandikiwa katika insha ya wasifu *(k.v. mtu, kitu, mnyama na mahali)*<br>• ajadili na wenzake kuhusu mada mbalimbali zinazoweza kutungiwa insha za wasifu *k.m. mwanafunzi mwadilifu, mtu aliyeshinda tuzo kwa wadilifu wake* n.k.<br>• aandike insha ya wasifu isiyopungua maneno 150 daftarini au kwenye tarakilishi.<br>• awasomee wenzake insha aliyoiandika ili kuitathmini. | 1. Unazingatia nini unapoandika insha ya wasifu? |

**Umilisi wa Kimsingi unaokuzwa**
- Hamu ya ujifunzaji - mwanafunzi anapotaja mada mbalimbali zinazoweza kutungiwa insha za wasifu.
- Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anapotumia tarakilishi katika utungaji wa insha ya wasifu.

| **Uhusiano na Masuala Mtambuko** | **Uhusiano na Maadili** |
|---|---|
| • Stadi za maisha – anapotunga insha kueleza sifa za watu, mahali au vitu.<br>• Uraia – anapofanya kazi pamoja na wenzake darasani. | • Heshima – anaposikiliza kwa makini wenzake wakisoma insha zao.<br>• Uwajibikaji – anapofanya kazi ya darasani na kuikamilisha kwa wakati. |
| **Uhusiano na masomo mengine** | **Shughuli za kijamii zinazochangia ujifunzaji** |
| • English na Indigenous Languages– Masomo haya yanashughulikia uandishi kama mojawapo ya stadi nne za lugha | • Anaposhiriki katika ziara za kielimu na kutagusana na watu, hali na vitu mbalimbali. |

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kutambua na kuandika insha ya wasifu kwa kuzingatia vipengele vya kimuundo na kimtindo kwa usahihi | Mwanafunzi anatambua na kuandika insha ya wasifu kwa kuzingatia vipengele vya kimuundo na kimtindo kwa usahihi na kwa ufasaha | Mwanafunzi anatambua na kuandika insha ya wasifu kwa kuzingatia vipengele vya kimuundo na kimtindo kwa usahihi | Mwanafunzi anatambua na kuandika insha ya wasifu kwa kuzingatia baadhi ya vipengele vya kimuundo na kimtindo kwa usahihi | Mwanafunzi anaandika insha ya wasifu bila kuzingatia vipengele vya kimuundo na kimtindo |

| MADA | MADA NDOGO | MATOKEO MAALUM YANAYOTARAJIWA | MAPENDEKEZO YA SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI | SWALI DADISI |
|---|---|---|---|---|
| **6.4 Sarufi** | **6.4.1 Umoja na Wingi wa Nomino:** Ngeli ya U-YA<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua nomino katika ngeli ya U-YA ili kuzitofautisha na nomino katika ngeli nyingine<br>b) kuandika nomino za ngeli ya U-YA katika umoja na wingi<br>c) kuandika umoja na wingi wa mafungu ya maneno katika ngeli ya ngeli ya U-YA<br>d) kuchangamkia kutumia nomino za ngeli ya U-YA katika mawasiliano. | Mwanafunzi:<br>• atambue nomino katika ngeli ya U-YA kwenye kadi, mti wa maneno, tarakilishi au kapu la maneno (*kama vile upishi, ulezi, ugonjwa)* aandike nomino katika ngeli ya U-YA katika umoja na wingi akiwa peke yake, wawiliwawili au katika vikundi<br>• asikize usomaji wa nomino za ngeli ya U-YA kutoka kwenye tepurekoda au kinasa sauti<br>• aandike mafungu ya maneno yenye nomino za ngeli ya U-YA katika umoja na wingi<br>• ajaze mapengo kwa kutumia viambishi vya ngeli ya U-YA kwa maandishi ya mkono au kwa tarakilishi. | 1.Je, ni nomino zipi hupatikana katika ngeli ya U-YA? |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**
- Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anashirikiana na wenzake katika vikundi
- Ubunifu - mwanafunzi anapotunga maneno
- Ujuzi wa kidijitali – kutumia tarakilishi kutambua nomino na ngeli zake

| **Uhusiano na Masuala Mtambuko** | **Uhusiano na Maadili** |
|---|---|
| • Utangamano – kufanya kazi kwa vikundi<br>• Stadi za Maisha - kujifanyia kazi darasani | • Uwajibikaji - kutunza vipakatalishi anavyotumia<br>• Uzalendo - kufanya kazi na wengine kwenye vikundi |
| **Uhusiano na Masomo Mengine** | **Mapendekezo ya shughuli za huduma za Kijamii zinazochangia ujifunzaji:** |
| • English na Indigenous Languages – masomo haya yanajumuisha ngeli za nomino | • Mwanafunzi atatumia lugha kwa ufasaha kuimarisha mawasiliano katika jamii |

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kutambua nomino za ngeli ya U-YA, kuziandika katika umoja na wingi na kuzitumia kutunga mafungu sahihi. | Mwanafunzi anatambua kwa wepesi nomino za ngeli ya U-YA, anaziandika katika umoja na wingi na kuzitumia kutunga mafungu sahihi. | Mwanafunzi anatambua nomino za ngeli ya U-YA, anaziandika katika umoja na wingi na kuzitumia kutunga mafungu sahihi. | Mwanafunzi anatambua baadhi ya nomino za ngeli ya U-YA, anaziandika katika umoja na wingi na kuzitumia kutunga mafungu sahihi. | Mwanafunzi anatambua baadhi ya nomino za ngeli ya U-YA, anaandika baadhi ya nomino alizotambua katika umoja na wingi na kuzitumia kutunga mafungu. |

<table>
<tr><th>MADA</th><th>MADA NDOGO</th><th>MATOKEO MAALUM YANAYOTARAJIWA</th><th>MAPENDEKEZO YA SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI</th><th>SWALI DADISI</th></tr>
<tr><td>6.4 Sarufi</td><td>6.4.2 Umoja na wingi wa sentensi: Ngeli ya U-YA<br>(Vipindi 2)</td><td>Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua viambishi vipatanishi vya ngeli ya U-YA kwenye sentensi<br>b) kuunda sentensi akitumia nomino za ngeli ya U-YA katika umoja na wingi akizingatia upatanisho wa kisarufi<br>c) kufurahia matumizi ya ngeli ya U-YA katika mawasiliano</td><td>Mwanafunzi:<br>• atambue viambishi vya ngeli ya U-YA katika sentensi kwa kuvipigia mstari daftarini mwake au kuvikoleza rangi katika tarakilishi<br>• atumie nomino za ngeli ya U-YA katika sentensi akiwa peke yake, wawiliwawili au katika vikundi<br>• asikize usomaji wa sentensi zilizoundwa kutokana na nomino za ngeli ya U-YA kutoka kwenye tepurekoda au kinasa sauti<br>• aunde sentensi kwa kutumia nomino ya ngeli ya U-YA akiwa peke yake au kwa kushirikiana na wengine<br>• ajaze mapengo kwa kutumia viambishi vya ngeli ya U-YA kwa maandishi ya mkono au tarakilishi.</td><td>1. Je, nomino za ngeli ya U-YA huchukua viambishi gani katika sentensi?</td></tr>
<tr><td colspan="5">Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa<br>• Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anashirikiana na wenzake katika vikundi<br>• Ubunifu - mwanafunzi anapotunga sentensi<br>• Ujuzi wa kidijitali - kutumia tarakilishi kutambua maneno na katika kusikiliza sentensi kwenye tepurekoda</td></tr>
<tr><td colspan="3">Uhusiano na Masuala Mtambuko<br>• Uraia – kufanya kazi kwa vikundi<br>• Stadi za Maisha - kujifanyia kazi darasani</td><td colspan="2">Uhusiano na Maadili<br>• Uwajibikaji - kutunza vipakatalishi anavyotumia<br>• Umoja - kufanya kazi na wengine kwenye vikundi</td></tr>
<tr><td colspan="3">Uhusiano na Masomo Mengine<br>• English na Indigenous Languages – masomo haya yanafunza ngeli za nomino</td><td colspan="2">Mapendekezo ya shughuli za huduma za Kijamii zinazochangia ujifunzaji:<br>• Mwanafunzi atatumia lugha kwa ufasaha kuimarisha mawasiliano katika jamii.</td></tr>
</table>

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kutambua nomino za ngeli ya U-YA, viambishi vyake na kutumia nomino za ngeli hii kutunga sentensi sahihi zenye maana. | Mwanafunzi anatambua nomino za ngeli ya U-YA, viambishi vyake na kutumia nomino za ngeli hii kutunga sentensi sahihi zenye maana kwa urahisi. | Mwanafunzi anatambua nomino za ngeli ya U-YA, viambishi vyake na kutumia nomino za ngeli hii kutunga sentensi sahihi zenye maana. | Mwanafunzi anatambua baadhi ya nomino za ngeli ya U-YA, viambishi vyake na kutumia nomino za ngeli hii kutunga sentensi sahihi zenye maana. | Mwanafunzi anatambua baadhi ya nomino za ngeli ya U-YA, viambishi vyake na kutumia baadhi ya nomino alizotambua kutunga sentensi sahihi zenye maana. |

## 7.0 ELIMU YA MAZINGIRA

| MADA | MADA NDOGO | MATOKEO MAALUM YANAYOTARAJIWA | MAPENDEKEZOYA SHUGHULIZA UJIFUNZAJI | MASWALI DADISI |
|---|---|---|---|---|
| **7.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **7.1.1 Nahau:** Nahau za usafi na mazingira (Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua nahau za usafi na mazingira katika matini mbalimbali<br>b) kufafanua maana ya nahau mbalimbali za kazi na ushirikiano kwa kutoa mifano<br>c) kutumia nahau za usafi na mazingira katika mawasiliano<br>d) kuthamini matumizi ya nahau za usafi na mazingira katika mawasiliano. | Mwanafunzi:<br>• atambue nahau za usafi na mazingira (*k.v. angua kucha, penga kamasi*, *piga deki*, *piga mswaki*, *chokonoa meno, futa vumbi*) katika chati, michoro, picha, vikapu maneno, mti maneno, chati, kamusi na katika vyombo vya kidijitali<br>• ashiriki katika kujadili na wenzake maana za nahau za usafi na mazingira na kutoa mifano<br>• kutumia nahau za usafi na mazingira kutunga sentensi akiwa pekee au kwa kushirikiana na wenzake<br>• ashirikiane na wenzake kujaza mapengo katika sentensi kwa kutumia nahau mwafaka kwenye zoezi la ubaoni, vitabuni au katika tarakilishi. | 1) Je, ni nahau zipi zinahusu usafi?<br>2) Je, ni nahau zipi zinahusu mazingira? |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**
- Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za vikundi
- Ujuzi wa kijidijitali – matumizi ya vifaa vya kidijitali katika kutambua nahau za usafi na mazingira
- Hamu ya kuendelea kujifunza – mwanafunzi anapotafuta maana za nahau na kuzitumia kwa ufasaha katika mawasiliano
- Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo – mwanafunzi anapofikiria kuhusu maana za nahau na matumizi yake

**Uhusiano na Masuala Mtambuko**
- Umoja wa kijamii – majadiliano kwa vikundi
- Stadi za Maisha (kujiamini) – mwanafunzi anapotumia nahau kuimarisha mawasiliano

**Uhusiano na Maadili**
- Umoja – kutokana na kufanya katika vikundi
- Heshima – mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika vikundi

**Uhusiano na Masomo Mengine**
- English na Indigenous Languages – masomo haya hufunza mada ya nahau

**Mapendekezo ya Shughuli za Huduma za Kijamii Zinazochangia Ujifunzaji**:
- Mwanafunzi kuwa kielelezo kwa wengine katika utumiaji wa lugha kiubunifu.

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kutambua nahau za usafi na mazingira, kueleza maana za nahau hizo na kuzitumia kujieleza kwa ufasaha. | Mwanafunzi anatambua nahau za usafi na mazingira, anaeleza maana za nahau hizo na kuzitumia kujieleza kwa ufasaha na kwa urahisi. | Mwanafunzi anatambua nahau za usafi na mazingira, anaeleza maana za nahau hizo na kuzitumia kujieleza kwa ufasaha. | Mwanafunzi anatambua baadhi ya nahau za usafi na mazingira, anaeleza maana za nahau hizo na kuzitumia kujieleza kwa ufasaha. | Mwanafunzi anatambua baadhi ya nahau za usafi na mazingira, anaeleza maana za baadhi ya nahau hizo na kuzitumia kujieleza. |

<table>
<tr><th>MADA</th><th>MADA NDOGO</th><th>MATOKEO MAALUM YANAYOTARAJIWA</th><th>MAPENDEKEZO YA SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI</th><th>MASWALI DADISI</th></tr>
<tr><td>7.2 Kusoma</td><td>7.2.1 Kusoma kwa Mapana: Matini<br>(Vipindi 3)</td><td>Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua matini anazotaka kusoma kwenye maktaba<br>b) kusoma matini ili kufaidika na ujumbe na lugha inayotumiwa<br>c) kufurahia usomaji wa matini za aina mbalimbali ili kujenga utamaduni wa kusoma</td><td>Mwanafunzi:<br>• atambue aina mbalimbali za matini (kama vile vitabu, magazeti, na majarida) kwenye maktaba, tarakilishi au kadi za katalogi.<br>• achague matini atakayosoma<br>• asome matini kimyakimya ili kupata ujumbe uliopo na kufaidi matumizi ya lugha.<br>• asimulie ujumbe kutokana na matini alizosoma kwa wenzake.<br>• ajadiliane na wenzake matini alizosoma ili kuchochea hamu ya usomaji wa mapana miongoni mwao.</td><td>1) Unapenda kusoma matini ya aina gani?<br>2) Ni vipi unavyoweza kupata matini ya kusoma?<br>3) Kusoma aina mbalimbali za matini kuna umuhimu gani?</td></tr>
<tr><td colspan="5">Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa<br>• Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anaposoma na kusimulia ujumbe aliosoma kutokana na matini za aina mbalimbali<br>• Hamu ya ujifunzaji –mwanafunzi anapotagusana na matini za aina mbalimbali maktabani.</td></tr>
<tr><td colspan="3">Uhusiano na Masuala Mtambuko<br>• Stadi za maisha – anapojenga uwezo wa kujichagulia matini kuhusu afya na mazingira<br>• Elimu na maendeleo endelevu;mazingira- anaposoma matini kuhusu mazingira.</td><td colspan="2">Uhusiano na Maadili<br>• Heshima – anaposhirikiana na wengine na kuzingatia maoni katika mijadala.<br>• Uwajibikaji – anapoazima, kutunza na kurudisha vitabu maktabani.</td></tr>
<tr><td colspan="3">Uhusiano na masomo mengine<br>• Social Studies hufunza mada ya mazingira<br>• English – hufunza stadi ya kusoma kwa mapana</td><td colspan="2">Shughuli za kijamii zinazochangia ujifunzaji<br>• Anapotumia maarifa aliyoyapata katika utunzaji wa mazingira kuihamasisha jamii.</td></tr>
</table>

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Utamaduni mzuri wa kutambua na kusoma matini za aina mbalimbali shuleni na nje ya shule na kusimulia kwa ufasaha alichokisoma | Mwanafunzi ana utamaduni mzuri wa kutambua na kusoma matini za aina mbalimbali shuleni na nje ya shule na anapenda kusimulia kwa ufasaha alichokisoma | Mwanafunzi ana utamaduni mzuri wa kutambua na kusoma matini za aina mbalimbali shuleni na nje ya shule na kusimulia kwa ufasaha alichokisoma | Mwanafunzi ana utamaduni wa kutambua na kusoma baadhi ya sampuli za matini shuleni na kuzisimulia | Mwanafunzi anasoma baadhi ya matini shuleni |

| MADA | MADA NDOGO | MATOKEO MAALUMU YANAYOTARAJIWA | MAPENDEKEZO YA SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI | SWALI DADISI |
|---|---|---|---|---|
| **7.3 Kuandika** | **7.3.1 Kuandika insha:** Insha ya Maelezo (Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua insha za maelezo katika matini mbalimbali<br>b) kuandika insha ya maelezo kwa kuzingatia muundo na mtindo ufaao<br>c) kuchangamkia utungaji wa insha za maelezo ili kuimarisha uandishi bora. | Mwanafunzi:<br>• atambue vifungu vya insha za maelezo vilivyoandikwa kwenye matini mbalimbali au tarakilishi (*k.v. maelezo kuhusu upandaji wa miche, kusafisha darasa, kufua nguo, kuzuia mmomonyoko wa udongo, kupanda miti)*<br>• ashiriki na wenzake kujadili mada ya insha na muundo wa insha ya maelezo<br>• aandike insha ya maelezo isiyopungua maneno 150 akizingatia anwani, mpangilio mzuri wa mawazo, hati safi, tahajia, kanuni za kisarufi, uakifishaji mwafaka na kwa lugha ya kiubunifu unaojumuisha methali na nahau alizojifunza awali<br>• atunge insha ya maelezo mtandaoni na kuisambaza kwa wenzake na mwalimu ili kuisoma na kuitathmini<br>• awasomee wenzake insha aliyoandika ili kuisikiliza na kuitathmini. | 1. Je, ni shughuli gani zinazoweza kuandikiwa insha za maelezo? |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa**:
- Mawasiliano na ushirikiano – Huu unakuzwa wanafunzi wanaposhiriki katika mijadala na kazi za vikundi
- Ujuzi wa kidijitali – Huu unakuzwa wakati vifaa vya kiteknolojia vinapotumiwa kuandika insha mtandaoni na kurejelea kielelezo cha insha ya maelezo
- Ubunifu – Huu unajengeka mwanafunzi anapoandika insha ya maelezo
- Hamu ya ujifunzaji – Huu unakuzwa mwanafunzi anapoyatafakari maswali dadisi na anapoimarisha ujuzi wake wa kutumia tarakilishi

| | |
|---|---|
| **Uhusiano na masuala mtambuko**:<br>• Uraia kutokana na kufanya kazi pamoja.<br>• Stadi za maisha – anapotunga insha na kujieleza kwa kurejelea mazingira anamoishi | **Uhusiano na Maadili**:<br>• Heshima na adabu hasa katika shughuli za vikundi |
| **Uhusiano na masomo mengine**:<br>• English na Indigeneous Language – masomo haya yana mada kuhusu uandishi. | **Mapendekezo ya shughuli za huduma za kijamii zinazochangia ujifunzaji**:<br>• Kuwahamasisha wenzake shuleni na nyumbani kuhusu umuhimu wa uandishi mzuri katika mawasiliano<br>• Kuwaelezea wengine kuhusu umuhimu wa kuhifadhi mazingira. |

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kuandika insha ya maelezo inayojenga picha dhahiri, yenye kuzingatia kanuni za lugha na mpangilio mzuri wa mawazo. | Mwanafunzi anaandika kwa ufasaha insha ya maelezo inayojenga picha dhahiri, yenye kuzingatia kanuni za lugha na mpangilio mzuri wa mawazo. | Mwanafunzi anaandika insha ya maelezo inayojenga picha dhahiri, yenye kuzingatia kanuni za lugha na mpangilio mzuri wa mawazo. | Mwanafunzi anaandika insha ya maelezo inayojenga picha dhahiri, yenye kuzingatia kanuni za lugha na mpangilio mzuri wa mawazo. | Mwanafunzi anaandika insha ya maelezo bila kujenga picha dhahiri ya anachoandikia. |

| MADA | MADA NDOGO | MATOKEO MAALUM YANAYOTARAJIWA | MAPENDEKEZO YA SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI | SWALI DADISI |
|---|---|---|---|---|
| **7.4 Sarufi** | **7.4.1 Umoja na wingi wa nomino:** Ngeli ya KU-KU<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua nomino katika ngeli ya KU-KU<br>b) kuandika nomino za ngeli ya KU-KU katika umoja na wingi<br>c) kuandika umoja na wingi wa mafungu ya maneno katika ngeli ya ngeli ya KU-KU<br>d) kuchangamkia kutumia nomino za ngeli ya KU-KU katika mawasiliano. | Mwanafunzi:<br>• atambue nomino katika ngeli ya KU-KU (kama vile *kupika, kufyeka, kuzuru, kukariri, kufua)* kwenye kadi, mti wa maneno, tarakilishi au kapu la maneno<br>• aandike nomino katika ngeli ya KU-KU katika umoja na wingi akiwa peke yake, wawiliwawili au katika vikundi<br>• asikize usomaji wa nomino za ngeli ya KU-KU kutoka kwenye tepurekoda au kinasa sauti<br>• aandike mafungu ya maneno yenye nomino za ngeli ya KU-KU katika umoja na wingi<br>• ajaze mapengo kwa kutumia viambishi vya ngeli ya KU-KU kwa maandishi ya mkono au kwa tarakilishi. | 1. Je, ni nomino zipi hupatikana katika ngeli ya KU-KU? |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**
- Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anashirikiana na wenzake katika vikundi
- Ubunifu - mwanafunzi anapotunga maneno
- Ujuzi wa kidijitali - kutumia tarakilishi kutambua nomino na ngeli zake

| Uhusiano na Masuala Mtambuko | Uhusiano na Maadili |
|---|---|
| • Utangamano – kufanya kazi kwa vikundi<br>• Stadi za Maisha - kujifanyia kazi darasani | • Uwajibikaji - kutunza vipakatalishi anavyotumia<br>• Uzalendo - kufanya kazi na wengine kwenye vikundi |
| **Uhusiano na Masomo Mengine** | **Mapendekezo ya shughuli za huduma za Kijamii zinazochangia ujifunzaji:** |
| • English na Indigenous Languages – masomo haya yanajumuisha mada ngeli za nomino | • Mwanafunzi atatumia lugha kwa ufasaha kuimarisha mawasiliano katika jamii |

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kutambua nomino za ngeli ya KU-KU, viambishi vyake mbalimbali na kuzitumia kutunga mafungu sahihi yenye maana. | Mwanafunzi anatambua nomino za ngeli ya KU-KU, viambishi vyake mbalimbali na kuzitumia kutunga mafungu sahihi yenye maana kwa urahisi. | Mwanafunzi anatambua nomino za ngeli ya KU-KU, viambishi vyake mbalimbali na kuzitumia kutunga mafungu sahihi yenye maana. | Mwanafunzi anatambua baadhi ya nomino za ngeli ya KU-KU, viambishi vyake mbalimbali na kuzitumia kutunga mafungu sahihi yenye maana. | Mwanafunzi anatambua baadhi ya nomino za ngeli ya KU-KU, viambishi vyake mbalimbali na kuzitumia baadhi ya nomino alizotambua kutunga mafungu sahihi yenye maana. |

| MADA | MADA NDOGO | MATOKEO MAALUM YANAYOTARAJIWA | MAPENDEKEZO YA SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI | SWALI DADISI |
|---|---|---|---|---|
| **7.4 Sarufi** | **7.4.2 Umoja na wingi wa sentensi:** Ngeli ya KU-KU<br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua viambishi vipatanishi vya ngeli ya KU-KU kwenye sentensi<br>b) kuunda sentensi akitumia nomino za ngeli ya KU-KU katika umoja na wingi akizingatia upatanisho wa kisarufi<br>c) kufurahia matumizi ya ngeli ya KU-KU katika mawasiliano | Mwanafunzi:<br>• atambue viambishi vya ngeli ya KU-KU katika sentensi kwa kuvipigia mstari au kuvikoleza rangi katika tarakilishi<br>• atumie nomino za ngeli ya KU-KU katika sentensi akiwa peke yake, wawiliwawili au katika vikundi<br>• asikize usomaji wa sentensi zilizoundwa kutokana na nomino za ngeli ya KU-KU kutoka kwenye tepurekoda au kinasa sauti<br>• aunde sentensi kwa kutumia nomino ya ngeli ya KU-KU akiwa peke yake au kwa kushirikiana na wenzake<br>• ajaze mapengo kwa kutumia viambishi vya ngeli ya KU-KU kwa maandishi ya mkono au tarakilishi. | 1. Je, nomino za ngeli ya KU-KU huchukua viambishi gani katika sentensi? |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**
- Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anashirikiana na wenzake katika vikundi
- Ubunifu - mwanafunzi anapotunga sentensi
- Kufikiri kwa kina - mwanafunzi anapowaza kwa kina kuhusu atakachoandika
- Ujuzi wa kidijitali - kutumia tarakilishi kutambua maneno na katika kusikiliza sentensi kwenye tepurekoda

| **Uhusiano na Masuala Mtambuko** | **Uhusiano na Maadili** |
|---|---|
| • Utangamano – kufanya kazi kwa vikundi<br>• Stadi za Maisha – kujifanyia kazi darasani | • Uwajibikaji - kutunza vipakatalishi anavyotumia<br>• Uzalendo - kufanya kazi na wengine kwenye vikundi |
| **Uhusiano na Masomo Mengine** | **Mapendekezo ya shughuli za huduma za Kijamii zinazochangia ujifunzaji:** |
| • English na Indigenous Languages – masomo haya yanafunza sarufi | • Mwanafunzi atatumia lugha kwa ufasaha kuimarisha mawasiliano katika jamii. |

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kutambua nomino za ngeli ya KU-KU, viambishi vyake mbalimbali na kutumia nomino za ngeli hii kutunga sentensi sahihi zenye maana kwa urahisi. | Mwanafunzi anatambua nomino za ngeli ya KU-KU, viambishi vyake mbalimbali na kutumia nomino za ngeli hii kutunga sentensi sahihi zenye maana kwa urahisi. | Mwanafunzi anatambua nomino za ngeli ya KU-KU, viambishi vyake mbalimbali na kutumia nomino za ngeli hii kutunga sentensi sahihi zenye maana. | Mwanafunzi anatambua baadhi ya nomino za ngeli ya KU-KU, viambishi vyake mbalimbali na kutumia nomino za ngeli hii kutunga sentensi sahihi zenye maana. | Mwanafunzi anatambua baadhi ya nomino za ngeli ya KU-KU, viambishi vyake mbalimbali na kutumia baadhi ya nomino alizotambua kutunga sentensi sahihi zenye maana. |

<table>
<tr><th colspan="5">8.0 NDEGE WA PORINI</th></tr>
<tr><th>MADA</th><th>MADA NDOGO</th><th>MATOKEO MAALUM YANAYOTARAJIWA</th><th>MAPENDEKEZO YA SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI</th><th>SWALI DADISI</th></tr>
<tr><td>8.1 Kusikiliza na Kuzungumza</td><td>8.1.1 Visawe: Visawe vya maneno matatu (Vipindi 2)</td><td>Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua maneno matatu yenye maana sawa katika kundi la maneno<br>b) kutumia visawe ifaavyo katika mawasiliano<br>c) kuthamini matumizi ya maneno matatu yenye maana sawa katika mawasiliano</td><td>Mwanafunzi:<br>• atambue maneno matatu yenye maana sawa (k.v. nyumbani- kiamboni, mastakimuni, chengoni. Barabara- tariki, gurufa, baraste. Jitimai- huzuni, kihoro, simanzi) kwa kutumia kapu la maneno, kadi za maneno, mti maneno, kuburura kwa kutumia tarakilishi, n.k.<br>• kueleza maana ya maneno matatu yenye maana sawa akiwa peke yake au kwa kujadiliana na wenzake<br>• kuambatanisha maneno matatu yenye maana sawa katika kapu maneno, mti maneno, ubao, chati, vyombo vya kidijitali, kadi maneno n.k<br>• ahusishe visawe na vifaa halisi, picha, michoro kwenye chati, kitabu au katika vyombo vya kidijitali n.k.<br>• ashiriki kujadili visawe mbalimbali katika vikundi vya wanafunzi wawiliwawili au zaidi<br>• atumie kisawe kimoja kuchukua nafasi ya kingine katika sentensi.</td><td>1. Unajua maneno gani ya Kiswahili yaliyo na maana sawa?</td></tr>
<tr><td colspan="5">Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa<br>• Mawasiliano na ushirikiano - kwa kufanya kazi katika vikundi<br>• Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo - kwa kufikiria visawe mwafaka<br>• Ujuzi wa kidigitali - anapotumia vifaa vya kidijitali</td></tr>
<tr><td colspan="3">Uhusiano na Masuala Mtambuko<br>• Umoja wa kijamii kwa kufanya kazi katika vikundi<br>• Stadi za Maisha - katika kujieleza kwa visawe mbalimbali</td><td colspan="2">Uhusiano na Maadili<br>Sentensi zitakazorejelewa zijumuishe maadili mbalimbali kv umoja, uzalendo, uwajibikaji, upendo n.k.</td></tr>
</table>

| Uhusiano na Masomo Mengine | Mapendekezo ya shughuli za huduma za Kijamii zinazochangia ujifunzaji: |
|---|---|
| • English – somo linafunza mada ya visawe | • Mwanafunzi awe kielelezo kwa wanajamii katika kutumia lugha mwafaka na maneno tofauti kujieleza |

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kutambua maneno matatu yenye maana sawa na kutumia visawe vifaavyo katika sentensi. | Mwanafunzi anatambua maneno matatu yenye maana sawa na kutumia visawe vifaavyo katika sentensi kwa urahisi. | Mwanafunzi anatambua maneno matatu yenye maana sawa na kutumia visawe vifaavyo katika sentensi. | Mwanafunzi anatambua baadhi ya maneno matatu yenye maana sawa na anatumia visawe hivyo ifaavyo katika sentensi. | Mwanafunzi anatambua baadhi maneno matatu yenye maana sawa na anatumia baadhi ya visawe alivyotambua katika sentensi. |

| MADA | MADA NDOGO | MATOKEO MAALUM YANAYOTARAJIWA | MAPENDEKEZO YA SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI | MASWALI DADISI |
|---|---|---|---|---|
| **8.2 Kusoma** | **8.2.1 Kusoma kwa Ufahamu:** Mchezo wa kuigiza<br>(Vipindi 3) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua mchezo wa kuigiza katika matini<br>b) kusoma mchezo mfupi wa kuigiza kwa ufasaha<br>c) kueleza maana ya msamiati uliotumiwa katika mchezo wa kuigiza<br>d) kuonyesha ufahamu wa mchezo wa kuigiza kwa kujibu maswali<br>e) kuigiza mchezo mfupi ili kukuza uwezo wa kujieleza<br>f) kufurahia kusoma michezo na kuigiza. | Mwanafunzi:<br>• aeleze maana ya mchezo wa kuigiza akiwa peke yake, wawiliwawili au katika kikundi<br>• atambue mchezo wa kuigiza, wahusika na maelekezo katika matini mbalimbali kama vile vitabu, chati na vilevile kwa kutumia tarakilishi<br>• asome mchezo wa kuigiza akizingatia wahusika, maelekezo na ujumbe<br>• ashiriki katika majadiliano kuhusu msamiati wa suala lengwa (ndege wa porini) uliotumiwa katika mchezo wa kuigiza (*k.v. chiriku, kasuku, tai, korongo, mwewe na kanga*)<br>• atazame mchezo mfupi wa kuigiza ukiigizwa darasani au kwenye vifaa vya kidijitali<br>• aigize mchezo mfupi aliousoma akishirikiana na wenzake<br>• ashiriki mjadala kuhusu ujumbe unaojitokeza kwenye mchezo wa kuigiza<br>• asome mchezo wa kuigiza kwenye mtandao<br>• ashiriki katika kutoa muhtasari wa mchezo aliousoma<br>• kuuliza na kujibu maswali ya ufahamu | 1) umewahi kusoma michezo ipi ya kuigiza?<br>2) Unakumbuka nini katika mchezo uliowahi kuusoma?<br>3) Kusoma michezo ya kuigiza kuna umuhimu gani? |

| |
|---|
| **Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**<br>• Mawasiliano na ushirikiano – wanafunzi wanaposhiriki katika kazi za vikundi<br>• Ujuzi wa kidijitali – matumizi ya kidijitali kufanikisha somo<br>• Uwazaji kina – mwanafunzi anapong’amua ujumbe uliomo kwenye mchezo<br>• Kujiamini – anaposhiriki katika kusoma na kuigiza mchezo |

| **Uhusiano na Masuala Mtambuko** | **Uhusiano na Maadili** |
|---|---|
| • Elimu ya maendeleo endelevu – mwanafunzi anapowathamini ndege wa | • Heshima – heshima kwa wanyama wa porini na kuendeleza shughuli za |

| | |
|---|---|
| porini | vikundi |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>• English na Indigenous languages – masomo haya yanajumuisha usomaji wa michezo mifupi | **Mapendekezo ya shughuli za huduma za Kijamii zinazochangia ujifunzaji:**<br>• Kuwa kielelezo kwa wenzake katika usomaji na uigizaji wa michezo. |

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| **Viwango** / **Vigezo** | **Kuzidisha Matarajio** | **Kufikia Matarajio** | **Kukaribia Matarajio** | **Mbali na Matarajio** |
|---|---|---|---|---|
| Kutambua mchezo wa kuigiza, wahusika na maelekezo, kuusoma kwa kuzingatia ujumbe na kujibu maswali kwa usahihi | Mwanafunzi anatambua mchezo wa kuigiza, wahusika na maelekezo, anausoma kwa kuzingatia ujumbe na kujibu maswali kwa usahihi na urahisi | Mwanafunzi anatambua mchezo wa kuigiza, wahusika na maelekezo, anausoma kwa kuzingatia ujumbe na kujibu maswali kwa usahihi | Mwanafunzi anatambua mchezo wa kuigiza, wahusika na maelekezo, anausoma kwa kuzingatia ujumbe na kujibu baadhi ya maswali kwa usahihi | Mwanafunzi anatambua baadhi ya vipengee katika mchezo wa kuigiza, anasoma sehemu za mchezo huo na kujibu baadhi ya maswali kwa usahihi |

<table>
<tr><th>MADA</th><th>MADA NDOGO</th><th>MATOKEO MAALUMU YANAYOTARAJIWA</th><th>MAPENDEKEZO YA SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI</th><th>SWALI DADISI</th></tr>
<tr><td>8.3 Kuandika</td><td>8.3.1 Kuandika insha:<br>Insha za masimulizi<br>(Vipindi 2)</td><td>Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze,<br>a) kueleza sifa za insha ya masimuizi ili kuibainisha<br>b) kuandika insha ya masimulizi kwa kufuata kanuni zifaazo<br>c) kuchangamkia utunzi mzuri.</td><td>Mwanafunzi:<br>• atambue insha ya masimulizi kwa kurejelea vielelezo vya insha zilizoandikwa kwenye matini mbalimbali au tarakilishi<br>• ashiriki na wenzake kujadili mada ya insha na muundo wa insha ya masimulizi<br>• aandike insha isiyopungua maneno 150, inayosimulia tukio linalohusiana na ndege wa porini kwa kuzingatia anwani, mpangilio mzuri wa mawazo, hati safi, tahajia, kanuni za kisarufi, uakifishaji mwafaka na kwa lugha ya kiubunifu<br>• aandike insha ya masimulizi katika vifaa vya kidijitali na kuisambaza kwa wenzake na mwalimu ili kuisoma na kuitathmini<br>• awasomee wenzake insha aliyoandika ili waitathmini na kumwelekeza .</td><td>1. Ni mambo gani unayozingatia ili kuandika insha ya masimulizi ya kuvutia?</td></tr>
<tr><td colspan="5">Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:<br>• Mawasiliano na ushirikiano – Huu unakuzwa wanafunzi wanaposhiriki katika mijadala na kazi za vikundi<br>• Ujuzi wa kidijitali – Huu unakuzwa wakati vifaa vya kiteknolojia vinapotumiwa kuandika insha mtandaoni na kurejelea kielelezo cha insha ya masimulizi<br>• Ubunifu – Huu unajengeka mwanafunzi anapoandika insha ya masimulizi</td></tr>
<tr><td colspan="3">Uhusiano na masuala mtambuko:<br>• Uraia kutokana na kufanya kazi pamoja.</td><td colspan="2">Uhusiano na Maadili:<br>• Heshima na adabu hasa katika shughuli za vikundi</td></tr>
<tr><td colspan="3">Uhusiano na masomo mengine:<br>• English na Indigeneous Language – masomo haya hufunza uandishi kama mojawapo ya stadi za lugha.</td><td colspan="2">Mapendekezo ya shughuli za huduma za kijamii zinazochangia ujifunzaji:<br>• Mwanafunzi awahamasishe wenzake shuleni na nyumbani kuhusu umuhimu wa uandishi bora katika mawasiliano.</td></tr>
</table>

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kuandika insha ya masimulizi kwa kuzingatia kanuni za lugha, mpangilio mzuri wa mawazo na lugha ya kiubunifu. | Mwanafunzi anaandika insha ya masimulizi kwa kuzingatia kanuni za lugha, mpangilio mzuri wa mawazo na kwa ubunifu wa hali ya juu. | Mwanafunzi anaandika insha ya masimulizi kwa kuzingatia kanuni za lugha, mpangilio mzuri wa mawazo na lugha ya kiubunifu. | Mwanafunzi anaandika insha ya masimulizi kwa kuzingatia baadhi ya kanuni za lugha | Mwanafunzi anajaribu kuandika insha ya masimulizi |

<table>
<tr><th>MADA</th><th>MADA NDOGO</th><th>MATOKEO MAALUM YANAYOTARAJIWA</th><th>MAPENDEKEZO Y SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI</th><th>SWALI DADISI</th></tr>
<tr><td>8.4 Sarufi</td><td>8.4.1 Mnyambuliko wa Vitenzi:<br>Kauli za kutendewa, kutendeka na kutendana<br><br>(Vipindi 3)</td><td>Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua vitenzi katika hali ya kutendewa, kutendeka na kutendana katika matini<br>b) kutumia vitenzi katika hali za kutendewa, kutendeka na kutendana ipasavyo anapowasiliana<br>c) kuchangamkia matumizi ya vitenzi katika hali ya kutendewa, kutendeka na kutendana katika mawasiliano.</td><td>Mwanafunzi:<br>• atambue vitenzi katika hali za kutendewa, kutendeka na kutendana katika chati, jedwali, kapu la maneno, mti maneno, ubao na vyombo vya kidijitali<br>• anyambue vitenzi katika hali lengwa akiwa peke yake, wakiwa wawiliwawili au katika vikundi<br>• atumie vitenzi katika hali lengwa kwenye sentensi<br>• ashirikiane na wenzake kujaza mapengo katika jedwali la mnyambuliko we vitenzi kwenye daftari au kwa kutumia tarakilishi<br>• aandike sentensi upya kwa kutumia vitenzi katika hali mbalimbali.</td><td>1. Je, vitenzi vinaweza kubadilika vipi mwishoni ili kuleta maana mbalimbali?</td></tr>
<tr><td colspan="5">Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa<br>• Mawasiliano na ushirikiano- kufanya kazi wakiwa wawiliwawili na katika vikundi<br>• Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo - Mwanafunzi ananyambua vitenzi katika hali mbalimbali<br>• Kujiamini- wanapotoa majibu na kushiriki katika shughuli mbalimbali</td></tr>
<tr><td colspan="3">Uhusiano na Masuala Mtambuko<br>• Umoja wa kijamii: kufanya kazi pamoja<br>• Sentensi zinazotungwa zisingatie masuala mbalimbali ya mtambuko</td><td colspan="2">Uhusiano na Maadili<br>• Ushirikiano – wanafunzi wanaposhirikiana katika kazi za vikundi</td></tr>
<tr><td colspan="3">Uhusiano na Masomo Mengine<br>• English na Indigenous Languages hufunza mnyambuliko wa vitenzi</td><td colspan="2">Mapendekezo ya shughuli za huduma za Kijamii zinazochangia ujifunzaji:<br>• Mwanafunzi awe kielelezo cha matumizi ya lugha ifaavyo katika mawasiliano.</td></tr>
</table>

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kutambua vitenzi katika hali ya kutendewa, kutendeka na kutendana, kuvibadilisha katika hali hizi na kuvitumia katika sentensi ifaavyo | Mwanafunzi anatambua vitenzi katika hali ya kutendewa, kutendeka na kutendana, anavibadilisha katika hali hizi na kuvitumia katika sentensi ifaavyo na kwa urahisi | Mwanafunzi anatambua vitenzi katika hali ya kutendewa, kutendeka na kutendana, anavibadilisha katika hali hizi na kuvitumia katika sentensi ifaavyo. | Mwanafunzi anatambua baadhi ya vitenzi katika hali kutendewa, kutendeka na kutendana ambavyo anavibadilisha katika hali hizi na kuvitumia katika sentensi ifaavyo. | Mwanafunzi anatambua baadhi ya vitenzi katika hali ya kutendewa, kutendeka na kutendana ambavyo anabadilisha baadhi yavyo katika hali hizi na kuvitumia katika sentensi. |

<table>
<tr><th colspan="5">9.0 MAGONJWA</th></tr>
<tr><th>MADA</th><th>MADA NDOGO</th><th>MATOKEO MAALUM YANAYOTARAJIWA</th><th>MAPENDEKEZO YA SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI</th><th>SWALI DADISI</th></tr>
<tr><td>9.1 Kusikiliza na Kuzungumza</td><td>9.1.1 Mazungumzo ya Kimuktadha:<br>Mazungumzo katika miktadha rasmi.<br>(Vipindi 2)</td><td>Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua miktadha rasmi kunakotumiwa lugha rasmi ili kukuza mawasiliano<br>b) kutumia lugha katika miktadha rasmi ili kufanikisha mawasiliano<br>c) kuchangamkia matumizi ya lugha katika miktadha rasmi.</td><td>Mwanafunzi:<br>• atambue miktadha rasmi kunakotumiwa lugha rasmi (k.v ofisini, hospitalini, mahakamani na bungeni)<br>• asikilize mazungumzo rasmi kwa kutazama maigizo kwenye vyombo vya kidijitali kama vile video, rununu, runinga, tarakilishi n.k<br>• ashiriki katika maigizo ya mazungumzo ya miktadha rasmi akishirikiana na wenzake<br>• ashiriki katika mazungumzo rasmi nje ya darasa k.m. akiwa kwenye gwaride na majilisini<br>• atambue nidhamu ya lugha inayozingatiwa katika mazingira rasmi k.m lugha ya heshima na adabu anapowasiliana.</td><td>1. Ni wapi katika shughuli zetu za kila siku tunaitumia lugha rasmi?</td></tr>
<tr><td colspan="5">Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa<br>• Mawasiliano na ushirikiano- kupitia kwa kushiriki katika kazi ya vikundi<br>• Ubunifu – unadhihirika anaposhiriki katika mazungumzo<br>• Ujuzi wa kidijitali – unakuzwa mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kusikiliza na kutazama mazungumzo</td></tr>
<tr><td colspan="3">Uhusiano na Masuala Mtambuko<br>• Mazungumzo yahusishe masuala mtambuko k.v. magonjwa hatari, matumizi ya dawa za kulevya, mazoezi ya viungo vya mwili n.k</td><td colspan="2">Uhusiano na Maadili<br>• Uwajibikaji katika kutunza vifaa vya kidijitali<br>• Heshima na ushirikiano katika uigizaji na kushiriki katika mazungumzo</td></tr>
<tr><td colspan="3">Uhusiano na Masomo Mengine<br>• English na Indigenous Languages – Masomo haya yana mada kuhusu kusikiliza na kuzungumza</td><td colspan="2">Mapendekezo ya shughuli za huduma za Kijamii zinazochangia ujifunzaji:<br>• Mwanafunzi awe kielelezo cha wengine katika kutumia lugha kwa heshima na ufasaha katika miktadha isiyo rasmi.</td></tr>
</table>

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kutambua lugha katika miktadha rasmi na kuitumia kwa ufasaha kwa kuzingatia hadhi ili kuleta utangamano. | Mwanafunzi anatambua lugha katika miktadha rasmi na kuitumia kwa ufasaha na urahisi kwa kuzingatia hadhi ili kuleta utangamano. | Mwanafunzi anatambua lugha katika miktadha rasmi na kuitumia kwa ufasaha kwa kuzingatia hadhi ili kuleta utangamano. | Mwanafunzi anatambua lugha katika baadhi ya miktadha rasmi na kuitumia kwa kuzingatia hadhi ili kuleta utangamano. | Mwanafunzi anatumia lugha bila kuzingatia miktadha rasmi. |

<table>
<tr><th>MADA</th><th>MADA NDOGO</th><th>MATOKEO MAALUM YANAYOTARAJIWA</th><th>MAPENDEKEZO YA SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI</th><th>MASWALI DADISI</th></tr>
<tr><td>9.2 Kusoma</td><td>9.2.1 Kusoma kwa Mapana: Matini<br><br>(Vipindi 3)</td><td>Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua matini ya aina mbalimbali ya kusoma na kuchagua yanayomvutia<br>b) kusoma matini aliyochagua ili kufaidika na ujumbe na lugha iliyotumiwa<br>c) kufurahia usomaji wa aina mbalimbali za matini ili kupanua mawazo yake.</td><td>Mwanafunzi:<br>• achague matini (k.v. vitabu, majarida, magazeti) yanayomvutia maktabani na mtandaoni<br>• asome matini aliyochagua ili kufaidi ujumbe uliomo<br>• awatolee wenzake muhtasari wa kile alichosoma kwenye matini ili kupashana ujumbe na kuchocheana kusoma zaidi kwa ajili ya kujifurahisha<br>• ajadiliane na wenzake matini ambayo wamesoma kwa kuzingatia ukuzaji wa msamiati.</td><td>1) Ni habari zipi unazopenda kusoma kwenye matini ?<br>2) Unachagua matini hayo kwa nini ?</td></tr>
<tr><td colspan="5">Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa<br>• Mawasiliano na ushirikiano - mwanafunzi anaposimulia na kujadiliana na wenzake<br>• Ujuzi wa kidijitali – Mwanafunzi anapotumia tarakilishi na mtandao kupata matini ya kusoma<br>• Hamu ya ujifunzaji – mwanafunzi anapojichagulia matini na kuyasoma</td></tr>
<tr><td colspan="3">Uhusiano na Masuala Mtambuko<br>• Matini anayochagua mwanafunzi yajumuishe masuala mtambuko mbalimbali</td><td colspan="2">Uhusiano na Maadili<br>• Uwajibikaji – mwanafunzi anapotunza matini anayoyasoma<br>• Heshima – mwanafunzi anapojadiliana na wenzake kuhusu alichosoma</td></tr>
<tr><td colspan="3">Uhusiano na Masomo Mengine<br>• English – somo hili linashughulikia mada ya kusoma kwa mapana</td><td colspan="2">Mapendekezo ya shughuli za huduma za Kijamii zinazochangia ujifunzaji:<br>• Kuwa kielelezo cha utamaduni wa kusoma shuleni na nyumbani<br>• Maarifa anayopata mwanafunzi kutokana na usomaji wake anautumia shuleni na nyumbani kuifaidi jamii.</td></tr>
</table>

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Utamaduni mzuri wa kusoma matini za aina mbalimbali shuleni na nje ya shule na kusimulia kwa ufasaha alichokisoma | Mwanafunzi ana utamaduni mzuri wa kusoma matini za aina mbalimbali shuleni na nje ya shule na anapenda kusimulia kwa ufasaha alichokisoma | Mwanafunzi ana utamaduni mzuri wa kusoma matini za aina mbalimbali shuleni na nje ya shule na kusimulia alichokisoma | Mwanafunzi ana utamaduni wa kusoma baadhi ya sampuli za matini shuleni na kuzisimulia | Mwanafunzi anasoma baadhi ya matini shule |

<table>
<tr><th>MADA</th><th>MADA NDOGO</th><th>MATOKEO MAALUMU YANAYOTARAJIWA</th><th>MAPENDEKEZO YA SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI</th><th>SWALI DADISI</th></tr>
<tr><td>9.3 Kuandika</td><td>9.3.1 Insha za Maelezo<br>(Vipindi 2)</td><td>Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze,<br>a) kutambua vifungu vya maelezo vilivyoandikwa kwenye matini mbalimbali<br>b) kuandika insha ya maelezo kwa kufuata mtindo na muundo ufaao<br>c) kuchangamkia utunzi mzuri wenye ujumbe mahususi.</td><td>Mwanafunzi:<br>• atambue vifungu vya maelezo vilivyoandikwa kwenye matini mbalimbali au tarakilishi<br>• ashiriki na wenzake kujadili mada ya insha na muundo wa insha ya maelezo<br>• aandike insha ya maelezo isiyopungua maneno 150 kwa kuzingatia msamiati unaohusu suala lengwa na kwa kuzingatia vigezo kama vile: ujumbe, tahajia, anwani, muundo, mtindo, mapambo ya lugha k.v methali, nahau, tashbihi, istiari n.k. alizojifunza awali<br>• aandike insha ya maelezo mtandaoni na kuisambaza kwa wenzake na mwalimu ili kuisoma na kuitathmini.<br>• awasomee wenzake insha aliyoandika ili kuisoma na kuitathmini.</td><td>1. Je, ni mada gani inayoweza kuandikiwa insha za maelezo?</td></tr>
<tr><td colspan="5">Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:<br>• Mawasiliano na ushirikiano – Huu unakuzwa wanafunzi wanaposhiriki katika mijadala na kazi za vikundi<br>• Ujuzi wa kidijitali – Huu unakuzwa wakati vifaa vya kiteknolojia vinapotumiwa kuandika insha mtandaoni na kurejelea kielelezo cha insha ya maelezo<br>• Ubunifu – Huu unajengeka mwanafunzi anapoandika insha ya maelezo</td></tr>
<tr><td colspan="3">Uhusiano na masuala mtambuko:<br>• Uraia kutokana na kufanya kazi pamoja.</td><td colspan="2">Uhusiano na Maadili:<br>• Heshima na adabu hasa katika shughuli za vikundi</td></tr>
<tr><td colspan="3">Uhusiano na masomo mengine:<br>• English na Indigeneous Languages – masomo haya yanashughulikia mada kuandika</td><td colspan="2">Mapendekezo ya shughuli za huduma za kijamii zinazochangia ujifunzaji:<br>• Kuwahamasisha wenzake shuleni na nyumbani kuhusu umuhimu wa uandishi mzuri katika mawasiliano</td></tr>
</table>

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kuandika insha ya maelezo yenye kujenga picha dhahiri, kuzingatia kanuni za lugha na mpangilio mzuri wa mawazo. | Mwanafunzi anaandika insha ya maelezo yenye kujenga picha dhahiri, kuzingatia kanuni za lugha na mpangilio mzuri wa mawazo kwa urahisi. | Mwanafunzi anandika insha ya maelezo yenye kujenga picha dhahiri, kuzingatia kanuni za lugha na mpangilio mzuri wa mawazo. | Mwanafunzi anandika insha ya maelezo yenye kujenga picha dhahiri, kuzingatia baadhi ya kanuni za lugha na mpangilio mzuri wa mawazo. | Mwanafunzi anaandika insha ya maelezo bila kujenga picha dhahiri ya anachoandikia. |

| MADA | MADA NDOGO | MATOKEO MAALUM YANAYOTARAJIWA | MAPENDEKEZO YA SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI | SWALI DADISI |
|---|---|---|---|---|
| **9.4 Sarufi** | **9.4.1 Vinyume: Vinyume vya Vitenzi** (Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua vinyume vya vitenzi katika matini<br>b) kuunda sentensi kwa kutumia vinyume vya vitenzi<br>c) kuchangamkia matumizi ya vinyume vya vitenzi katika mawasiliano ya kila siku. | Mwanafunzi<br>• atambue vinyume vya vitenzi *(k.m. Simama-keti, cheka-lia, enda- rudi, chimba-chimbua n.k)* katika chati, kadi za maneno, kapu la maneno, mti maneno au vifaa vya kidijitali<br>• ashirikiane na wenzake kutafuta vinyume vya vitenzi kwa kurejelea orodha ya vitenzi aliyopewa<br>• atalii mazingira yake na kuunda orodha ya vinyume vya vitenzi anavyovitambua.<br>• atunge sentensi kwa kutumia vinyume vya vitenzi kwa kuzingatia upatanisho wa kisarufi<br>• aandike upya sentensi kwa kutumia vinyume vya vitenzi. | 1. Je, ni vitenzi gani unavyoweza kutambua vinyume vyake? |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**
- Mawasiliano na ushirikiano- kupitia kwa kushiriki kazi ya vikundi
- Ubunifu-unadhihirika anapotunga sentensi
- Ujuzi wa kidijitali – unakuzwa mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali

| Uhusiano na Masuala Mtambuko | Uhusiano na Maadili |
|---|---|
| • Elimu endelevu – mwanafunzi anapanua mawazo kuhusu mazingira yake anapotambua vinyume vya vitenzi kutokana na vitendo anavyovishuhudia katika jamii yake. | • Uwajibikaji katika kutunza vifaa vya kidijitali<br>• Heshima na ushirikiano katika shughuli za vikundi |
| **Uhusiano na Masomo Mengine** | **Mapendekezo ya shughuli za huduma za Kijamii zinazochangia ujifunzaji**: |
| English – somo hili hushughulikia mada ya vinyume | • Mwanafunzi awe kielelezo kwa wengine katika lugha kwa kuzingatia kanuni zake |

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kutambua vinyume vya vitenzi mbalimbali na kuvitumia katika sentensi ipasavyo kwa urahisi | Mwanafunzi anatambua vinyume vya vitenzi mbalimbali na kuvitumia katika sentensi ipasavyo kwa urahisi | Mwanafunzi anatambua vinyume vya vitenzi mbalimbali na kuvitumia katika sentensi ipasavyo | Mwanafunzi anatambua baadhi ya vinyume vya vitenzi na kuvitumia katika sentensi ipasavyo | Mwanafunzi anatambua baadhi ya vinyume vya vitenzi na kutumia baadhi ya vinyume hivyo katika sentensi |

<table>
<tr><th colspan="5">10.0 KUDHIBITI ITIKADI ZA KIDINI NA ZA KIJAMII</th></tr>
<tr><th>MADA</th><th>MADA NDOGO</th><th>MATOKEO MAALUM YANAYOTARAJIWA</th><th>MAPENDEKEZO YA SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI</th><th>SWALI DADISI</th></tr>
<tr><td>10.1 Kusikiliza na Kuzungumza</td><td>10.1.1 Tashbihi:<br>Tashbihi za tabia<br>(Vipindi 2)</td><td>Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua tashbihi za tabia katika matini<br>b) kutumia tashbihi za tabia kwa usahihi katika sentensi<br>c) kufurahia matumizi ya tashbihi za tabia katika mawasiliano ya kila siku.</td><td>Mwanafunzi:<br>• atambue tashbihi za tabia (k.v. mjanja kama sungura, mlafi kama fisi, mwenye maneno mengi kama kasuku, -eusi kama makaa) katika vitabu, matini, chati na vyombo vya kidijitali.<br>• aeleze maana ya tashbihi mbalimbali za tabia kwa kutoa mifano<br>• akamilishe tashbihi mbalimbali za tabia akiwa peke yake au kwa kushirikiana na wenzake darasani<br>• ajaze mapengo katika sentensi kwa kutumia tashbihi mbalimbali za tabia<br>• atumie tashbihi za tabia katika sentensi akiwa peke yake au katika vikundi.</td><td>1. Ni tashbihi zipi hutumiwa kuelezea tabia?</td></tr>
<tr><td colspan="5">Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa<br>• Mawasiliano na ushirikiano - mwanafunzi anashiriki kazi ya vikundi<br>• Hamu ya kujifunza - kutokana na kutambua tashbihi za tabia katika matini<br>• Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali katika mada</td></tr>
<tr><td colspan="3">Uhusiano na Masuala Mtambuko<br>• Stadi za maisha hasa katika kuimarisha mawasiliano</td><td colspan="2">Uhusiano na Maadili<br>Heshima na adabu – anaheshimu maoni ya wenzake atika vikundi</td></tr>
<tr><td colspan="3">Uhusiano na Masomo Mengine<br>• English na Indigenous Languages – masomo haya hufunza tashbihi</td><td colspan="2">Mapendekezo ya shughuli za huduma za Kijamii zinazochangia ujifunzaji:<br>Kuwa kielelezo cha kutumia lugha kwa ufasaha shuleni na nyumbani.</td></tr>
</table>

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango<br>Vigezo | **Kuzidisha Matarajio** | **Kufikia Matarajio** | **Kukaribia Matarajio** | **Mbali na Matarajio** |
|---|---|---|---|---|
| Kutambua tashbihi za tabia na kuzitumia kwa usahihi katika sentensi. | Mwanafunzi anatambua tashbihi za tabia na kuzitumia kwa usahihi na urahisi katika sentensi. | Mwanafunzi anatambua tashbihi za tabia na kuzitumia kwa usahihi katika sentensi. | Mwanafunzi anatambua baadhi ya tashbihi za tabia na kuzitumia kwa usahihi katika sentensi. | Mwanafunzi anatambua baadhi ya tashbihi za tabia na kutumia baadhi ya zile alizotambua kwa usahihi katika sentensi. |

| MADA | MADA NDOGO | MATOKEO MAALUM YANAYOTARAJIWA | MAPENDEKEZO YA SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI | MASWALI DADISI |
|---|---|---|---|---|
| **10.2 Kusoma** | **10.2.1 Kusoma Mapana:** Matini ya Kidijitali<br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua na kuzingatia hatua za kiusalama katika matumizi ya vifaa vya kidijitali<br>b) kutambua na kufungua faili iliyo na kifungu cha kusoma ili kuimarisha umilisi wake wa kutumia tarakilishi<br>c) kusakura kwenye tovuti salama ili kupata vifungu vya kusoma<br>d) kutumia vyombo vya kidijitali kwa urahisi kupata matini zinazolengwa<br>e) kuchangamkia matumizi ya vifaa vya kidijitali katika kutafuta na kusoma ujumbe ili kuimarisha maarifa yake. | Mwanafunzi:<br>• atambue na kuzingatia hatua za kiusalama kutoka kwenye chati au kwenye tarakilishi na mitandao.<br>• atambue jina la faili lengwa kwenye tarakilishi na kufanya mazoezi ya kufungua na kufunga<br>• atambue mitandao salama yenye matini inayoafiki kiwango na mahitaji yake<br>• atambue umuhimu wa kutoa habari kwa mwalimu, mzazi au mlezi wake endapo atapata ujumbe kutoka kwa watu asiowajua mtandaoni na kutowasiliana nao<br>• atafute maana za maneno mapya kwenye kamusi mtandaoni<br>• asimulie habari kuhusu matini aliyosoma kwa wenzake. | 1. Unapenda kusoma habari kuhusu nini mtandaoni?<br>2. Unakumbuka habari gani uliyoisoma mtandaoni?<br>3. Ni hatua gani za kiusalama unazozingatia unapotafuta habari mtandaoni? |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Ujuzi wa kidijitali – unakuzwa mwanafunzi anapotumia vifaa vya kiteknolojia katika kutafuta, kusakura na kusoma matini.
- Hamu ya kujifunza – inakuzwa mwanafunzi anapopata hamu ya kutafuta matini za kusoma kwenye tarakilishi na mitandaoni

| **Uhusiano na Masuala Mtambuko** | **Uhusiano na Maadili** |
|---|---|
| • Stadi za maisha – mwanafunzi anapozingatia usalama wa mtandaoni | • Uwajibikaji – katika utunzaji wa vifaa vya kidijitali na kuzingatia mitandao salama |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>• Masomo yote kwa vile yanatakiwa kuzingatia ujuzi wa kidijitali | **Mapendekezo ya shughuli za huduma za kijamii zinazochangia ujifunzaji**:<br>• Kuwahamasisha wenzake shuleni na nyumbani kuhusu usalama mitandaoni na manufaa ya ujuzi wa kidijitali katika kuimarisha usomaji na kupata maarifa yanayohusu nyanja mbalimbali |

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| **Viwango** / **Vigezo** | **Kuzidisha Matarajio** | **Kufikia Matarajio** | **Kukaribia Matarajio** | **Mbali na Matarajio** |
|---|---|---|---|---|
| Kutambua na kuzingatia hatua za kiusalama mtandaoni. | Mwanafunzi anatambua na kuzingatia hatua za kiusalama mtandaoni kwa urahisi | Mwanafunzi anatambua na kuzingatia hatua za kiusalama mtandaoni | Mwanafunzi anatambua na kuzingatia baadhi ya hatua za kiusalama mtandaoni. | Mwanafunzi anatatizika kutambua hatua za kiusalama mtandaoni. |
| Kutambua na kufungua faili iliyo na kifungu cha kusoma kwa urahisi | Anatambua na kufungua faili iliyo na kifungu cha kusoma kwa urahisi na wepesi | Anatambua na kufungua faili iliyo na kifungu cha kusoma kwa urahisi | Anatambua na kufungua faili iliyo na kifungu cha kusoma | Ana changamoto kutambua na kufungua faili iliyo na kifungu cha kusoma |
| Kusakura kwenye tovuti salama ili kupata vifungu vya kusoma | Anasakura kwenye tovuti salama kwa wepesi ili kupata vifungu vya kusoma | Anasakura kwenye tovuti salama ili kupata vifungu vya kusoma | Anasakura kwenye tovuti salama ili kupata baadhi ya vifungu vya kusoma | Anatatizika kusakura kwenye tovuti salama ili kupata vifungu vya kusoma |
| Kutumia vyombo vya kidijitali kwa urahisi kupata matini | Anatumia vyombo vya kidijitali kwa urahisi na wepesi kupata matini | Anatumia vyombo vya kidijitali kwa urahisi kupata matini | Anatumia baadhi ya vyombo vya kidijitali kupata matini | Ana shida kutumia vyombo vya kidijitali kupata matini |

| MADA | MADA NDOGO | MATOKEO MAALUMU YANAYOTARAJIWA | MAPENDEKEZO YA SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI | SWALI DADISI |
|---|---|---|---|---|
| **10.2 Kuandika** | **10.2.1 Aina za Insha:** Insha ya masimulizi (Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua insha ya masimulizi kwa kuzingatia muundo<br>b) kuandika insha ya masimulizi kwa kufuata kanuni zifaazo<br>c) kuchangamkia utunzi mzuri. | Mwanafunzi:<br>• atambue insha ya masimulizi kwa kurejelea vielelezo vya insha zilizoandikwa kwenye matini mbalimbali au tarakilishi<br>• ashiriki na wenzake kujadili mada ya insha na muundo wa insha ya masimulizi<br>• aandike insha ya masimulizi (*k.v. kuhusu itikadi za kidini na za kijamii, sherehe, hadithi, ndoto, ndoa za lazima n.k*) isiyopungua maneno 150 akizingatia aina mbalimbali za maneno, mnyambuliko wa vitenzi, na nyakati ili kejenga picha dhahiri ya anachokiandikia daftarini. Pia azingatie mada, mpangilio mzuri wa mawazo, hati safi, tahajia, kanuni za kisarufi, uakifishaji mwafaka, lugha ya kiubunifu<br>• aandike insha ya masimulizi katika vifaa vya kidijitali na kuisambaza kwa wenzake na mwalimu ili kuisoma na kuitathmini<br>• awasomee wenzake insha aliyoandika ili waitathmini na kumwelekeza. | 1. Unawezaje kupata kwa haraka hoja za kusimulia katika insha? |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa**:

- Mawasiliano na ushirikiano – Huu unakuzwa wanafunzi wanaposhiriki katika mijadala na kazi za vikundi
- Ujuzi wa kidijitali – Huu unakuzwa wakati vifaa vya kiteknolojia vinapotumiwa kuandika insha mtandaoni na kurejelea kielelezo cha insha ya mawasiliano
- Ubunifu – Huu unajengeka mwanafunzi anapoandika insha ya masimulizi
- Hamu ya ujifunzaji – Huu unakuzwa mwanafunzi anapoyatafakari maswali dadisi na anapoimarisha ujuzi wake wa kutumia tarakilishi

| **Uhusiano na masuala mtambuko**: | **Uhusiano na Maadili:** |
|---|---|
| • Uraia kutokana na kufanya kazi pamoja. | • Heshima na adabu hasa katika shughuli za vikundi |
| **Uhusiano na masomo mengine**: | **Mapendekezo ya shughuli za huduma za kijamii zinazochangia ujifunzaji**: |
| • English na Indigeneous Language – masomo haya yanafunza uandishi kama mojawapo ya stadi za lugha. | • Kuwahamasisha wenzake shuleni na nyumbani kuhusu umuhimu wa uandishi bora katika mawasiliano. |

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kuandika insha ya masimulizi kwa ubunifu kwa kuzingatia kanuni za lugha, mpangilio mzuri wa mawazo na kwa ufasaha na urefu ufaao. | Mwanafunzi anaandika insha ya masimulizi yenye urefu ufaao kwa kuzingatia kanuni za lugha, mpangilio mzuri wa mawazo na kwa ubunifu wa kiwango cha juu. | Mwanafunzi anaandika insha ya masimulizi yenye urefu ufaao kwa kuzingatia kanuni za lugha, mpangilio mzuri wa mawazo na kwa ubunifu. | Mwanafunzi anaandika insha ya masimulizi kwa kuzingatia kanuni za lugha, mpangilio mzuri wa mawazo. | Mwanafunzi anaandika insha ya masimulizi kwa kuzingatia baadhi ya kanuni za lugha. |

| MADA | MADA NDOGO | MATOKEO MAALUM YANAYOTARAJIWA | MAPENDEKEZO YA SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI | MASWALI DADISI |
|---|---|---|---|---|
| **10.4 Sarufi** | **10.4.1 Nyakati na Hali**<br>**-**Hali ya Mazoea<br>-Hali Timilifu<br>(Vipindi 3) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua viambishi vya hali ya mazoea na hali timilifu kwenye kitenzi<br>b) kutambua vitenzi katika hali ya mazoea na hali timilifu kwenye matini<br>c) kutumia vitenzi vya hali ya mazoea na timilifu katika sentensi ili kuimarisha mawasiliano<br>d) kufurahia matumizi ya hali ya mazoea na timilifu katika mawasiliano. | Mwanafunzi:<br>• atambue viambishi vya hali ya mazoea (hu) na hali timilifu (me) kwenye vitenzi katika chati, ubao au kwa kutumia vifaa vya kidijitali<br>• atambue vitenzi katika hali ya mazoea (hu) na hali timilifu (me) kwenye sentensi, chati, ubao au kwa kutumia vifaa vya kidijitali<br>• ashiriki na wenzake katika mazoezi ya kutumia hali ya mazoea (hu) na hali timilifu (me) katika sentensi na kuziandika daftarini au kupiga chapa kwenye tarakilishi/kipakatalishi<br>• ashirikiane na wenzake katika vikundi kubadilisha sentensi kutoka hali moja hadi nyingine<br>• atunge sentensi katika hali ya mazoea na hali timilifu kwenye blogi ili wenzake waweze kuisoma na kutathmini usahihi wake. | 1) Je, wewe hufanya shughuli gani kila siku? |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anashiriki katika shughuli za vikundi darasani na mtandaoni
- Ubunifu – mwanafunzi anapotunga sentensi
- Hamu ya ujifunzaji – mwanafunzi anapoendelea kutunga sentensi katika hali ya mazoea na hali timilifu
- Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anapotumia kipakatalishi au tarakilishi kutunga sentensi na vile vile kuzisambaza mtandaoni
- Hamu ya kuendelea kujifunza hasa anapotunga sentensi sahihi

| **Uhusiano na Masuala Mtambuko** | **Uhusiano na Maadili** |
|---|---|
| • Stadi za Maisha: kujitambua na kujithamini anapotunga sentensi na kuzitumia kujieleza | • Heshima – anapojifunza kuthamini maoni ya wengine |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>• English – somo hili lina mada kuhusu sarufi | **Mapendekezo ya shughuli za huduma za Kijamii zinazochangia ujifunzaji**:<br>• Mwanafunzi anapokuwa kielelelzo kwa wenzake shuleni na nyumbani katika kutumia Kiswahili kwa kuzingatia kanuni za kisarufi. |

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kutambua viambishi vya hali ya mazoea na hali timilifu kwenye kitenzi | Mwanafunzi anatambua viambishi vya hali ya mazoea na hali timilifu kwenye kitenzi kwa urahisi. | Mwanafunzi anatambua viambishi vya hali ya mazoea na hali timilifu kwenye kitenzi. | Mwanafunzi anatambua baadhi ya viambishi vya hali ya mazoea na hali timilifu kwenye kitenzi. | Mwanafunzi ana changamoto kutambua viambishi vya hali ya mazoea na hali timilifu kwenye kitenzi. |
| Kutambua vitenzi katika hali ya mazoea na hali timilifu kwenye matini | Anatambua vitenzi katika hali ya mazoea na hali timilifu kwenye matini kwa wepesi. | Anatambua vitenzi katika hali ya mazoea na hali timilifu kwenye matini | Anatambua baadhi ya vitenzi katika hali ya mazoea na hali timilifu kwenye matini | Anatatizika kutambua vitenzi katika hali ya mazoea na hali timilifu kwenye matini |
| Kutumia vitenzi vya hali ya mazoea na timilifu katika sentensi kwa usahihi. | Anatumia vitenzi vya hali ya mazoea na timilifu katika sentensi kwa usahihi na wepesi | Anatumia vitenzi vya hali ya mazoea na timilifu katika sentensi kwa usahihi. | Anatumia baadhi ya vitenzi vya hali ya mazoea na timilifu katika sentensi kwa usahihi. | Anatatizika kutumia vitenzi vya hali ya mazoea na timilifu katika sentensi. |

| 11.0 UWEKEZAJI | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **MADA** | **MADA NDOGO** | **MATOKEO MAALUM YANAYOTARAJIWA** | **MAPENDEKEZO YA SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI** | **SWALI DADISI** |
| **11.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **11.1.1 Kutoa Masimulizi** (Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kusimulia tungo mbele ya wenzake kwa kuzingatia mada, ubunifu na usanifu wa lugha<br>b) kutumia ishara zifaazo kuimarisha masimulizi yake<br>c) kuchangamkia masimulizi katika mazingira mbalimbali | Mwanafunzi:<br>• asikilize masimulizi yakitolewa na mgeni mwalikwa, mwalimu, mwanafunzi mwenzake au kutokana na vifaa vya kidijitali.<br>• abuni masimulizi yanayohusiana na mada husika kwa kutazama picha, michoro au kujadiliana na wenzake<br>• kutoa masimulizi kuhusu mada (*k.v. Jinsi ya kuwekeza na Faida za uwekezaji)*<br>• atumie ishara za mwili zifaazo k.v ishara za uso, za mikono na mabega kuimarisha masimulizi yake<br>• ajadiliane na wenzake kuhusu ubora wa masimulizi aliyosikiliza. | 1.Je, ni nini unachozingatia katika kutoa masimulizi? |

| | |
|---|---|
| **Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**<br>• Mawasiliano na ushirikiano - kujadili kwenye vikundi<br>• Ubunifu - mwanafunzi kutunga na kusimulia visa mbalimbali<br>• Kujiamini - mwanafunzi kusimulia visa mbele ya wenzake | |
| **Uhusiano na Masuala Mtambuko**<br>• Ujuzi wa matumizi ya fedha anaposimulia kuhusu uwekezaji | **Uhusiano na Maadili**<br>• Uwajibikaji – kukamilisha shughuli mbalimbali |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>• English – kuhusu ufasaha wa kusema kwa ubunifu | **Mapendekezo ya shughuli za huduma za Kijamii zinazochangia ujifunzaji:**<br>• Mwanafunzi kutoa masimulizi kuhusu uwekezaji kwa wenzake katika miktadha mbalimbali |

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kubuni na kusimulia tungo kwa kuzingatia ujumbe, ufasaha wa lugha na ishara zafaazo. | Mwanafunzi anabuni na kusimulia tungo kwa kuzingatia ujumbe, ufasaha wa lugha na ishara zifaazo kwa urahisi | Mwanafunzi anabuni na kusimulia tungo kwa kuzingatia ujumbe, ufasaha wa lugha na ishara zafaazo | Mwanafunzi anabuni na kusimulia tungo kwa kuzingatia ujumbe. | Mwanafunzi anabuni na kusimulia tungo bila kuzingatia mpangilio mzuri wa hoja. |

| MADA | MADA NDOGO | MATOKEO MAALUM YANAYOTARAJIWA | MAPENDEKEZO YA SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI | MASWALI DADISI |
|---|---|---|---|---|
| **11.2 Kusoma** | **11.2.1 Kusoma kwa Ufahamu:**<br>Kifungu cha hadithi (Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua msamiati wa mada lengwa uliotumika katika kifungu<br>b) kueleza maana za msamiati wa mada lengwa uliotumika katika kifungu<br>c) kutumia msamiati ulio katika kifungu kwa usahihi katika sentensi<br>d) kusoma kifungu kwa ufasaha ili kupata ujumbe<br>e) kuonyesha ufahamu wa kifungu kwa kutoa muhtasari na kujibu maswali<br>f) kuchangamkia usomaji wa kifungu ili kujenga maarifa ya ufahamu | Mwanafunzi:<br>• atambue msamiati wa suala lengwa (uwekezaji) (*k.v. kuwekeza, faida, hasara, fidia, mtaji, ajira, mkopo, mwanabiashara, deni, mteja, biashara, bidhaa, bajeti, kilimo biashara, benki, vyama vya ushirika, ushuru kutokana na mapato,* n.k akitumia kapu maneno, mti maneno au tarakilishi.<br>• aeleze maana ya msamiati huu kama unavyotumiwa katika jamii wakati wa mawasiliano na shughuli za uwekezaji.<br>• atunge sentensi akitumia msamiati husika, akiwa peke yake, kwenye jozi au kikundi.<br>• atazame chati kwenye tarakilishi au matini inayoonyesha bajeti<br>• ajadili na wenzake matukio kwenye picha zinayoonyesha wafanyibiashara na wateja wao katika shughuli za kibiashara.<br>• asome ufahamu kwa kuzingatia ujumbe akiwa peke yake au kwa sauti akipishana zamu na wenzake<br>• ajibu maswali kutokana na kifungu<br>• atoe muhtasari wa kifungu alichosoma | 1. Je, ni mambo gani yanayokuvutia unaposoma kifungu cha ufahamu?<br>2. Unafanya nini ili kujua maana ya msamiati uliotumiwa katika kifungu? |

**Umilisi wa Kimsingi unaokuzwa**
- Mawasiliano na ushirikiano- anaposoma kifungu au mchezo mfupi kwa sauti na kupishana nafasi na wenzake.
- Kufikiri kwa kina – anapojibu maswali kutokana na kifungu.
- Ubunifu –anaposoma kuhusu uwekezaji na jinsi ya kujikimu kimaisha

**Uhusiano na Masuala Mtambuko**
- Elimu kwa maendeleo endelevu anapojifunza kuhusu elimu ya fedha hususan uwekezaji.
- Stadi za maisha – anapopata maarifa ya kujitegemea anapoandaa bajeti yake.

**Uhusiano na Maadili**
- Heshima – anaposikiliza wengine wakisoma kifungu au mchezo mfupi.
- Uwajibikaji – anapojifunza mambo kuhusu uwekezaji.
- Kujiamini – anapofuatilia mambo yanayotokea katika shughuli za biashara

**Uhusiano na masomo mengine**
- English – somo hili linashughulikia mada ya kusoma vifungu vya ufahamu

**Shughuli za kijamii zinazochangia ujifunzaji**
- Mwanafunzi awahamasishe wenzake katika jamii kuhusu kusoma kwa ufahamu.

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | **Kuzidisha Matarajio** | **Kufikia Matarajio** | **Kukaribia Matarajio** | **Mbali na Matarajio** |
|---|---|---|---|---|
| Kusoma kifungu cha ufahamu, kueleza maana ya msamiati kwa usahihi na kujibu maswali kwa ufasaha | Mwanafunzi anasoma kifungu cha ufahamu kwa wepesi, anaeleza maana ya msamiati kwa usahihi na kujibu maswali ya kifungu kwa ufasaha na urahisi | Mwanafunzi anasoma kifungucha ufahamu, anaeleza maana ya msamiati kwa usahihi na kujibu maswali ya kifungu kwa ufasaha. | Mwanafunzi anasoma kifungu cha ufahamu, kueleza maana ya baadhi ya msamiati kwa usahihi na kujibu baadhi ya maswali ya kifungu. | Mwanafunzi anasoma baadhi ya sehemu za kifungu cha ufahamu, kueleza maana ya baadhi ya msamiati na kujibu maswali machache. |

<table>
<tr><th>MADA</th><th>MADA NDOGO</th><th>MATOKEO MAALUM YANAYOTARAJIWA</th><th>MAPENDEKEZO YA SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI</th><th>SWALI DADISI</th></tr>
<tr><td>11.3 Kuandika</td><td>Kuandika Insha:<br>Baruapepe<br>(Vipindi 2)</td><td>Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua baruapepe kwa kuzingatia muundo wake<br>b) kuandika baruapepe kwa kuzingatia ujumbe, muundo na mtindo<br>c) kuchangamkia uandishi wa baruapepe katika mawasiliano.</td><td>Mwanafunzi:<br>• atambue muundo wa baruapepe kwa kurejelea kielelezo chake kilichochapishwa au kwenye tarakilishi.<br>• ajadili sehemu mbalimbali za baruapepe kama vile anwanipepe ya mtumaji (k.m. tina18@gmail.com), anwanipepe ya mpokeaji, mada ya baruapepe, mtajo, mwili, hitimisho na jina la mwandishi/mtumaji.<br>• aandike baruapepe kwa rafiki, mzazi, mwalimu n.k akishirikiana na wenzake darasani, kwa kutumia tarakilishi akizingatia muundo wa uandishi wa baruapepe.<br>• aandike baruapepe akiwa peke yake.<br>• atume baruapepe aliyoiandika kwa mpokeaji.<br>• ajadiliane na wenzake kuhusu umuhimu wa baruapepe katika mawasiliano.</td><td>1. Unazingatia vipengele gani unapoandika baruapepe?</td></tr>
<tr><td colspan="5">Umilisi wa Kimsingi unaokuzwa<br>• Mawasiliano na ushirikiano-anapoandika na kutuma baruapepe.<br>• Ujuzi wa kidijitali- anapotumia tarakilishi kuandika na kutuma baruapepe.</td></tr>
<tr><td colspan="3">Uhusiano na Masuala Mtambuko<br>• Stadi za maisha – anapotumia baruapepe kuwasiliana.<br>• Elimu kwa maendeleo endelevu – anapotumia teknolojia kuwasiliana</td><td colspan="2">Uhusiano na Maadili<br>• Upendo – anapotuma baruapepe kwa wazazi au marafiki kuwajulia hali.<br>• Heshima – anapozingatia maoni ya wengine wakati wa mijadala.<br>• Uwajibikaji – anapotunza tarakilishi anayoitumia katika uandishi wa baruapepe.</td></tr>
<tr><td colspan="3">Uhusiano na masomo mengine<br>• Masomo yote yanayoshughulikia ujuzi wa kidijitali</td><td colspan="2">Shughuli za kijamii zinazochangia ujifunzaji<br>• Anapotumia tarakilishi kuwaandikia wazazi na marafiki baruapepe.<br>• Anapowashirikisha wenzake shuleni na nyumbani katika uandishi wa baruapepe.</td></tr>
</table>

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kuandika baruapepe kwa kuzingatia ujumbe, muundo na mtindo na kuituma. | Mwanafunzi anaandika baruapepe kwa urahisi kwa kuzingatia ujumbe, muundo na mtindo na kuituma. | Mwanafunzi anaandika baruapepe kwa kuzingatia ujumbe, muundo na mtindo na kuituma. | Mwanafunzi anaandika baruapepe kwa kuzingatia ujumbe na baadhi ya vipengee vya kimuundo na kimtindo na kuituma. | Mwanafunzi anajaribu kuandika baruapepe bila kuzingatia ujumbe, muundo na mtindo. |

| MADA | MADA NDOGO | MATOKEO MAALUM YANAYOTARAJIWA | MAPENDEKEZO YA SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI | MASWALI DADISI |
|---|---|---|---|---|
| **11.4**<br><br>**Sarufi** | **11.4.1 Ukanushaji wa maneno na sentensi:** Viambishi vya nafsi na wakati katika sentensi (Vipindi 3) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua viambishi vya wakati na nafsi katika sentensi<br>b) kukanusha viambishi vya nafsi na wakati katika maneno na sentensi kwa usahihi<br>c) kutunga sentensi sahihi zenye viambishi vya nafsi na wakati na kuzikanusha<br>d) kufurahia ukanushaji wa viambishi vya nafsi na wakati katika sentensi. | Mwanafunzi:<br>• atambue viambishi vya nafsi (*ni, tu, u, m, a, wa)* na vya wakati (*li, na, ta)* katika vitenzi kwa kuvipigia mistari kwenye vitabu au kuvikolezea wino kwenye tarakilishi<br>• atambue viambishi vya wakati *li, na, ta* katika hali yakinishi na *ku, ta, si, ha*, katika hali kanushi<br>• asome sentensi zenye viambishi lengwa kwenye vitabu au tarakilishi katika hali yakinishi na kanushi<br>• akanushe maneno na sentensi akizingatia nafsi na nyakati kwenye daftari au kwa kutumia tarakilishi<br>• asikilize au kutazama vipindi vya ukanushaji wa nafsi na wakati kupitia vyombo vya kidijitali. | 1) Viambishi vya nafsi katika vitenzi ni vipi?<br>2) Viambishi vya wakati katika vitenzi ni vipi?<br>3) Unatumia viambishi gani wakati wa kukanusha vitenzi? |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**:
- Mawasiliano na ushirikiano – kujadili kwenye vikundi
- Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo - mwanafunzi anapojaribu kukanusha maneno na sentensi
- Ujuzi wa kidijitali - mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali katika somo

| | |
|---|---|
| **Uhusiano na Masuala Mtambuko**:<br>• Stadi za Maisha - mwanafunzi anakuza uwezo wa kukabili au kukataa mambo mbalimbali maishani | **Uhusiano na Maadili:**<br>• Heshima na ushirikiano – mwanafunzi anaposhiriki katika kazi za vikundi |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**:<br>• English na Indigenous Languages – Masomo haya hushughulikia mada ya sarufi. | **Mapendekezo ya shughuli za huduma za Kijamii zinazochangia ujifunzaji**:<br>• Mwanafunzi anakuwa kielelezo kwa wenzake katika kutumia Kiswahili ifaavyo. |

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kutambua viambishi vya nafsi na wakati katika maneno na kukanusha maneno na sentensi kwa kuzingatia wakati na nafsi kwa usahihi. | Mwanafunzi anatambua viambishi vya nafsi na wakati katika maneno na kukanusha maneno na sentensi kwa kuzingatia wakati na nafsi kwa usahihi na urahisi. | Mwanafunzi anatambua viambishi vya nafsi na wakati katika maneno na kukanusha maneno na sentensi kwa kuzingatia wakati na nafsi kwa usahihi. | Mwanafunzi anatambua baadhi ya viambishi vya nafsi na wakati katika maneno na kukanusha maneno na sentensi alizotambua kwa kuzingatia wakati na nafsi kwa usahihi. | Mwanafunzi anatambua baadhi ya viambishi vya nafsi na wakati katika maneno na kukanusha baadhi ya maneno na sentensi kwa kuzingatia wakati na nafsi kwa usahihi. |

| MADA | MADA NDOGO | MATOKEO MAALUM YANAYOTARAJIWA | MAPENDEKEZO YA SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI | SWALI DADISI |
|---|---|---|---|---|
| **11.4 Sarufi** | **11.4.2 Ukubwa na udogo wa nomino:** Nomino zinazoanza kwa **m-** na zenye mzizi wa silabi mbili (Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua nomino zinazoanza kwa herufi **m-** na zenye mzizi wa silabi mbili<br>b) kutambua nomino zinazoanza kwa herufi **m-** katika hali ya ukubwa na udogo<br>c) kubadilisha nomino katika hali wastani kuwa katika hali ya ukubwa na udogo<br>d) kutumia nomino zinazoanza kwa herufi **m-** katika hali ya ukubwa na udogo kwenye sentensi<br>e) kufurahia kutumia nomino katika hali ya ukubwa na udogo kwa usahihi ili kuimarisha mawasiliano. | Mwanafunzi:<br>• atambue nomino zinazoanza kwa herufi **m-** na zenye mzizi wa silabi moja *(k.m mtoto, mlango, mkate na mlima)* kwenye chati, ubao, mti maneno, kapu la maneno au kifaa cha kidijitali.<br>• atambue nomino zinazoanza kwa herufi **m-** na zenye mzizi wa silabi moja katika ukubwa na udogo (k.v. mtoto (toto- kitoto), mlango (lango - kilango), mkate (kate- kikate)<br>• ashiriki katika vikundi kubadilisha nomino kutoka hali ya wastani hadi hali ya ukubwa na udogo.<br>• ashiriki katika mchezo wa vikundi ambapo kikundi kimoja kitataja wastani wa nomino na kingine kutaja ukubwa na udogo wa nomino hiyo.<br>• apewe orodha ya nomino katika hali ya ukubwa na orodha nyingine ya nomino katika hali ya udogo kwenye tarakilishi ili aziburure kuziambatanisha.<br>• atunge sentensi zinazorejelea nomino lengwa katika ukubwa na udogo akiwa peke yake au kwenye vikundi. | 1. Ni nomino gani unazoweza kutaja ukubwa wake? |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano – wanafunzi wanaposhiriki mijadala kuhusu nomino katika ukubwa na udogo
- Ubunifu – unadhihirika mwanafunzi anapotunga sentensi katika hali ya ukubwa na udogo
- Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anatumia tarakilishi kutambua na kuambatanisha nomino katika hali ya wastani, ukubwa na udogo

| **Uhusiano na Masuala Mtambuko** | **Uhusiano na Maadili** |
|---|---|
| • Uraia – kutunga sentensi zinazolenga uraia mwema. | • Ushirikiano- wanafunzi wanapofanya kazi katika makundi |
| **Uhusiano na Masomo Mengine** | **Mapendekezo ya shughuli za huduma za Kijamii zinazochangia ujifunzaji:** |
| • English na Indigenous Language - Masomo haya hushughulikia mada ya sarufi | • Mwanafunzi atakuwa kielelezo cha kutumia lugha kwa ufasaha shuleni na nyumbani. |

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango<br>Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kutambua nomino zinazoanza kwa herufi **m-** za mzizi wa silabi mbili. | Mwanafunzi anatambua nomino zinazoanza kwa herufi **m-** za mzizi wa silabi mbili kwa urahisi. | Mwanafunzi anatambua nomino zinazoanza kwa herufi **m-** za mzizi wa silabi mbili. | Mwanafunzi anatambua baadhi ya nomino zinazoanza kwa herufi **m-** za mzizi wa silabi mbili. | Mwanafunzi anajaribu kutambua baadhi ya nomino zinazoanza kwa herufi **m-** za mzizi wa silabi mbili. |
| Kutambua nomino katika hali ya ukubwa na udogo na kutumia nomino hizo katika hali ya ukubwa na udogo kwenye sentensi kwa usahihi | Mwanafunzi anatambua nomino katika hali ya ukubwa na udogo, anatumia nomino katika hali ya ukubwa na udogo kwenye sentensi kwa usahihi na kwa urahisi. | Mwanafunzi anatambua nomino katika hali ya ukubwa na anatumia nomino katika hali ya ukubwa na udogo kwenye sentensi kwa usahihi. | Mwanafunzi anatambua baadhi ya nomino katika hali ya ukubwa na udogo na anatumia nomino alizotambua kwenye sentensi kwa usahihi. | Mwanfunzi anatambua baadhi ya nomino katika hali ya ukubwa na udogo na anatumia baadhi ya nomino alizotambua kwenye sentensi kwa usahihi. |

<table>
<tr><th>MADA</th><th>MADA NDOGO</th><th>MATOKEO MAALUM YANAYOTARAJIWA</th><th>MAPENDEKEZO YA SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI</th><th>SWALI DADISI</th></tr>
<tr><td>11.4<br>Sarufi</td><td>11.4.3 Ukubwa na udogo wa nomino: Ukubwa na udogo wa nomino zinazoanza kwa kwa herufi n<br>(Vipindi 2)</td><td>Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua nomino zinazoanza kwa herufi n- ili kuzitofautisha na nonimo nyingine<br>b) kutambua nomino zinazoanza kwa herufi n- katika hali ya ukubwa na udogo<br>c) kubadilisha nomino katika hali wastani kuwa katika hali ya ukubwa na udogo<br>d) kutumia nomino katika hali ya ukubwa na udogo kwenye sentensi<br>e) kufurahia kutumia nomino katika hali ya ukubwa na udogo kwa usahihi ili kuimarisha mawasiliano.</td><td>Mwanafunzi:<br>• atambue nomino zinazoanza kwa herufi n- kwenye chati, ubao, mti maneno, kapu la maneno au kifaa cha kidijitali.<br>• ashiriki katika vikundi kubadilisha nomino kutoka hali ya wastani hadi hali ya ukubwa na udogo.<br>• ashiriki katika mchezo wa vikundi ambapo kikundi kimoja kitataja wastani wa nomino, kingine ukubwa na kingine kutaja udogo wa nomino hiyo.<br>• apewe orodha ya nomino katika hali ya ukubwa na orodha nyingine ya nomino katika hali ya udogo kwenye tarakilishi ili aziburure kuziambatanisha.<br>• atunge sentensi zinazorejelea nomino lengwa katika ukubwa na udogo akiwa peke yake au kwenye vikundi.</td><td>1. Ni nomino gani unazoweza kutaja udogo wake?</td></tr>
<tr><td colspan="5">Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa<br>• Mawasiliano na ushirikiano - wanafunzi wanaposhiriki mijadala kuhusu mada hii<br>• Ubunifu- unadhihirika wamapotunga sentensi katika hali ya udogo<br>• Ujuzi wa kidijitali – mwanafunzi anatumia tarakilishi kutambua na kuambatanisha nomino katika hali wa wastani na udogo</td></tr>
<tr><td colspan="3">Uhusiano na Masuala Mtambuko<br>• Uraia – kutunga sentensi zinazolenga uraia mwema.</td><td colspan="2">Uhusiano na Maadili<br>Ushirikiano- kufanya kazi katika makundi</td></tr>
<tr><td colspan="3">Uhusiano na Masomo Mengine<br>• English Activities na Indigenous Language - Masomo haya hushughulikia sarufi</td><td colspan="2">Mapendekezo ya shughuli za huduma za Kijamii zinazochangia ujifunzaji:<br>• Mwanafunzi atakuwa kielelezo cha kutumia lugha kwa ufasaha shuleni na nyumbani.</td></tr>
</table>

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kutambua nomino zinazoanza kwa herufi **n** kwa urahisi | Mwanafunzi anatambua nomino zinazoanza kwa herufi **n** kwa urahisi na wepesi. | Mwanafunzi anatambua nomino zinazoanza kwa herufi **n** kwa urahisi. | Mwanafunzi anatambua baadhi ya nomino zinazoanza kwa herufi **n** kwa urahisi. | Mwanafunzi anajaribu kutambua baadhi ya nomino zinazoanza kwa herufi **n**. |
| Kutambua nomino katika hali ya ukubwa na udogo na kutumia nomino katika hali hizo kwenye sentensi kwa usahihi | Mwanafunzi anatambua nomino katika hali ya ukubwa na udogo na anatumia nomino katika hali hizo kwenye sentensi kwa usahihi na kwa urahisi. | Mwanafunzi anatambua nomino katika hali ya udogo na anatumia nomino katika hali hizo kwenye sentensi kwa usahihi. | Mwanafunzi anatambua baadhi ya nomino katika hali ya ukubwa na udogo na anatumia nomino alizotambua kwenye sentensi kwa usahihi. | Mwanfunzi anatambua baadhi ya nomino katika hali ya ukubwa na udogo na anatumia baadhi ya nomino alizotambua kwenye sentensi kwa usahihi. |

**MUHTASARI WA MBINU ZA KUTATHMINI, NYENZO ZA KUFUNDISHIA NA MAPENDEKEZO YA SHUGHULI NYINGINE ZILIZORATIBIWA ZA UJIFUNZAJI**

| MADA | MAPENDEKEZO YA MBINU ZA KUTATHMINI | MAPENDEKEZO YA NYENZO ZA KUFUNDISHIA | MAPENDEKEZO YA SHUGHULI NYINGINE ZILIZORATIBIWA ZA UJIFUNZAJI |
|---|---|---|---|
| 1.0 KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA | a) Kumakinikia jinsi mwanafunzi anavyotumia lugha katika mawasiliano<br>b) Kujibu maswali<br>c) Maigizo<br>d) Kutambua k.m. kwenye orodha<br>e) Kuambatanisha maneno na majibu<br>f) Mijadala<br>g) Mazungumzo<br>h) Matumizi ya ishara za mwili k.v ishara za uso, za mikono na mabega kuimarisha masimulizi yake<br>i) Wanafunzi kufanyiana tathmini | • Chati<br>• Michoro na picha<br>• Mgeni mwalikwa<br>• Vifaa vya kidijitali (k.v tarakilishi/vipakatalishi, kinasasauti, rununu, projekta, video)<br>• Mti maneno<br>• Kapu maneno<br>• Vitabu mbalimbali | 1. Kazi ya vikundi<br>2. Vyama vya ushirika shuleni<br>3. Mijadala inayohusu masuala mtambuko mbalimbali<br>4. Ziara za nyanjani<br>5. Kutagusana na vyombo vya habari na vifaa vingine vya kidijitali |
| KUSOMA | a) Kutunga sentensi k.m. kwa kutumia msamiati lengwa<br>b) Kujibu maswali k.m. katika ufahamu<br>c) Kutoa muhtasari wa ufahamu au matini yaliyosomwa<br>d) Kukariri na kuimba mashairi<br>e) Kusoma kwa sauti<br>f) Wanafunzi kufanyiana tathmini<br>g) Potfolio<br>h) Shajara | • Tarakilishi/vipakatalishi<br>• Kinasasauti<br>• Rununu<br>• projekta<br>• Tarakilishi/vipakatalishi<br>• Kinasasauti<br>• Rununu<br>• projekta<br>• Nakala ya shairi<br>• Kamusi mbalimbali | 1. Kazi ya vikundi<br>2. Vyama vya ushirika shuleni<br>3. Mijadala inayohusu masuala mtambuko mbalimbali<br>4. Ziara za nyanjani<br>5. Kutagusana na vyombo vya habari na vifaa vingine vya kidijitali |

| | | | |
|---|---|---|---|
| KUANDIKA | a) Kuandika tungo mbalimbali<br>b) Wanafunzi kufanyiana tathmini<br>c) Potfolio<br>d) Shajara<br>e) Mijadala kuhusu vidokezo vya insha | • Kielelezo cha insha ya masimulizi<br>• Kielelezo cha insha ya maelezo<br>• Kielelezo cha insha ya wasifu<br>• Nakala ya barua ya kirafiki<br>• Nakala ya barua rasmi | 1. Kazi ya vikundi<br>2. Vyama vya ushirika shuleni<br>3. Mijadala inayohusu masuala mtambuko mbalimbali<br>4. Ziara za nyanjani<br>5. Kutagusana na vyombo vya habari na vifaa vingine vya kidijitali |
| SARUFI | a) Kutambua k.m. kwenye orodha<br>b) Kuambatanisha maneno lengwa<br>c) Kujaza mapengo<br>d) Kujaza fumbo maneno<br>e) Kazi mradi | • Tarakilishi/vipakatalishi<br>• Kinasasauti<br>• Rununu<br>• projekta<br>• Kapu maneno<br>• Mti maneno<br>• Kadi za maneno<br>• Picha za vitu mbalimbali<br>• Michoro<br>• Chati<br>• Mabango<br>• Sanamu<br>• Nyenzo halisi | 1. Kazi ya vikundi<br>2. Vyama vya ushirika shuleni<br>3. Ziara za nyanjani<br>4. Kutagusana na vyombo vya habari na vifaa vingine vya kidijitali |